

**DISKOSI YA MAFUNZO YA TENDO LA NDOA KATIKA JANDO  
MIONGONI MWA WAKIPSIGIS NCHINI KENYA**

**KIRUI NICHOLAS KIMUTAI**

Tasnifu hii imewasilishwa katika Shule ya Mafuzu ili kutimiza mahitaji ya  
Shahada ya Uzamili katika Kiswahili na Mawasiliano ya Chuo kikuu cha  
Laikipia.

**OKTOBA, 2024**

## UNGAMO NA IDHINI

### **Ungamo**

Tasnifu hii ni kazi yangu na haijawahi kuwasilishwa tena kwa mahitaji ya shahada ingine katika chuo chochote.

Sahihi: \_\_\_\_\_ Tarehe: \_\_\_\_\_

Kirui Nicholas Kimutai

MK22/2517/18

### **Idhini**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi ili kutimiza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Kiswahili na Mawasiliano Chuo Kikuu cha Laikipia.

Sahihi: \_\_\_\_\_ Tarehe: \_\_\_\_\_

Prof. James Ogola Onyango

Idara ya Usomilugha na Mawasiliano

**Chuo Kikuu cha Laikipia**

Sahihi: \_\_\_\_\_ Tarehe: \_\_\_\_\_

Dkt. Sheila Wandera Simwa

Idara ya Usomilugha na Mawasiliano

**Chuo Kikuu cha Laikipia**

## **HAKIMILIKI**

Haki zote zimehifadhiwa na ni hatia kunakili kazi hii kwa njia yoyote ile bila idhini ya mwandishi au chuo kikuu cha Laikipia.

*Kirui Nicholas Kimutai ©2024*

## **TABARUKU**

Naitabaruku tasnifu hii mamangu Dinah Tonui na marehemu babangu Francis Tonui.

## SHUKRANI

Kufaulu kwa utafiti huu kulihusisha watu wengi. Nitakuwa mchache wa fadhila iwapo sitawashukuru. Awali ya yote, namshukuru Rabuka kwa kunipa uwezo wa kuendelea na masomo yangu. Pili, nawashukuru waelekezi wangu Prof. James Onyango Ogolla, Dkt. Sheila Wandera Simwa na Marehemu Dkt. James Gwachi Mayaka kwa nasaha zao ambazo zimekuwa mwanga wa kuikamilisha kazi hii. Ushauri wao ulinipa moyo wa kukamilisha kazi hii. Tatu, ninawashukuru wahadhiri wangu wa kozi ya uzamili; Prof. James Onyango Ogolla, Marehemu Dkt. James Gwachi Mayaka, Prof. Wendo Nabea, Dkt. Sheila Simwa Wandera na Marehemu Prof. Francis Aswani Buliba. Tunu za elimu nilizopata kwao zimenifaa sana katika kazi hii. Nne, wazamili wenzangu; Lucy Mugo, Simon Wanjohi, Mburu wa Kamau, Kerryann Mburu na Peter Kamau natoa shukrani sufufu kwa ushirikiano wenu katika kuwezesha mijadala mbalimbali ya kiusomi chuoni. Tano, nawashukuru pia wote waliokosoa tasnifu hii. Hatimaye, mamangu, ndugu yangu Vincent Kirui na dadangu Daisy Chemutai na rafiki yangu Betty Chebet Mutai pokeeni shukrani zangu za dhati kwa kunipa moyo na kunihimiza kuendeleza masomo yangu. Ni wengi ambao walinifaa japo sijaweza kuwataja kwa majina. Naomba radhi na kuwashukuru sana. Nyote nawaombea Baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

## IKISIRI

Miviga za jandoni ni mojawapo ya tanzu za fasihi simulizi. Utanzu huu hutumiwa kupitisha mafunzo kuhusu masuala ya ngono kwa wavulana wakiwa jandoni. Mafunzo yanayohusu tendo la ndoa katika jamii yoyote huwa nyeti. Hata hivyo, hayazungumzwi hadharani. Yanapojitokeza katika kauli za wanajamii, huwasilishwa kwa mikakati mahususi ya kujaribu kuuficha uwazi huo. Ingawa wataalamu mbalimbali wamechunguza diskosi za tendo la ndoa katika nyanja tofauti tofauti, uchanganuzi wa diskosi za tendo la ndoa katika muktadha wa jandoni haujafanyiwa utafiti wa kina. Utafiti huu hivyo basi, ulidhamiria kuchanganua diskosi za tendo la ndoa zinavyojitokeza katika mafunzo ya jandoni katika jamii ya Wakipsigis. Malengo ya utafiti yalikuwa kuchanganua mada za diskosi za tendo la ndoa na kutathmini mikakati inayotumiwa katika mafunzo ya diskosi za tendo la ndoa katika shughuli za jando. Utafiti huu ulielekezwa na Nadharia ya Diskosi hasa kwa Mkabala wa Historia. Mihimili ya nadharia hii ni mikakati ya; urejelezi, uarifishaji, ubishi, mikabala, kuongeza na kufifisha makali ya usemi. Asilimia kubwa ya utafiti huu ilikuwa ya nyanjani, kwa ajili ya kukusanya data ya kimsingi. Aidha, mtafiti alihusisha utafiti wa maktabani ili kupata michango ya wataalamu wa awali kuhusu suala hili. Data ilikusanywa kwa njia ya mahojiano, kurekodi, picha na majadiliano. Jamii ya Wakipsigis ndio ilikuwa kundi lengwa la utafiti huu na mafunzo yanayohusu suala la tendo la ndoa jandoni yalilengwa. Data ya utafiti huu iliwasilishwa na kuchanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo ili kudadavua matokeo ya utafiti. Utafiti huu ulifanyika katika eneo la Bomet wanakoishi asilimia kubwa ya Wakipsigis. Ngariba watatu waliteuliwa kutoka maeneo matatu makuu ambayo ni Kaunti ndogo za Chepalungu, Bomet Mashariki na Sotik. Maeneo haya yaliteuliwa kwa kuwa yana utamaduni asilia ambao haujaathiriwa na tamaduni za kigeni na usasa. Sampuli ya utafiti huu ilihusisha kuteua watahiriwa wawili kutoka mfumo wa rika saba inayopatikana kwa jamii hiyo ili kupata data ya kutegemewa. Matokeo ya utafiti yameonyesha kwamba mada zinazozungumziwa ni; idhini ya kushiriki ngono, jinsi ya kushiriki tendo la ngono, washiriki katika tendo la ngono, unyeti na maadili katika tendo la ndoa. Baadhi ya mikakati inayotumiwa kupitisha mada hizi ni kama vile; jazanda, taashira, tasfida, sitiari, nyimbo na istihizai. Utafiti huu ulinuia kuongeza maarifa kwa wasomi, wahakiki na watafiti wa masuala ya uchanganuzi usemi. Matokeo ya utafiti huu yatafaa wataalamu wa lugha, wachanganuzi wa diskosi na utachangia kuelewa suala la diskosi katika muktadha wa jinsia. Aidha, utafiti huu utawaauini washikadau wote wanaohusika katika kubuni sera zinazohusiana na jinsia..

## ABSTRACT

Initiation ceremony is a very crucial avenue for advising initiates on matters of sexuality. Though sexuality in most African communities is a taboo issue that is rarely openly discussed, a number of scholars have written on discourse analysis in different fields. In this aspect not much has been done on sexuality discourse in the initiation context among the Kipsigis community. This study therefore, seeks to unravel the sexuality discourses in initiation context of the Kipsigis community. The specific objectives of this research was to discuss the themes of sexuality discourses and to evaluate modes of expressing sexuality discourses during Kipsigis initiation rites. This research was guided by the Discourse-Historical Approach (DHA) theory guided by these pillars: Referential, predicational, argumentation, perspectivation, intensification and mitigation. The data for this research was collected from the library and in the field. At the library the researcher read articles, journals and books from different scholars on internet. At the field, the researcher interacted with the community while collecting data. The researcher used two methods of collecting data that is interview and discussions. Field work research was aided by a recording device called a digital tape recorder. The taped teachings were transcribed in order to identify sexuality discourse topics and strategies used to teach them. The target population was the Kipsigis community and all the topics taught during seclusion. This research dealt with discourses of sexuality taught during male initiation in Kipsigis community. The main place of research was Bomet County, where the Kipsigis community lives. Only three subcounties of Bomet County were selected to represent whole county, these were: Chepalungu, Bomet east and Sotik sub-counties. One specialist from each region was picked. The selection of these subcounties were based on cultural consideration since they have not been affected by urbanization. In order to get accurate data, this research also picked two initiates from the seven age sets. Some of the outcomes of this research revealed that the themes taught are; permission to engage into sexual intercourse, how to engage into sexual affair, persons with whom to engage sexual affairs with and ethics to consider during sexual affair. Some of the strategies used to teach these topics are metaphors, euphemism, symbolism and sarcasm. The findings of this research will be reference point to discourse scholars and discourse analysts. It is anticipated that this research will create a deeper insight into sexuality discourses in gender context. Hopefully the findings will help the policy makers in formulation of policies and strategies that will address gender issues.

## YALIYOMO

UNGAMO NA IDHINI .....	ii
HAKIMILIKI.....	iii
TABARUKU .....	iv
SHUKRANI.....	v
IKISIRI .....	vi
ABSTRACT.....	vii
YALIYOMO.....	viii
UFAFANUZI WA ISTILAHU .....	x
<b>SURA YA KWANZA .....</b>	<b>1</b>
<b>UTANGULIZI.....</b>	<b>1</b>
1.1 Usuli wa Mada.....	1
1.2 Suala la Utafiti.....	5
1.3 Madhumuni ya Utafiti .....	5
1.4 Maswali ya Utafiti .....	5
1.5 Umuhimu wa Utafiti.....	6
1.6 Upeo na Mipaka .....	6
<b>SURA YA PILI.....</b>	<b>8</b>
<b>MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA .....</b>	<b>8</b>
2.1 Utangulizi .....	8
2.2 Yaliyoandikiwa kuhusu Diskosi za Mafunzo ya Jandoni.....	8
2.3 Mikakati ya Diskosi ya Tendo la Ndoa .....	14
2.4 Msingi wa Nadharia .....	21
2.4.1 Uchanganuzi Usemi-Mkabala wa Kihistoria.....	22
2.4.2 Mkakati wa Urejelezi/unominishaji .....	23
2.4.3 Mkakati wa Uarifishaji .....	23
2.4.4 Mkakati wa Mkabala .....	23
2.4.5 Mkakati wa Ubishi .....	23
2.4.6 Mkakati wa Ufifishaji na Uongezaji Makali .....	24
<b>SURA YA TATU.....</b>	<b>25</b>
<b>MBINU ZA UTAFITI.....</b>	<b>25</b>
3.1 Utangulizi .....	25
3.2 Muundo wa Utafiti .....	25
3.3 Mahali pa Utafiti.....	25
3.4 Njia za Utafiti .....	26
3.4.1 Utafiti Maktabani.....	26

3.4.2 Utafiti Nyanjani .....	26
3.5 Kikundi Lengwa .....	26
3.6 Sampuli.....	27
3.6.1 Mbinu za Kuteua Sampuli .....	27
3.6.2 Usampulishaji Lengwa .....	27
3.7 Mbinu za Kukusanya.....	28
3.8 Uchanganuzi wa Data.....	28
3.9 Tafsiri ya Data .....	30
3.10 Uzingativu wa Maadili .....	30
<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>31</b>
<b>UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA .....</b>	<b>31</b>
4.1 Utangulizi .....	31
4.2 Mada za Tendo la Ndoa.....	31
4.2.1 Idhini ya Kushiriki Tendo la Ndoa.....	33
4.2.2 Kiwango cha Kushiriki Tendo la Ndoa .....	40
4.2.3 Jinsi ya Kushiriki Tendo la Ndoa .....	42
4.2.4 Unyeti na Maadili ya Tendo la Ndoa .....	45
4.3 Mikakati Inayotumiwa katika Mafunzo .....	49
4.3.1 Jazanda .....	50
4.3.2 Mkakati wa Kitafida .....	55
4.3.3 Sitiari .....	58
4.3.4 Taashira .....	59
4.3.5 Nyimbo.....	63
4.3.6 Stihizai.....	64
<b>SURA YA TANO .....</b>	<b>66</b>
<b>MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....</b>	<b>66</b>
5.1 Utangulizi .....	66
5.2 Muhtasari wa Tasnifu.....	66
5.3 Matokeo ya Utafiti.....	66
5.4 Mapendekezo.....	67
5.5 Hitimisho .....	68
MAREJELEO .....	69
VIAMBATISHO.....	75

## UFAFANUZI WA ISTILAHU

**Diskosi:** imetumika kuonyesha usemaji au matamko na usimulizi wa jinsi sherehe za jando hufanyika katika jamii ya Kipsigis.

**Itikadi:** imetumika kwa maana ya kanuni na imani ambazo huongoza mfumo wa maisha. Katika utafiti huu, tunarejelea mila na desturi za Wakipsigis.

**Jamii:** ni watu wanaoishi pamoja na wanaotofautiana na watu wengine kwa msingi wa lugha na kaida. Kwa mujibu wa utafiti huu, tunarejelea jamii ya Wakipsigis.

**Jando:** mahali ambapo watoto wa kiume hukaa na kutahiriwa ambapo hupata mafunzo kuhusu maisha.

**Mafundisho ya jandoni:** elimu inayopeanwa katika eneo la kitamaduni wakati wa kutahiriwa.

**Miviga:** ni sherehe zinazofanyika kila mwaka, katika utafiti huu ni wakati wa tohara ya wavulana wa jamii ya Kipsigis. Sherehe hizi huandamana na matambiko ya kitamaduni katika sherehe za tohara.

**Rika:** watu wenye umri unaokaribiana ambao walifuzu katika shughuli za jando kwa kipindi kimoja. Katika utafiti huu tunajikita kwa watu kutoka jamii ya Wakipsigis ambao wamefuzu tohara.

**Tendo la ndoa:** kitendo cha kujamiiana kinachofanywa baina ya mwanamume na mwanamke.

**Topoi:** mahitimisho yanayotokana na uhakiki wa yaliyomo kwenye usemi, tamko au kauli ya msemaji. Mahitimisho haya hujengwa na kuendelezwa na vidokezo na viarifu vya semi.

**Ubabedume:** imetumika kurejelea uwezo na mamlaka ya jinsia ya kiume katika jamii ambayo hujengwa na kushamirishwa na sifa za: uhuru, udhabiti, nguvu, ushujaa, uwezo wa kutawala, mamlaka ya kuamuru na kuongoza.

## SURA YA KWANZA

### UTANGULIZI

#### 1.1 Usuli wa Mada

Utafiti huu ulikuwa wa uchanganuzi wa diskosi katika fasihi simulizi kipera cha miviga katika Kaunti ya Bomet wanakoishi jamii ya Wakipsigis. Vijana hupata mafunzo kuhusu masuala ya tendo la ndoa wanapokuwa jandoni na hutarajiwa kuyatumia maishani. Mafunzo haya yanalenga kulifanya tendo la ndoa wakati wa ndoa liwe la kufurahisha. Kipsigis ni kabila la Waniloti wanaoishi Kenya. Wakipsigis ni watu wa kabila la Wakalenjin na wanazungumza lahaja ya lugha ya Kalenjin inayotambulika kwa jina la jamii yao. Wakipsigis walitoka eneo la Misiri, na kufikia karne ya 19, walikuwa wameishi katika Bonde la Ufa. Wakipsigis ndio wengi zaidi kati ya Wakalenjin. Sensa ya karibuni iliyofanyika nchini Kenya mwaka wa 2019; ilionyesha kuwepo kwa jumla ya milioni 1.972 ya watu wanaozungumza Kikalenjin ambao ni asilimia 45% ya idadi ya wazungumzaji wote wa lugha hiyo. Kikalenjin. Wanamiliki sehemu za Bomet, nyanda za juu za Kericho zinazoanzia Timboroa hadi mto Mara upande wa kusini, magharibi mwa msitu wa Mau. Pia wanamiliki sehemu za Laikipia, Kitale, Nakuru na Narok.

Tafiti kuhusu masuala ya lugha na jinsia zimeegemea sana upande wa ufeministi, kwa hivyo suala la lugha, tendo la ndoa, ni la karibuni kutokana na unyeti unaohusiana na suala hili. Mijadala kuhusu tendo la ndoa huwa nyeti na wengi huchelea kuizungumzia kwa uwazi na aghalabu huchukuliwa kuwa ni miiko katika jamii. Hili limechangia katika uhaba wa tafiti kuhusu masuala haya ya lugha na tendo la ndoa. Hivyo basi utafiti huu ulijikita katika fasihi simulizi utanzu wa maigizo kijipera cha miviga ili kubaini jinsi mafunzo yanayohusiana na tendo la ndoa yanavyopitishwa kwa watahiriwa katika jamii ya Wakipsigis.

Kuzungumzia suala la tendo la ndoa kwa lugha ya wazi huchukuliwa huwa ni mwiko kwa hivyo ni wataalamu wachache tu wakiwemo Moore na Rosenthal (1993) ambao wamezungumzia elimu kuhusu tendo la ndoa. Wasomi hawa wanaeleza kwamba tabia nzuri na mahusiano mema katika tendo la ndoa yatafanikiwa iwapo wakufunzi watatekeleza majukumu yao kwa walengwa. Aidha, wanaeleza kwamba ujuzi wa suala hili husaidia katika kubadili tabia na mienendo. Undie na wenzake (2006) walisisitiza kwamba mienendo ya kutumbua lugha ya tendo la ndoa, muktadha na utamaduni huwa

nguzo muhimu sana. Wanadai kwamba lugha ni kigezo muhimu cha kuelewa jinsi mafunzo ya tendo la ngono na masuala mengine ya kujamiana yanapitishwa kwa wanajamii. Nkumbo (2013) ameeleza kwamba masuala yanayohusiana na tendo la ngono hayawekwi wazi katika tamaduni nyingi za jamii nyingi za Kiafrika kwa sababu ni ya mwiko na iwapo yatazungumziwa huwa katika miktadha maaalum. Kwa jumla, elimu kuhusu tendo la ndoa ni muhimu ndiposa pawe na aila zilizo na misingi thabiti katika aushi ya ndoa. Wasomi hawa wanatilia mkazo dhana ya kutumia lugha katika miktadha maalum ya tamaduni. Hali hii husaidia katika uelewa wa masuala ya tendo la ndoa miongoni mwa wanajamii hasa wavulana wanapokuwa jandoni.

Mafunzo ya jandoni miongoni mwa wavulana yanaendana na tohara ya wasichana kwa baadhi ya jamii ambazo zinaruhusu tohara ya wasichana. Wavulana kwa wasichana hupata mafunzo kuhusu maadili kama vile kuheshimu wakubwa, kuwa jasiri, kuwajibika, majukumu ya kutunza familia na kudumisha mila na tamaduni (Undie na wenzake, 2006). Mafunzo ya jando na unyago hunuia kuwaandaa vijana kuingia katika majukumu ya utu uzima. Baada ya kuhitimu, wanajamii wanawatarajia vijana kuwa na uwezo wa kujitolea kutetea haki za wanyonge, kuchuma na kupiga vita uharibifu na mizozo miongoni mwa familia. Kimsingi, mafunzo hayo yanawasaidia vijana kujitambua na kutambua mabadiliko katika ukuaji wao.

Masuala ya jando hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine kutokana na maendeleo ya sayansi, teknolojia na dini miongoni mwa mambo mengine. Kila jamii huwa na sababu za kipekee za kutahiri na sababu hizo zinaandamana na mafunzo ya jandoni. Katika nchi za Bara Uropa tohara hufanywa kwa manufaa ya kiafya na kuzuia kuenea kwa magonjwa kama Ukimwi. Mashirika mbalimbali kama vile World Health Organization yamejaribu kutoa mafunzo kuhusu umuhimu wa tohara na pia kupiga marufuku baadhi ya vitendo hasi vinavyohusiana na tohara ya wasichana na wavulana.

Barani Afrika, mafunzo ya jando huambatana na sherehe za miviga. Japo dini hupinga vikali mafunzo na shughuli za jandoni, bado sherehe hizo hufanywa. Karugendo (2009) anaeleza kuwa dini ni mojawapo wa asasi zinazopiga vita tamaduni za unyago na jando. Kwa sababu dini hizi ni za kigeni zilichangia kuleta utamaduni mpya na kujaribu kuzika tamaduni za Kiafrika. Mwelekeo huu unaungwa mkono na viongozi wengi wa dini ambao wanasisitiza mafunzo yanayomjenga mwanajamii kwa misingi ya kidini. Katika taifa la Tanzania Gazeti la *Mwananchi*, 10 oktoba 2010 lilieleza jinsi mkuu wa Wilaya

alipiga marufuku wananchi kuhudhuria sherehe za jando huku akiwarai wahudhurie mkutano wa kisiasa. Hii ilidhihirisha kwamba wakuu wa elimu na wanasiasa hawakuwa wakithamini sherehe za jando na unyago.

Kwa kawaida wavulana hupelekwa jandoni ambako huwa kama shule ya kitamaduni ambapo watahiriwa hutengwa na jamii kwa siku kadhaa. Kutengwa kwao ni kwa ajili ya kupata mafunzo kuhusu mada mbalimbali za kimaishahasa kuhusu tendo la ndoa. Mafunzo haya ya tendo la ndoa huhusisha diskosi za tendo la ndoa ili kufanikisha malengo yake. Uchanganuzi wa diskosi za jandoni katika tamaduni nyingi za Kiafrika hujenga na kushamiri uhusiano wa kiuwezo na utawala katika jamii (Laclau na Mouffe, 1985). Diskosi za tendo la ndoa jandoni huchangia dhana ya ubabedume miongoni mwa wavulana. Kwa sababu tohara ni njia ya kupita kutoka utotoni hadi utu uzima miongoni mwa jamii ya Wakipsigis mafunzo ya utu uzima hufunzwa watahiriwa kwa lengo la kuwafanya wawe watu wazima baada ya sherehe hizo za tohara.

Nchini Kenya, jamii nyingi huheshimu shughuli za jando na hutenga kipindi maalum katika kila mwaka (miviga) kwa lengo la kushiriki katika mchakato huo. Kwa mujibu wa Mang'uliechi (2007), Wabukusu wameipa tohara umuhimu mkubwatangu jadi. Inakisiwa kwamba sherehe hii ilianza zaidi ya miaka mia tatu iliyopita. Katika sherehe hizo, mafunzo yanayoambatana na nyimbo hufunzwa ili kutekeleza wajibu maalum kama kuonya, kuadilisha, kukashifu, kuburudisha na kuelimisha. Mutwiri (2005), alifanya utafiti wa mafunzo ya nyimbo za tohara katika jamii ya Watigania kwa kujikita katika mitazamo ya utendakazi wa nyimbo hizo za kiasili. Alieleza sababu za utamaduni kutokufa licha ya upinzani mkubwa uliopo kutokana na mwingiliano wa utamaduni wao na wa Kimagharibi.

Nyimbo huchukua sehemu kubwa katika miviga ya jamii mbalimbali. Wamitila, (2003). Ni katika muktadha huu ambapo utafiti huu ulichunguza majukumu ya nyimbo kwa mujibu wa miviga ya tohara za wavulana. Katika jamii ya Wakipsigis miviga ya tohara hutumika kama mbinu ya kupitisha mafunzo kuhusu tendo la ndoa. Miviga kama utanzu wa fasihi simulizi, una umuhimu wake katika jamii husika. Kupitia miviga, jamii husika huburidika, huelimika, huonywa na huadilika, Maendeleo na mabadiliko ya kijamii huathiri miviga kimaudhui, mtindo, vifaa na uwasilishaji. Aidha, miviga za tohara katika jamii ya Wakipsigis hutekelezwa katika mandhari mahususi ya sherehe za tohara, huwa na hadhira teule (watahiriwa) na matini bayana ili kutekeleza wajibu

wake barabara. Miviga ni utanzu unaotekeleza majukumu maalum katika jamii husika. Takribani shughuli zote za kijamii, mathalan kulima, kupalilia, kuwinda ndege, tohara, harusi na mazishi huandamana na miviga ya kitamaduni kila wakati, Wamitila (2003), Kieti na Coughlin (1990).

Katika kutafiti juu ya majukumu ya miviga ya tohara katika mafunzo ya tendo la ndoa, utafiti huu ulidhamiria kuweka wazi umuhimu wa miviga katika jamii ya Wakipsigis kufunza kuhusu tendo la ndoa. Miviga ya tohara katika jamii ya Wakipsigis huendelezwa wakati wavulana wanapopashwa tohara. Miviga hii imetengwa katika awamu mbili; inayoigizwa wakati wa kuandaa wavulana kuingia jandoni na inayoigizwa wavulana wakiwa Jandoni. Utafiti huu ulilenga miviga zote mbili ili kudavua mafunzo ya tendo la ndoa.

Fairclough (1995) anatofautisha dhana ya lugha na diskosi kwa kufafanua kwamba, chombo kinachotumika ili kuwasiliana ni lugha nayo njia ya kubainisha tendo fulani ni diskosi katika jamii.; Usemi, mazungumzo na mawasiliano ndivyo vigezo vya kutambua diskosi.

Halliday (1985) alitumia dhana ya diskosi katika urejelezi wa matini. Cameron (2001) anasema tafiti nyingi zimetumia matini za kusimulia na kuandikwa kama diskosi. Matumizi haya ya lugha semwa na andishi huzua utofauti katika fasili na ufasiri wa maana kwa vile hutegemea lugha katika muktadha. Huu ni uamilifu wa lugha. Uamilifu wa diskosi huweza kufasiriwa kwa njia mbili; kama kipengele cha maisha na kama njia ya kutazama ulimwengu. Utafiti huu, ulitumia ufasiri huu wa diskosi. Fairclough (2003) alibainisha diskosi kwa njia tatu; matini, zao la usemi na tendo la kijamii. Kwa hivyo anayetumia dhana ya diskosi hajikiti tu katika usemi bali pia matini anapochanganua data.

Mawaidha hupimwa ubora wake kwa kuzingatia mikakati ya usemi inayotumika kupitisha ujumbe kwa wasikilizaji. Mikakati ya usemi katika mawaidha hudhihirisha nyenzo ambazo mshauri ametumia kufanikisha maudhui yake. Tafiti mbalimbali zimedhibitisha kuwa lugha inayotumika katika diskosi za tendo la ndoa huwa ya kimafumbo na huonyesha taswira halisi ya maisha katika jamii. Picha halisi ya jamii hushamirishwa na fani mbalimbali za lugha. Kwa misingi hii mikakati ya diskosi katika

mafunzo ya tendo la ndoa jandoni ilitathminiwa ili kuweka wazi mada mbalimbali za ubabedume zinazojitokeza.

Katika Kaunti ya Bomet wanakoishi jamii ya Wakipsigis, vijana hupata mafunzo kuhusu masuala ya tendo la ndoa wanapokuwa jandoni na hutarajiwa kuyatumia maishani. Mafunzo haya yanalenga kulifanya tendo la ndoa wakati wa ndoa liwe la kufurahisha kwa wakati wowote. Hata hivyo, suala la lugha ya tendo la ndoa katika mchakato wa mafunzo ya tendo la ndoa katika muktadha wa jandoni halijafanyiwa utafiti wa kina. Utafiti huu uliazimia kuchanganua diskosi hizo ili kuweka wazi mada za tendo la ndoa zinazodhihirisha ubabedume katika mafunzo ya jandoni miongoni mwa Wakipsigis.

## **1.2 Suala la Utafiti**

Ingawa kuna tafiti nyingi ambazo zimefanywa kuhusu diskosi za mafunzo ya tohora nchini Kenya, bado kuna masuala mengi yanayoendelea kuibuka katika mafunzo ya jandoni. Tafiti nyingi zimejikita katika masuala ya lugha na jinsia, zimeegemea sana upande wa ufeministi. Hata hivyo, suala la lugha ya tendo la ndoa ni la karibuni kutokana na unyeti unaohusiana na suala hili. Mijadala kuhusu tendo la ndoa huwa nyeti na wengi huchelea kuizungumzia kwa uwazi na aghalabu huchukuliwa kuwa ni miiko katika jamii. Hili limechangia katika uhaba wa tafiti kuhusu masuala haya ya lugha ya tendo la ndoa. Tafiti zilizofanywa zabainisha kwamba mafunzo ya tendo la ndoa katika muktadha wa jandoni hayajafanyiwa utafiti wa kina. Mpaka sasa, kwa uelewa wa mtafiti, utafiti kuhusu diskosi zinazofunzwa jandoni katika jamii ya Wakipsigis haujashughulikiwa. Kwa hivyo, utafiti huu una azma ya kuziba pengo hili la kiusomi.

## **1.3 Madhumuni ya Utafiti**

1. Kuchanganua mada za diskosi ya tendo la ndoa zinazofunzwa jandoni.
2. Kutathmini mikakati inayotumiwa katika mafunzo ya diskosi za tendo la ndoa.

## **1.4 Maswali ya Utafiti**

1. Je, ni mada zipi za diskosi ya tendo la ndoa zinazodhihirika katika mafunzo ya jandoni katika jamii ya Wakipsigis?
2. Je, ni mikakati ipi inayotumiwa katika mafunzo ya diskosi za tendo la ndoa zinazofunzwa jandoni katika jamii ya Wakipsigis?

## **1.5 Umuhimu wa Utafiti**

Utafiti huu ulinuia kufafanua mikakati inayotumiwa kufunzia diskosi za tendo la ndoa jandoni. Utawafumbua macho wanajamii na kutarajiwa kupendekeza mbinu zinazoweza kutumiwa kuimarisha mafunzo haya. Fauka ya hayo, wasomi, wahakiki na watafiti wa masuala ya tendo la ndoa watakuwa na msingi bora ya kurejelea wanapofanya kazi zao.

Utafiti huu ulitokana na msukumo kwamba suala la kuchunguza diskosi za tendo la ndoa katika jamii ya Wakipsigis halijashughulikiwa kwa mapana. Hivyo basi, utafiti huu ni mchango mwafaka kwa tahakiki zilizoko kuhusu diskosi ya tendo la ndoa katika muktadha wa jandoni. Matokeo ya utafiti huu yatachochea kuibuka kwa mada nyingi za utafiti, kuhusu jando na tendo la ndoa katika jamii mbalimbali. Uelewa wa diskosi za tendo la ndoa zilizotumiwa kwenye shughuli za jandoni katika mawasiliano utachangia katika kuhamasisha wasomi kuhusu masuala yanayosheni usiri na unyeti.

Aidha, utachochea mbinu ya kusafidi lugha katika matumizi ya diskosi hizo. Matokeo ya utafiti huu yatawafaa wasomi wa diskosi kwa kuwaongezea maarifa kuhusu jinsi ya kuchanganua diskosi zinazohusu tendo la ndoa hasa katika miktadha ya jando na unyago. Vilevile washauri wa ndoa watanufaika kutokana na utafiti huu, kwa sababu watapata maarifa zaidi na kuelewa kwa kina kuhusu masuala ya tendo la ndoa. Kutokana na utafiti huu, wataibuka na mbinu mpya ya kuwashauri wanandoa na kuwaelekeza kwa msingi ya kitamaduni. Pia, watapata maarifa na tajriba ya kuwashauri wanandoa ambao walitahiriwa. Vilevile, watafahamu zaidi kuhusu umuhimu wa mafunzo ya jandoni.

Fauka ya hayo, utafiti huu unatoa mchango katika kuhifadhi tanzu za fasihi simulizi hasa utanzu wa maigizo kiperi cha miviga cha jamii ya Wakipsigis katika kiwango cha othografia au kimaandishi. Aidha, utafiti huu utawauni washikadau wote wanaohusika kubuni sera zinazohusu masuala ya jinsia.

## **1.6 Upeo na Mipaka**

Utafiti huu ulihusu masuala ya jandoni kwa kuangazia diskosi za tendo la ndoa ukiwa na dhamira ya kubainisha, kufafanua, kuchanganua na kueleza jinsi diskosi za tendo la ndoa zinavyosawiriwa katika muktadha wa jandoni. Utafiti huu ulihusu mafunzo ya jandoni katika jamii ya Wakipsigis katika jimbo la Bomet hasa kwa kurejelea kipengele

kimoja pekee cha mafunzo hayo ambacho ni diskosi za suala la tendo la ndoa. Uchanganuzi ulijikita katika masimulizi na utendaji wa ngariba katika miviga ya tohara za wavulana jandoni.

## SURA YA PILI

### MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA

#### 2.1 Utangulizi

Kwenye sura hii mtafiti alishughulikia tahakiki za maandishi yaliyohusiana na mada inayotafitiwa pamwe na kueleza jinsi nadharia teule katika utafiti huu ilivyotumiwa katika uchanganuzi wa data. Sehemu hii mapitio ya maandishi ilianguzia diskosi ya mafunzo ya jandoni na uchanganuzi wa diskosi za tendo la ndoa. Maoni ya watafiti wa awali kuhusu diskosi yalizingatiwa ili kuonyesha jinsi yalisaidia katika utafiti huu pamoja na kuonyesha pengo lilopo ili kujaribu kuliziba pengo hilo kupitia utafiti huu. Zaidi, misingi ya kinadharia ilishughulikiwa kwa kujikita katika historia, waasisi na namna mihimili ya nadharia ilivyotumika katika utafiti huu. mwisho historia ya Wakipsigis ilishughulikiwa.

#### 2.2 Yaliyoandikiwa kuhusu Diskosi za Mafunzo ya Jandoni

Kieti (1999) alitafiti kuhusu sherehe na mafunzo ya tohara katika jamii ya Wakamba. Matokeo ya utafiti wake yalibaini kwamba watahiriwa hufunzwa ulengaji wa shabaha msituni wakitumia mti kama zana ya kuwinda. Sherehe hii ilifanywa kwa lengo la kuwafunza jinsi ya kuikinga jamii. Tohara hii inaitwa *kuatha mbusya* yenye maana ya kuwinda kifaru. Kifaru alikuwa wa kidhahania kwa muktadha wa sherehe hii. Ni mti ambao ulitengenezwa ili utumike, ndani yake kukiwa na shimo ambapo ngariba huiga sauti ya kifaru akiwa ndani. Matarajio ya watahiriwa ni kumwinda na kumuua kifaru huyo. Mchakato huu uliashiria kwamba walikuwa tayari kutetea na kuulinda jamii yao dhidi ya uvamizi wowote ule. Vilevile, ulionyesha kuwa katika jamii hii, kulikuwa na tishio la kuvamiwa na vifaru. Ili kuelewa mambo kama haya, muktadha wa kihistoria kwa tohara ni lazima ufahamike. Kazi ya Kieti iliufaa utafiti huu kwa sababu lengo letu ni kutathmini mikakati inayotumiwa katika mafunzo ya jandoni. Tofauti na utafiti wa Kieti ambao ulichunguza sherehe na mafunzo ya tohara katika jamii ya Wakamba utafiti huu ulichunguza diskosi za lugha inayotumika katika kuwosia vijana kuhusu tendo la ndoa katika jamii ya Wakipsigis. Nandwa (1976) alieleza kwamba tohara ilikuwa shughuli muhimu sana kwa mtu binafsi na jamii kwa jumla; kwa sababu waliotahiriwa walipata mafunzo ya: maadili, siri, utu uzima, utamaduni na historia ya jamii yao. Wasomi wengine kama vile Nyaga (1970) na Kanake (2001) wanaunga mkono kauli hii. Kwa hivyo, mawazo haya yalikuwa muhimu sana katika utafiti huu

kwa sababu tulidhamiria kuonyesha jinsi mafunzo ya tendo la ndoa yanavyopitishwa kwa wavulana kupitia sherehe za jando katika jamii ya Kipsigis.

Akichangia kuhusu suala la mafunzo kuhusu tendo la ndoa Wathome (2009) anasema, tohara si tendo la kutahiri pekee bali lina umuhimu mkubwa katika jamii husika kama; kuwaandaa vijana kwa majukumu ya utu uzima katika jamii zao na kuwapa mafunzo maalum kwa ajili ya kufanikisha majukumu hayo. Katika jamii ya Wakamba, vijana hupashwa tohara baada ya kubaleghe. Kipindi hicho kilikuwa muhimu na ulikuwa wakati mwafaka wa kutayarisha vijana kwa masuala ya utu uzima. Kwa hivyo kipindi hicho kiliwaunganisha watahiriwa na tamaduni za jamii zao. Walipata mafunzo kuhusu tabia njema na tamaduni zinazokubalika na wanajamii. Aidha, sherehe hizo zilikuwa mojawapo ya njia za kuwakusanya pamoja wanajamii wa Wakamba. Utafiti huu, ulikaribiana na wa Wathome kwa kiasi japo, tulijikita katika mafunzo ya tendo la ndoa katika miviga ya sherehe za tohara.

Kazi ya Kakai (1992) inahusu mfumo wa marika ya tohara ambao hupatikana katika jamii nyingi hapa nchini Kenya na hata Uganda. Majina kama vile Sawe, Maina na Chuma yanapatikana katika jamii kama Agikuyu, Abakuria, Kalenjin, Aembu, Akamba, Bukusu na Ameru. Hata hivyo, majina haya yanatofautiana kimatamshi katika jamii tofauti kwa mfano katika jamii ya Abugusii na Kipsigis: Bamaina-Maina, Banyange-Nyongi, Bakolongolo-Korongoro, Basawa-Sawe, Bakikwameti-Kipkoimet, Bakananachi-Kiplelach, Bakinyikewi-Kimnyikei, Bachuma-Chumo. Mfumo wa marika ni mojawapo wa mada kuu inayofunzwa jandoni. Kazi ya Kakai ilitufaa katika utafiti wetu kwa sababu tunarejelea mfumo wa marika katika uteuzi wa sampuli. Hata hivyo, yeye alitumia nadharia tofauti na yetu alitumia Ethnografia ya mawasiliano katika utafiti huu tilitumia nadharia ya uchanganuzi matini mkabala wa historia.

Greer (2000) anaegemeza uchunguzi wake kuhusu jinsia na kudai kuwa suala la uume limenawiri sana katika utamaduni na kuliondoa ni vigumu. Greer anaeleza kwamba kwa kuegemea kuumeni katika jamii mbalimbali, katika umri wa miaka kumi na mitano mwanamume amepata uhuru wa kushiriki tendo la ndoa akilinganishwa na mwanamke ambaye hajaruhusiwa. Utafiti wake ulibaini kuwa jamii huamini kwamba ni jukumu la mwanamke kumtoshela mwanamume katika tendo la ndoa, lakini suala la mwanamke kutoshelezwa limepuuzwa. Anaendelea kudokeza kuwa mwanamke anatarajiwa kuutunza mwili wake na jinsi anavyoonekana anadhibitiwa hata katika

upande wa mavazi. Suala la mwanamume kusawiriwa kama mwenye uwezo linazingatiwa na kutiliwa mkazo sana ilhali wanawake wanafunzwa waweze kuwaogopa wanaume ambao wamedhaniwa kuwa visirani na wabakaji. Msomi Greer aligundua kuwa wanawake wanapata mafundisho ya sheria za jinsi ya kuwa mwanamke wakiwa na umri mdogo hii ndio sababu wanaona soni ya uchi wao hivyo basi kupoteza dhana ya ukombozi na utawala wao. Hali hii ndio huwafanya wajidunishe, wajione dhaifu, wajitenge na wanakosa furaha. Greer anaeleza wanawake wanapaswa kuijua na kuikubali miili yao. Kazi ya Greer ilifaa sana utafiti huu, kwa sababu mafunzo ya jando katika jamii ya Wakipsigis yanahimiza mada ya tendo la ndoa na yalichangia kufanikisha kuibuka na mada zinazofunzwa wakati wa tohara kuhusu tendo la ndoa.

Mafunzo ya jando yanasababisha kudorora kwa maadili. Said (2009) anaeleza kuwa, mporomoko huo wa maadili ya vijana unatokana na mabadiliko ya mwenendo na tabia ya vijana kila uchao. Zamani baada ya vijana kufuzu jandoni, walikuwa na mazao makubwa katika jamii. Vijana walikuwa na uwezo wa kusaidia kazi ndogo ndogo za jamii kama kukata kuni, kulea watoto wadogo, kilimo, kuteka maji mtoni na kuvuna. Lakini hali hiyo imebadilika kwa sasa. Kwa mujibu wa Said umri wa vijana wanaofuzu jandoni ni mdogo kiasi kwamba hawawezi kufanya kazi hizo. Kushindwa kwa vijana hawa kunawafanya kufasiri kuwa huo ndio mtindo wa maisha ya kawaida. Kazi ya Said inakaribiana na yetu kwa kiasi kwa kuwa tunaangazia mafunzo ya jandoni, lakini kwa upande mwingine unatofautiana kwa sababu tulilenga diskosi za lugha ya tendo la ndoa.

Kwa mujibu wa Matei (2011) anaeleza kwamba, miviga huadhimishwa na jamii mbalimbali kila mwaka. Miviga za jandoni hutekelezwa wakati jamii imevuna mazao tele. Kiviga cha maziko hutekelezwa muda mahususi kwa mujibu wa kaida na desturi za jamii inayohusika. Nayo sherehe ya kuwapa majina watoto hufanyika baada ya kipindi maalum mtoto anapozaliwa. Mawazo haya yalitusadia kubaini namna miviga hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Mawazo yake yalitufaa katika utafiti huu kwani miviga ya jando ya jamii ya Wakipsigis ni tofauti sana na miviga za jamii zingine.

Akichangia kuhusu suala la mafunzo kupitia miviga M'Ngaruthi (2008) alieleza kwamba, miviga huwa ni sherehe maalum ambazo hufanywa na jamii katika kipindi na majira mahususi ya mwakani. Miviga hii huandamana pamoja na vitanzi vingine vya usimulizi kwa mfano ngoma, nyimbo, ukariri na kughani mashairi, utegaji wa

vitendawili, mafumbo, semi, maigizo na matambiko. Anasema kwamba, mara nyingi miviga hufanywa na watu waliokomaa kutoka kundi moja hadi nyingine. Miviga pia hufanywa wakati jamii inapitia misukosuko ya kimazingira na kibinadamu. Mambo ya sanaa huandamana na shughuli ya miviga pamoja na maombi kwa mwenyezi Mungu au miungu. Mawazo muhimu kuhusu msomi huyu ni kwamba miviga hufanyika wakati wa kipindi maalum mwakani na inahusisha imani za wanajamii husika na pia kutoa mafunzo fulani kwa wanajamii wengine. Jambo ambalo ni la muhimu katika utafiti huu kwa sababu tulichunguza jinsi miviga ya tohara ya wavulana hutumika kutoa mafunzo kuhusu tendo la ndoa katika jamii ya Wakipsigis.

Naye Mulokozi (1989) anaeleza kwamba, miviga ilitokana na michezo ya kuigiza na hadithi simulizi za kale na vitendo vya kiimani vya uko bara la Uropa. Wayunani pamoja na Wagiriki wa kale walihusisha miviga ya kiimani katika tamthilia. Miviga hiyo ilihusu tambiko la kuzaliwa, kuolewa, kifo na kupata maumbile mapya ya ubinadamu katika dunia nyingine. Nchini India inaaminika kwamba asili ya miviga ni mchezo wa kuigiza ambao ulitokana na utenzi ulioitwa Mahabharatana katika mahekalu. Barani Afrika miviga huhusishwa na michezo ya kitamthilia ambayo ilipatikana kule Misiri. Michezo hii ilihusu kifo na kufufuka kwa mungu wa Wamisiri anayejulikana kama Oasisi. Mintarafu ya haya utanzu wa usimulizi una uhusiano wa kidini, dhana ya miviga haiwezi kupuuzwa. Hatuwezi kutenganisha miviga ya jamii na dini kwani kuna mafundisho yanayotokana na miviga hiyo. Mawazo haya yalikuwa muhimu katika utafiti huu kwani tunaona kwamba kuna mafundisho yanayotokana na miviga. Kwa hivyo, tulichunguza jinsi mafundisho ya tendo la ndoa yanavyoendelezwa kupitia miviga ya jando katika jamii ya Wakipsigis.

Akichangia jinsi miviga hutumiwa kutoa mafunzo Wanjala (2010) alichunguza miviga ya Embali katika jamii ya Babukusu anaeleza kwamba, sherehe za tohara katika jamii hii huwa zimepangwa na hufuata utaratibu maalum. Sherehe hizi huandamana na matambiko ambayo hutokea kama drama huku yakitoa funzo fulani kwa wanajamii. Sherehe hizi huzingatia muundo na arudhi za tamthilia kama vile mwanzo ambao ni msingi wa mgogoro, mgogoro kukuzwa na kuendelezwa hadi kileleni. Alitoa mfano wa miviga pale ambapo ng'ombe alichinjwa ili kuwazawidi watahiriwa na luliki iliwekwa shingoni mwao wanapowasili katika boma la mjomba wao kwani wanaamini kwamba hiyo ni nyama ya kuwasetiri wakiwa tumboni. Aidha, msomi huyu alitafiti sherehe za

*Mwaka-Kogwa.* Anaeleza kwamba hafla hii ilifanyika kisiwani cha Pemba na Unguja katika eneo la Makunduchi ili kuukaribisha mwaka mpya. Sherehe hizi huchukua muda wa siku nne ambapo ndugu wawili wawili kutoka Mashariki na Kaskazini hupigana kwa kutumia migomba. Mashabiki nao hujiunga na wapiganaji kisha kuchangia katika kuharibu ndizi. Hii ilikuwa funzo ya kuleta utakaso katika jamii pamoja na kusherehekea mwisho wa mwaka na kukaribisha mwingine katika jamii hii. Mawazo haya ndiyo nguzo ya utafiti huu, kuchunguza mafunzo ya tendo la ndoa kupitia miviga ya jando. Miviga ilikuwa ya manufaa kwenye tasnifu hii kwa sababu, katika jamii ya Wakipsigis, kuna utendaji unaoendelezwa na ngariba huku akiwapa mafunzo wavulana. Utendaji huu usawiri ubabedume kupitia lugha, historia na itikadi hasa kupitia kwa masimulizi na matendo ya ngariba katika kutoa mafunzo yanayohusu tendo la ndoa.

Naye Alembe (2012) akichangia suala la mafunzo kupitia miviga anaeleza kwamba, miviga ya Shilemba katika jamii ya Wanyore inahusu kuangamiza mimea hasa migomba ya ndizi. Hili hutokea wakati wa maziko ya mtu ambaye ni mashuhuri hasa mwanamume katika jamii hii. Anafafanua kwamba wahusika hujipanga na fahali kwenye kiingilio kuu na kuandamana moja kwa moja hadi sehemu iliyo na migomba ya ndizi nyuma ya nyumba. Wao husababisha uharibifu wa migomba na mimea mingine kwa kuikata na kukanyagia chini. Fahali na watu uhusika katika uharibifu huo. Uharibifu huo huwa ni ishara ya kupotea kwa mtu mashuhuri katika jamii hiyo. Baada ya tukio hili wahusika huandamana hadi kwenye kaburi la mwendazake ambaye alikuwa shujaa na kulitandaza vilivyo. Umuhimu wa kulitandaza kaburi na kutawanya mchanga huwa ni ishara ya kumpa shujaa fursa ya kuomba msamaha kwa watu aliowaua na pia inaaminika ni ishara ya kuandaa njia atakayotumia kwenda ulimwengu mwingine. Maelezo yalitufaa katika tasnifu hii kwa sababu yanatoa nafasi ya kutafitia mambo yanayohusu viviga na kaida na desturi za wanajamii wa Kipsigis. Ingawa kuna tofauti na utafiti wake kwani Alembe alitafiti miviga ya mazishi ya mtu shujaa utafiti huu ulitafiti miviga ya jandoni kwa kuzingatia mafunzo ya tendo la ndoa katika jando yanayotolewa kwa njia ya miviga.

Khaemba (2013) amejitosa katika utafiti wa miviga alijikita katika ubabedume na jinsi unavyojengwa katika miviga ya Wabukusu. Alichunguza mambo matatu ambayo ni tohara, mafundisho kwa vijana waliopashwa tohara jandoni na sherehe ambayo

hufanywa siku tatu baada ya mzee mkongwe kuzikwa. Aligundua kwamba dhana ya ubabedume huendelezwa na kutiliwa mkazo na itikadi zinazokuza jinsia ya kiume na kudhalilisha jinsia ya kike. Msomi huyu alionyesha pia jinsi wanaume wanatumia mbinu ainati za uzungumzaji kujichipua, kujikuza na kuendeleza satua yao katika jamii hii kupitia mafunzo ya jandoni. Utafiti wa Khaemba ulikuwa nguzo kuu katika utafiti huu. Licha ya kwamba alishughulikia suala la ubabedume katika miviga ya tohara katika jamii ya Wabukusu jamii ambayo ni tofauti na ile inatafitiwa katika utafiti huu. Mawazo yake kuhusu jinsi ubabedume hujengwa na kuendelezwa miongoni jinsia ya kiume yalikuwa muhimu kwani tulichunguza jinsi ubabedume unaendelezwa kupitia mafundisho ya jandoni njia ya miviga kuhusu mada za diskosi za tendo la ndoa.

Kwa mujibu wa Manguliechi (2007), tohara katika jamii ya Wabukusu, ni miongoni mwa sherehe muhimu sana katika jamii hii. Kwa jumla, lengo kuu la sherehe hii ni kuwatoa vijana utotoni hadi utu uzima. Sherehe hii ya tohara katika jamii ya Wabukusu pia hutumiwa kupitisha mila, itikadi, imani, falsafa, hisia, maadili na mihemko ya Wabukusu. Majukumu haya yote hupitishwa kupitia kwa nyimbo, mawaidha, maigizo na kucheza. Utafiti wetu ulilenga nyimbo kama mojawapo ya mbinu zinazotumiwa kuwasilisha dhamira mbalimbali za sherehe za tohara katika jamii ya Wakipsigis. Wakati wa sherehe hii ya tohara. Nyimbo zilitungwa na bado hutungwa kutegemea muktadha, kipindi kwa mujibu wa wakati na madhumuni. Utafiti wa Manguliechi umesaidia utafiti huu kwani tulichunguza nyimbo zinazoandamana na miviga ya tohara. Tofauti ni kwamba yeye alitafiti nyimbo tu lakini utafiti huu ulitafiti nyimbo na miviga.

Katika utafiti wa Hanke (1998) alidhihirisha jinsi ambavyo vyombo vya habari hasa runinga huendeleza suala la ubabedume kupitia kwa picha na unenaji. Matinde (2015) alishadidia mawazo haya ya Hanke alipofanya utafiti kuhusu ubabedume katika majigambo ya Abakuria. Aligundua kwamba Abakuria hudhihirisha na kuendeleza ubabedume kupitia majigambo. Mawazo ya wasomi hawa yalikuwa ya manufaa katika utafiti huu kwani tuliweza kuweka msingi wa ubabedume katika jamii. Watafiti hawa wamedhihirisha jinsi utamaduni na mazingira husaidia katika kuendeleza uwezokiume ambao unajengeka katika ufahamu wa wanajamii. Kwa hivyo, hali hii huathiri uhusiano kati wa kijinsia kwa wanajamii. Katika muktadha huu, tamaduni za Wakipsigis, kupitia lugha, utendaji wa ngariba na sherehe na miviga ya tohara ya wavulana zilitusaidia

katika kutambua mchango na umuhimu wa mazingira na utamaduni katika kukuza mada za diskosi za tendo la ndoa katika jando.

### **2.3 Mikakati ya Diskosi ya Tendo la Ndoa**

Katika sehemu hii tulijikata katika mitindo mbalimbali iliyotumika katika tafiti za awali. Fasihi hupimwa uzuri wake kwa kuzingatia mikakati ya usemi inayotumika kupitisha ujumbe kwa wasikilizaji. Mikakati ya usemi katika miviga hudhihirisha nyenzo ambazo mwasilishaji ametumia kufanikisha maudhui yake. Tafiti mbalimbali zimedhibitisha kuwa lugha inayotumika katika nyiso huonyesha taswira halisi ya maisha katika jamii. Picha halisi ya jamii hushamirishwa na fani mbalimbali za lugha. Kwa misingi hii mikakati ya usemi hudhihirisha masuala yanayofunzwa jandoni wakati fulani. Mikakati iliyobainika ni kama vile istiari, tasfida, jazanda, misemo kinaya na kadhalika.

Kwa mujibu wa Matinde (2015) anaeleza kwamba, uchanganuzi wa masuala ya miviga lazima yazingatie utaratibu wa kufasiri pamoja na kuchanganua miviga jinsi ilivyofafanuliwa na Beaugrade na Dressler (1991). Wasomi hawa wameeleza matini kama mawasiliano ambayo lazima yazingatie vigezo saba, wanadai kuwa, ni sharti matini ilandane na sheria za utunzi mahususi ama aina maalum ya kiperu. Vipera vya fasihi vina sifa maalum za kiisimu nauamilifuwake hujikita katika mipaka maalum ya kuzalisha na kupokelewa na wanajamii (Swales, 1991). Kuna maana ya juu na maana ya ndani ya matini inayochunguzwa. Maoni ya wataalam hawa yalifaa utafiti huu kwani tulijikita katika kuchanganua lugha iliyotumika katika miviga ya tohara kwa kuzingatia maana ya ndani inayowasilishwa. Vigezo saba ambavyo viliorodheshwa na De Beaugrade na Dressler (1981) ni kama vile; mshikamano unaohusisha umbo la nje la matini kwa mfano sintaksia. Mshikamano unafaa kuhusisha uradidi, udondoshaji na muungano wa vitenzi vya matini husika, kwa upande wa mchukuano maana ya matini huzingatia. Urejelezi wa matini ambazo hazihitaji utambuzi na maarifa ya kiisimu. Huzingatia maarifa ambayo hayajitokezi wazikatika matini ila huwa ni vidokezo vya lengo la msanii ambavyo kwa kiasi huweza kuleta athari katika upokeaji kwa hadhira (Grice, 1975, Wodak, 1987, Kintsch na Van Dijk, 1983).

De Beaugrade na Dressler (1981) wanasema kuna maana ambazo zimesimbwa na uhusisha utambuzi wa umbo la nje na ndani la matini. Dhamira nayo uhusisha kile ambacho mtunzi alikusudia kuwasilisha kwa hadhira. Katika miviga, watendaji

hupitisha masuala kama vile mitazamo, mielekeo itikadi na imani za jamii ambazo hujenga na kudumisha ubabedume. Watendaji hutumia weledi wao na ubunifu kusetiri hali mbalimbali za kijamii ambazo kwa namna ya kipekee hudhihirisha mitazamo, mielekeo, imani, desturi na historia ya jamii. Dhana ya ukubalifu hutumika kama dira ya dhamira ya mtendaji. Kwa hivyo, matini lazima ikubalike na itambuliwe na wanajamii husika ndani na nje ya eneo mahususi. Uarifishaji nao huzingatia thamana mpya za habari zinazotarajiwa. Ni uzuri wa habari iliyowasilishwa, utamkaji na dhana ainati za unenaji ambazo ni za manufaa kwa kuzalisha matini (Wodak na wenzake, 1989). Kunazo aina za kipekee za matini, mitindo ya kunena na mafumbo ambayo hutokea katika miktadha halisi ya kitamaduni na itikadi za kijamii pamoja na mwingiliano wa tanzu. Vigezo hivi vilikuwa muhimu katika utafiti huu hasa katika kuchanganua lugha inayotumiwa na ngariba ili kupata maana yake kisemantiki.

Cain na wenzake (2011) walitafiti kuhusu diskosi ya tendo la ndoa katika jamii ya Abagusii kwa kuangazia mafumbo ya tendo la ndoa. Matokeo ya utafiti wao yalibaini kuwa wanawake wanapoolewa katika jamii ya Abagusii hupewa hadhi tofauti ikilinganishwa na wale hawajaolewa. Kitendo cha tendo la ndoa huruhusiwa kuzungumzwa na kutendwa na wanawake walioolewa. Matumizi ya mafumbo kuhusu sehemu nyeti za wanawake yanaonyesha majukumu mbalimbali ambayo sehemu hizo hutekeleza. Miongoni mwa majukumu haya yanayodokezwa ni kukata kiu (*ensooko* na *egesima*), kuzaa (*enyebirero*) na kulimwa (*egeticha* na *omogondo*). Matini hii iliufaa utafiti huu katika kufanikisha malengo kwa kuwa suala walilochunguza linakaribiana na hili tunaloshughulikia katika utafiti huu kuhusu diskosi ya tendo la ndoa katika mafunzo ya jandoni.

Moto (2004) alitoa mifano ya tasfida na mafumbo kutoka lugha ya Chichewa inayozungumzwa nchini Malawi. Alidokeza kuwa tendo la ndoa hutajwa kwa mafumbo kama vile (*chikole*) kushika na (*chibwenzi*) kufanya urafiki. Ogechi (2006) alitafiti kuhusiana na mafumbo ya tendo la ndoa katika lugha ya sheng' na kung'amua kuwa kupeana, kusugwana, kutibiana, kuonwa na kadhalika ni msamiati unaorejelea tendo la ndoa. Ellis (1999) anasema matumizi ya mafumbo katika kueleza magonjwa yanayohusiana na tendo la ndoa katika lugha za Kiafrika yanaweza kusababisha kutoeleweka kwa ujumbe unaopitishwa. Kwa mfano, fumbo *ebuti* lilitumika kurejelea kondomu ya wanawake. Kwa hivyo, linaweza kueleweka vibaya hasa na wanawake,

kwa vile walifasiri kuwa wao ndio hatari zaidi na wanaume wanapaswa kujikinga dhidi yao. Matini hii iliufaa utafiti wetu katika kufanikisha malengo japo kwa upande mwingine utatofautiana kwa sababu tutajikita kwa masuala ya jandoni katika jamii ya Wakipsigis.

Kwa mujibu wa Magato (2010) anaeleza kwamba, utambulisho wa mahusiano ya jamii hujengwa na usemi. Tafiti mbalimbali zimedhibitisha kuwa lugha inayotumika katika nyimbo huonyesha taswira halisi ya maisha katika jamii. Utafiti wa Magato ulichanganua semi katika nyimbo za ukeketaji kwenye jamii ya Abagusii. Mtafiti alipambanua sifa za lugha inayotumiwa katika usemi wa ukeketaji na akabaini kwamba semi hujengwa na utambulisho wa mahusiano. Utafiti wetu unatofautiana na wa Magato kwa sababu katika utafiti wetu tunachanganua diskosi za tendo la ndoa ya mafunzo ya tohara kwa jumla. Aidha, utafiti wao ulijikita katika jinsia ya kike nasi utafiti wetu tulishughulikia vijana wa kiume. Isitoshe, utafiti wake uliifaa kazi yetu katika uchanganuzi wa semi za wahusika maalum kama vile ngariba na watahiriwa ambao walijenga msingi wa utafiti huu. Nyandiwa (2015) aliangazia vipengele mbalimbali vya kimtindo vinavyoendeleza maudhui. Alichanganua baadhi ya mitindo ya lugha kwa mfano tashhisi, chuku, sitiari na kejeli katika tamthilia. Utafiti wake ulionyesha jinsi vipengele hivi vinavyoendeleza maudhui. Japo utafiti wake ulishughulikia vipengele vya kimtindo katika tamthilia na jinsi vinavyoendeleza maudhui, utafiti wake iliufaa sana utafiti huu katika kuonyesha jinsi mikakati ya diskosi iliyotumika katika sherehe za jando inavyodhihirisha mafunzo ya tendo la ndoa. Chepkorir (2016) alichanganua mikakati ya diskosi kwenye tahariri ya Gazeti la Taifa leo. Katika utafiti wake aligundua kwamba tamathali za usemi na mitindo mingine ilitumiwa na mwandishi wa tahariri ya Taifa leo. Alichunguza sitiari, misemo na tashbihi. Alipata kuwa sababu kuu ya kutumia tamathali hizi za usemi ni kujenga picha halisi ya hali ya mambo katika jamii kwa vile tahariri huzungumzia masuala yanayoathiri mwananchi wa kawaida. Uchunguzi wake ulionyesha kuwa mbinu hizi zimetumika kufanikisha kueleweka kwa ujumbe. Fauka ya kuwa uchunguzi wa Chepkorir ulitofautiana na wetu, ulikuwa tunu kwetu katika kuhakiki mikakati ya diskosi iliyotumika katika sherehe za jando inavyodhihirisha mafunzo ya tendo la ndoa.

Safinia (2017) alichunguza matumizi ya lugha katika tamthilia pamwe na dhamira zilizojitokeza ndani ya matumizi hayo ya lugha. Alipata kuwa mwandishi ametumia

vipengele tofauti vya lugha katika kuwasilisha maudhui kwa mfano matumizi ya tamathali za usemi, lugha ishara, lugha ya taswira, uradidi, mdokezo tanakali za sauti na nyinginezo. Aidha, aligundua kuwa mitindo hiyo ya lugha iliibua maudhui tofauti kama vile kujishajiisha, kujikomboa, kukuza umoja, kusuta usaliti, matabaka, umaskini, uongozi mbaya na mengine mengi. Japo alijikita tu katika tamthilia, utafiti wake ulielekeza utafiti wetu katika kuhakiki jinsi mikakati ya diskosi iliyotumika katika sherehe za jando inavyodhihirisha mafunzo ya tendo la ndoa. Wekesa (2008) alitafiti kuhusu jinsi taswira inavyotumiwa kuwasilisha ujumbe wa mwimbaji. Alionyesha kuwa nyimbo hutumia taswira kutoka mazingira zilimoundiwa. Alibaini kuwa majina yanayotumiwa katika nyimbo huwa na maana fiche. Utafiti wa Wekesa umekuwa muhimu katika utafiti huu hasa katika kuchanganua maana fiche ya maneno ambayo yametumika katika mafunzo ya tendo la ndoa jandoni. Kwa upande mwingine, usomi ulikuwa tofauti na wetu kwa sababu alijikita katika kipengele kimoja tu cha taswira lakini utafiti huu ulishughulikia vipengele vingi vya mikakati ya diskosi iliyotumika katika sherehe za jando inavyodhihirisha mafunzo ya tendo la ndoa.

Jumbe (2015) alifanya utafiti kuhusu mikakati ya usemi katika muziki wa kisasa. Katika matokeo ya utafiti huu yalionyesha namna mikakati ya usemi inavyojitokeza kwenye muziki wa kisasa. Aliangalia mafunzo yanayotolewa na athari ya mikakati hii kichanya na uhasi. Utafiti wake ulidhihirisha kuwa mafunzo ya athari hasi kama vile wavulana kwa wasichana kuingilia shughuli za kimapenzi wakiwa wa miaka michache na hivyo kuchangia maovu ya kueneza magonjwa ya zinaa. Zaidi, aligundua mafunzo ya athari nyingine ya upotovu wa maadili miongoni mwa vijana kwa kuwa vijana ndio wanapenda kuiga mambo ambayo yanawasilishwa katika muziki na jinsi wasanii wanatenda katika tungo zao. Pamwe mafunzo hayo ya athari uhasi, mtafiti huyu alibainisha mafunzo ya athari chanya kama vile kutoa burudani, kuendeleza uhusiano mwema, na kuwazindua wanajamii. Ingawa utafiti wake ulitofautiana na utafiti wetu, ulitufaa sana katika kuhakiki jinsi mikakati ya diskosi iliyotumika katika sherehe za jando inavyodhihirisha mafunzo ya tendo la ndoa.

Utafiti wa Ndemo (2014) ulihusu uchanganuzi wa mitindo ya lugha ya kuleta amani na mahusiano mema katika muziki nchini Kenya. Alikusudia kuonyesha jinsi kuna upekee wa matumizi ya lugha ili kuwasilisha mafunzo ya maridhiano na namna ya kuishi kwa amani kupitia muziki. Mtafiti huyu alichanganua matumizi ya kipekee ya

maneno ya sintaksia, alishughulikia mahusiano ya kimtindo wa wima na isio wima. Matokeo yalidhihirisha kuna upekee wa matumizi ya lugha katika kuwasilisha mafunzo ya amani na maridhiano. Zaidi, katika utafiti huu alibainisha kwamba matumizi ya lugha hutekeleza dhima ainati katika jamii. Dhima hizi ni kutoa mafundisho ya amani na mahusiano mema, kuonya jamii dhidi ya tabia hasi ambayo inaweza kusambaratisha usalama wa nchi na kutoa mawaidha ya jinsi ya kuwezesha jamii kupata amani ya kutosha. Utafiti huu ulikuwa nguzo muhimu katika utafiti huu katika kubainisha majukumu ya diskosi za tendo la ndoa katika miviga ya sherehe ya tohara ya wavulana katika jamii ya Wakipsigis. Fauka ya hayo, utafiti huu ni tofauti na wetu kwani Ndemo alizingatia mitindo ya lugha, ilhali utafiti wetu umejikita katika miviga ya sherehe za jando kwa kujikita katika mikakati ya diskosi za tendo la ndoa.

Pichler (2001) alitafiti kuhusu mazungumzo ya tendo la ndoa miongoni mwa wasichana wa kitovu cha Ulaya. Matokeo ya utafiti huo yalibaini kwamba kuna aina za dayolojia katika mazungumzo haya. Mazungumzo ya moja kwa moja na mazungumzo yasio ya moja kwa moja kuhusu tendo la ndoa. Aidha, Pichler akimnukuu Sprecher na Hatfield (1994), anadai kuwa mojawapo wa mienendo kuhusu tendo la ndoa kwa baadhi ya wanawake huonekana kuwa mienendo mizuri. Jambo lililo bora kuhusu ung'amuzi huu ni kwamba baadhi ya tabia hukubaliwa na nyingine hazikubaliwi katika jamii. Uwepo wa migao ya upeo ulifaa utafiti huu katika kufanikisha malengo ya utafiti huu.

Diskosi ya wavulana kuhusu kuvunja ubikira hutumia lugha ya jazanda wao huonyesha hali kuwa 'mwanamume' kwa namna ambayo ni kinyume kwa tajriba ya wasichana, kama walivyodokeza Holland na wenzake (1991). Wavulana huwa na msukumo wa kudhihirisha uwezo wa kiume kwa kuwatafuta mabinti ambao watashiriki nao ngono nao mabinti hujikaza kuhifadhi hali yao ya kuwa bikira. Fauka ya uwepo wa masuala haya, ni dhahiri kwamba saula la kutunza ubikira miongoni mwa mabinti limedorara kwa sababu ya masuala mtambuko tofauti na hapo zamani. Utafiti wa Holland na wenzake uliufaa sana utafiti huu na utaongoza katika kuchanganua diskosi ya mafunzo ya jandoni hasa kuhusu mada ya tendo la ndoa.

Greer (2000) anaegemeza uchunguzi wake kuhusu jinsia na lugha na kudai kuwa suala la uwezo kiume limeshamiri sana katika tamaduni nyingi za jamii na ni vigumu kulitupilia mbali hii ni kwa sababu lugha ndiyo huothi utamaduni. Anadokeza kwamba kuegemea kuumeni katika sehemu mbalimbali kwa mfano katika umri wa miaka kumi

na mitano mwanamume amepata uhuru wa kushiriki tendo la ndoa akilinganishwa na mwanamke ambaye hajaruhusiwa. Utafiti wake ulibaini kuwa jamii huamini kwamba ni jukumu la mwanamke kumtoshela mwanamume katika tendo la ndoa, lakini suala la mwanamke kutoshelezwa limepuuzwa. Anaendelea kudokeza kuwa mwanamke anatarajiwa kuutunza mwili wake na jinsi anavyoonekana anadhibitiwa hata katika upande wa mavazi. Suala la wanaume kudhihirisha kama wenye uwezo linasisitizwa sana. Mwanamke hufunzwa kuwaogopa wavulana ambao ni vichwa ngumu na wabakaji. Greer alibaini kwamba wasichana wanafunzwa sheria za kuwa wanawake tangu utotoni ndiposa wanakuwa na haya kuhusu miili yao na kupoteza uhalisia wao ikiwa ni pamoja na haki ya kujikomboa au kujitawala. Matokeo yake huwa ni kujidunisha, kujiona kuwa dhaifu, kujitenga, na kukosa furaha. Greer anadai kuwa wanawake wanastahili kujua na kuikubali miili yao. Kazi ya Greer ulifaa sana utafiti huu, kwa sababu mafunzo ya jando katika jamii ya Wakipsigis yanahimiza mada ya tendo la ndoa na yalichangia kufanikisha malengo ya utafiti huu. Masuala ya tendo la ndoa hayazungumziwi hadharani. Kuzungumzia au kutaja masuala haya huwa mwiko kama alivyodai wa Bakhtin (1984) katika Mwamzandi (2001), yanapozungumziwa lugha ya tasfida au ya kimafumbo hutumika hasa wanaporejelea sehemu za siri (Nkumbo, 2013).

Huang na Tian (1990) wanatafsiri mwiko kuwa ni jambo au kitu ambacho kimekatazwa kutokana na mila na desturi za jamii. Kwa kawaida, wengi huchukulia mafungu ya maneno ambayo ni mwiko kama lugha mbovu au chafu. Mambo hayo ni yale yanoyohusishwa tendo la ndoa na kutaja sehemu nyeti au za siri za mwili. Hivyo basi, suala la tendo la ndoa huelekezwa na utamaduni. Watu wengi huibua hisia tofauti za kujitambulisha kijinsia na kuonea shauku muktadha wao wa wakati maalum katika historia, kabila lao, hadhi yao ya kijamii, dini na mipangilio inayoelekeza majukumu ya kijinsia.

Kwa mujibu wa (Foucault 1978; Rubin 1984). Joseph na Lewis, (1981) wanadai kuwa wanawake kutokana na miundo ya kitamaduni ya jinsia na tendo la ndoa, huishi maisha ya wasiwasi na duni kati ya raha na hatari. Utafiti wetu ulikaribiana na kazi ya wataalamu hawa kwa sababu suala la tendo la ndoa ni siri katika jamii yoyote ile, lakini kwa upande mwingine ulitofautiana kwa kuwa walengwa katika utafiti walikuwa wavulana hivyo basi tulikusudia kuchunguza mikakati ya diskosi ya tendo la ndoa.

Ulinganuzi wa jinsi njia ya usemi wa lugha hutumika kuongea kuhusu tendo la ndoa ulifafanuliwa na Cameron na Kulick (2003). Walijadili zaidi kuhusu jinsi maoni yanavyojengwa kuhusu tendo la ndoa na kudai kuwa kwa miaka mingi tendo la ndoa limeonekana kama tabia fulani na kuona kuwa ni bora au si bora. Wanaongeza kuwa usomi kuhusu masuala ya tendo la ndoa sharti uzingatie matumizi mbalimbali ya lugha. Kulingana nao, kile tunachofahamu na kuamini kuhusu tendo la ndoa ni sehemu ya mzigo tunaouleta katika tendo hilo na ujuzi wetu hautokani na tajriba ya kwanza, bali mambo mbalimbali yanayoizunguka jamii. Lugha huzalisha jinsi tunavyoshabikia jambo kulitambua mila na desturi za tendo la ndoa. Lugha pia huadilisha nafsi na kujenga ujuzi wa mada ya tendo la ndoa ikihusisha kiwango cha maingiliano na utafida. Kutokana na mwelekeo huu, utafiti huu uliangazia lugha inayotumika hasa katika kiwango cha semantiki katika mafunzo ya tendo la ndoa kwa muktadha wa jandoni katika jamii ya Wakipsigis.

Kwa mujibu wa Christensen na Miller (2006), diskosi ya tendo la ndoa ni jambo la kawaida katika maisha ya ndoa na huhusisha masuala mengi yanayohusiana na mtagusano wa kijamii na mtazamo wa hisia tofauti. Walibaini kuwa matatizo mengi ya kifamilia hasa kuhusu tendo la ndoa yamesababisha talaka kwa familia nyingi. Naye Benjamin (2006) katika jarida lake la lugha na tendo la ndoa alidhamiria kuwasilisha utafiti kuhusu uundaji elezi wa utambuzi, ashiki, siasa na uana kwa nchi za nje akilenga kazi katika isimu. Benjamin alifafanua kwa mawanda mapana kuhusu uchanganuzi wa isimu tumizi, pragmatiki, semantiki, isimu anthropolojia, uchanganuzi matini na kanuni zingine za lugha. Kazi ya watalaam hawa ilichangia maswali ya utafiti huu hasa katika kiwango cha isimu ambacho ni semantiki. Isitoshe, matini za uana na tendo la ndoa ilifaa sana katika utafiti huu.

Onyango (2011) alifafanua jinsi mwanamke hujikakamua kumfurahisha mumewe katika tendo la ndoa kwa mazungumzo na pia kutumia lugha za ishara. Mwanamke hujaribu kutumia lugha ya upole na unyenyekevu kwa mumewe na mara nyingi anastahili kuomba msamaha anapokosea. Anaendelea kusema, mwanamke asipofanya hivyo, anamwacha mumewe katika hali ya kutafuta wanawake wengine. Kulingana naye, katika baadhi ya jamii za Magharibi nchini Kenya wanaotagusana na Waganda, mwanamke hujitahidi kujipendekeza na kumvutia mumewe katika tendo la ndoa ili aweze kumkinga dhidi ya wanawake wengine kutoka Uganda ambao wanaweza

kumvutia na kumnyakua. Mwanamke asiyemtoshela mumewe katika tendo la ndoa huonekana kama asiyefaa. Majukumu ya mwanamke ni mengi mno kama vile; kupika, kulea, kulima, kuchota maji, kutafuta kuni na licha ya hayo anatarajiwa kumfurahisha mumewe katika tendo la ndoa. Kazi ya Onyango iliufaa utafiti wetu katika kufanikisha malengo ya utafiti japo kazi hii ilijikita katika muktadha wa jandoni.

Ogechi (2005) na Beck (2015) walitafiti kuhusu lugha ya vijana na wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Kenya kwa kuangazia tendo la ndoa na maradhi yanayoambukizwa kutokana na kushiriki tendo hilo. Katika tafiti zao, walibaini kuwa kuna ubunifu mkubwa miongoni mwa vijana katika kurejelea masuala hayo. Wasomi hawa wanadokeza kuwa watetezi, wahudumu, na watekelezi wa sera za afya, sharti wahusishwe na watumie lugha bunifu ya vijana hususan sheng kwa lengo la kufanikisha utoaji wa huduma za afya. Gonzalez na Anna-Brita (2011) pia walichunguza ubunifu wa lugha baina ya vijana wanaozungumza lugha ya Kiingereza na Kihispania wakilenga zaidi utumizi wa lugha ya mtaani (slang) katika mada za tendo la ndoa. Utafiti wa Gonzalez na Anna-Brita ulibaini kuwa matineja wa Kihispania huzungumzia kuhusu mihadarati ilhali matineja wa Uingereza huzungumzia mambo ya tendo la ndoa. Kazi za wataalamu hawa ziliufaa utafiti wetu katika kufanikisha malengo na kuweka wazi pengo la utafiti.

#### **2.4 Msingi wa Nadharia**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi (UHU) kwa kuzingatia mkabala wa historia. UHU ilitokana na uhakiki wa isimu ambayo ilitoka mwaka wa 1970. Iliasisiwa kama ruwaza ya wasomi mwanzoni mwa 1991 kutokana na warsha huko Amsterdam, Januari ya mwaka wa 1991. Hii ilitokana na mchango wataalamu mbalimbali kama Teun Van Dijk, Norman Fairclough, Gunther Kress, Theo van Leeuwen na Ruth Wodak waliochukua muda wa siku mbili kujadiliana nadharia na mbinu za utafiti wa uchanganuzi matini na hasa Uchanganuzi Hakiki Usemi. Mkutano huu wa Amsterdam ulianzisha taasisi iliyoanzisha masomo ya kubadilishana kwa miaka mitatu. Aidha, miradi mingi ya pamoja na uhusiano mwema ulianzishwa kati ya wataalamu mbalimbali na mielekeo pamoja na maswali spesheli ya usemi na jamii ambayo ilileta mielekeo tofauti ya wataalamu mbalimbali pamoja. Mwanzo huu wa ruwaza ya uchanganuzi hakiki usemi, ikatiliwa nguvu kwa kuanzishwa kwa majarida ya, *Discourse and Society* (1990) na Van Dijk, *Language power and ideology* (1989)

na Ruth Wodak, *Language and power* (1989) na Norman Fairclough, *Prejudice in Discourse* (1984).

Uchanganuzi Hakiki Usemi kwa mara ya kwanza ulianzishwa na shule ya Lancaster ambamo Norman Fairclough alikuwa mtu mashuhuri. Pia Wodak amechangia sana katika uwanja huu. Msingi wa nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi ni kuwa lugha ni shughuli ya kijamii (Fairclough na Wodak 1997), na huchukulia matumizi ya lugha kimuktadha kuwa muhimu (Wodak 2000c). Uchanganuzi Hakiki Usemi hutilia maanani uhusiano kati ya lugha na uwezo. Kiambajengo msingi cha uchanganuzi ni matini au usemi kwani, ndicho kipashio muhimu cha mawasiliano. Nadharia hii huchanganua muundo ulio wazi na usio wazi wa mahusiano ya kimamlaka, kibaguzi, kiuwezo na kiutawala ambayo hudhihirishwa na lugha.

Ingawa kuna nadharia zingine ambazo zinaweza kuhusishwa na utafiti huu, hata hivyo, mtafiti alichagua nadharia hii kwa kuwa ina nguzo ambazo ni muhimu katika kubainisha, kufafanua maana ya undani kuhusu masuala ya kihistoria na utamaduni wa jamii na kufanyia utafiti suala la diskosi ya tendo la ndoa. Hivyo basi, nadharia hii ilichangia kufanikisha malengo ya utafiti huu.

#### **2.4.1 Uchanganuzi Usemi-Mkabala wa Kihistoria**

Mafunzo ya jandoni husheheni historia ya jamii husika na mchakato wa mafunzo hayo huhusisha mikakati mbalimbali. Hivyo basi, uchanganuzi usemi mkabala wa kihistoria ulikuwa nadharia mwafaka ya kuchanganua mafunzo haya kwa kuangazia kwa undani mikakati mbalimbali inayohusiana na masuala ya jandoni. Kwa mujibu wa Wodak (2001), kubainisha msimamo wa usemi na matini, dhana ya mkakati ni kipengele muhimu kwa kuwa huangazia uhakika na dhamira ya msemaji. Kazi ya Reisigl na Wodak (2001) inaeleza kuwa mikakati ya usemi huzungumziwa wanapochanganua usemi wa kiubaguzi na upinzani wa kisemiti kwa kuirejelea nadharia ya uchanganuzi usemi. Utafiti wa Wodak (2001) imeorodhesha aina tano za mikakati ya usemaji;

1. Mkakati wa urejelezi.
2. Mkakati wa uarifishaji.
3. Mkakati wa mkabala.
4. Mkakati wa ubishi.
5. Mkakati wa ufifishaji na uongezaji wa makali.

#### **2.4.2 Mkakati wa Urejelezi/unominishaji**

Mkakati wa unominishaji huhusika na jinsi mtu anavyotajwa na kurejelewa kilugha. Unominishaji huwakilisha wahusika wa kikundi katika jamii Wodak (2001). Ifahamike kwamba mkakati huu hutoa taswira ya mhusika ambaye huwakilisha kundi fulani katika jamii. Kimsingi, kifaa kitumiwacho kumrejelea mhusika huwa ni kibayolojia, kiasili na kitamathali. Katika utafiti huu mkakati huu ulitumiwa kutambulisha wahusika au vifaa teule vilivyoyojenga msingi ya utafiti.

#### **2.4.3 Mkakati wa Uarifishaji**

Mkakati huu huja baada ya unominishaji, hivi kwamba baada ya kutambua mhusika au kundi fulani mkakati wa uarifishaji hufuata. Mkakati huu hueleza tabia kwa njia hasi na chanya kwa kutumia maelezo ya lugha kwa uwazi. Mkakati huu hulenga kumtambulisha mhusika kwa njia ambayo inaweza kupunguza au kuzidisha namna wanavyosawiriwa. Katika utafiti huu mkakati huu utamulika kwa undani zaidi hulka, sifa na mwenendo wa mhusika, kundi au chombo fulani kilichojenga msingi wa utafiti.

#### **2.4.4 Mkakati wa Mkabala**

Mkakati huu hutambuliwa kwa unukuzi, utoaji wa taarifa, matumizi ya maelezo na masimulizi. Wanenaji hudhihirisha haya kwa matumizi ya vihusishi, urudiaji, matumizi ya ishara, urudiaji na ukwepaji wa matamshi fulani. Mkakati huu hulenga kutoa mwelekeo wa mhusika mnenaji katika matamshi yake au kwenye maandishi. Mkakati unanua kueleza jinsi jambo au tendo fulani inavyofasiriwa katika jamii husika na inavyochukuliwa na itikadi za jamii. ulitumika katika kutathmini mikakati ya lugha inayotumika katika diskosi za tendo la ndoa.

#### **2.4.5 Mkakati wa Ubishi**

Barasa (2014) alisema dhana ya topoi hutumika katika mkakati wa ubishi kama mbinu ya upembuzi. Mkakati huu huwa na ukuruba wa ndani wa matukio ya ushawishi na uhalalishaji usemi wa kibaguzi. Utafiti huu unahusu usemi wa sherehe za tohara ambapo kuna msukumo wa kueleza dhana ya topoi, jinsi inaweza kubainishwa katika usemi. Topoi hufafanuliwa kama sehemu ya ubishi inayohusiana na uwajibikaji wa ukweli. Barasa (2014:69) akimnukuu Wodak (2006:74) anaeleza topoi kama jambo lenye maana, faida, kasoro, maelezo, tafsiri ya njia, utu, haki, mzigo, uwajibikaji, fedha, sheria na haki, historia, utamaduni, dhuluma, tishio, hatari na upimaji. Barasa (2014) akimnukuu Zagar (2010) alisema hakuna aina ya topoi ambayo inaweza kuchangunulia

usemi. Anaongeza kuwa topoi zaidi zinaweza kuongezwa kwenye orodha ya topoi za awali na pia topoi zinaweza kuondolewa kwa orodha ya awali. Katika utafiti huu mtafiti alichagua topoi chache kutegemea utaratibu mahususi. Barasa (2014) akimnukuu Reisigl na Wodak (2001) alitaja kuwa mikakati ya ubishi hutoa ishara chanya au hasi kuhusu mhusika au kundi fulani. Topoi hutumiwa kutoa usemi wa kupendelea au kubagua ili kuhalalisha jambo.

#### **2.4.6 Mkakati wa Ufifishaji na Uongezaji Makali**

Reisigl na Wodak (2001) walieleza mkakati huu kuwa ni wa kuvumisha ufahamu na ukubalifu wa vihusishi. Mkakati husaidia katika kupunguza na kuvumisha hadhi ya kihisishi kwa kufifisha au kuongeza makali nguvu ya usemi ilokusheni. Utafiti huu umebainisha jinsi wahusika, kundi au vyombo teule vilitumika katika usemi wa kuweka uzito au kupunguza uzito. Mkakati huu ulitoa mwanga wa jinsi jambo linavyofasiriwa na kudhaniwa kutegemea uwezo wa nadharia. Katika utafiti huu mihimili ya urejelezi, ubishi na ufifishaji ilitumika katika kuchanganua mada mbalimbali zilizojitokeza. Mihimili ya mkabala na uarifishaji ilitumika katika kutathmini mikakati diskosi katika mafunzo ya tendo la ndoa.

## **SURA YA TATU**

### **MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.1 Utangulizi**

Katika sura hii mtafiti alijadili muundo wa utafiti pamwe na mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Maelezo ya muundo wa utafiti, eneo la utafiti, watafitiwa, sampuli, mbinu za ukusanyaji wa data na jinsi data ilivyochanganuliwa yametolewa ufafanuzi wa kina. Mtafiti alitumia njia ya kuzuru na kusoma maktabani na nyanjani. Mtafiti alitembelea maktaba za vyuo vikuu vya Nairobi, Egerton, Laikipia, Kisii na Kabianga ili kusoma tafiti za hapo awali kuhusu diskosi za tohara. Tafiti katika maktaba zilimsaidia mtafiti kujenga na kukuza msingi wa utafiti huu.

#### **3.2 Muundo wa Utafiti**

Muundo wa utafiti huu ni wa kiuthamano ambapo uchanganuzi kifani ulihusishwa. Kothari, C. R. (1990) anafafanua kuwa utafiti wa kina hurekodi matukio na kufafanua namna matukio yalivyo. Mtafiti alifafanua aina mbalimbali za mada zinazofunzwa jandoni kuhusiana na tendo la ndoa, mikakati ya diskosi za tendo la ndoa tofauti tofauti katika miviga ya sherehe za jandoni. Kulingana na Oso na Onen (2005) anaeleza kwamba uchanganuzi wa kifani huhusisha muundo na utaratibu ambao ujumlisha eneo ndogo pamoja na watu wachache huchunguzwa kwa undani na kikamilifu katika kiwango fulani cha kutafitiwa. Fauka ya hayo, muundo huu unafaa kwa vile husaidia mtafiti kudadavua na kufafanua dhana fulani inayotafitiwa badala ya kufanyiwa ukadiriaji wa dhana hiyo. Muundo wa uchanganuzi kifani ulikuwa faafu sana katika utafiti huu kwa kuwa ulimwezesha mtafiti kufanya uchunguzi kwa kina wa suala lililotafitiwa kwa kutumia sampuli ndogo ambayo ilisimamia sehemu nzima kwa jumla. Muundo wa uchanganuzi kifani ulitumika katika kuchanganua diskosi za tendo la ndoa katika kuendeleza mafunzo ya jandoni.

#### **3.3 Mahali pa Utafiti**

Utafiti huu ulifanywa katika kaunti ya Bomet na hasa katika Kaunti ndogo za Chepalungu, Sotik na Bomet Mashariki. Maeneo haya yaliteuliwa kwa kuwa ni chemichemi ya utamaduni wa Wakipsigis na utamaduni wao haujaathiriwa kwa kiwango kikubwa na maendeleo ya miji na tamaduni za jamii zingine pamoja na za kigeni. Sababu ni kwamba sehemu hizo ziko mbali na miji mikuu katika maeneo hayo ya nchi ya Kenya na hivyo ni wazi kwamba haina athari kubwa ya dini na teknolojia

ikilinganishwa na sehemu zingine kama kaunti ndogo za Bomet ya kati na Konoin ambazo zinapatikana na miji ya Bomet na Kericho. Sehemu hizi ziliteuliwa kwa kuwa sherehe za jando hutiliwa mkazo sana na wazee wakongwe wenye tajriba nyingi huongoza sherehe hizo. Mtafiti aliweza kutangamana na ngariba na watahiriwa kwa lengo la kufahamu zaidi kuhusu mafunzo ya jando hususan diskosi za tendo la ndoa.

### **3.4 Njia za Utafiti**

Mbinu zifuatazo zilitumiwa na mtafiti kukusanya data: Mahojiano, kinasasauti, uchanganuzi wa yaliyomo makatabani, kamera za kunasa picha na kutazama ili kupata data madhubuti.

#### **3.4.1 Utafiti Maktabani**

Mtafiti aliweza kuzuru katika maktaba mbalimbali za vyuo vikuu ili kuchunguza yaliyoandikwa na watafiti wengine kuhusu mada hii na mada zingine zinazohusiana na utafiti huu. Mtafiti alichunguza baadhi ya kazi alizoziona kuwa na manufaa kwa utafiti huu. Aidha, alisoma kazi za wataalamu mbalimbali kama vile tasnifu, majarida na vitabu ambavyo vilifaa utafiti huu.

#### **3.4.2 Utafiti Nyanjani**

Kwa sababu utafiti huu ulifanywa nyanjani mtafiti alizuru nyanjani ili kukusanya data. Aliwahoji wanajamii na kunasa mahojiano hayo kwa ajili ya kuichanganua data hiyo baadaye. Mtafiti alitarajia kuwahoji ngariba watatu kutoka maeneo matatu ambayo hayajaathirika na teknolojia na dini. Aidha, wanaume wawili ambao wamefuzu jandoni pia walihojiwa, wanaume hao waliteuliwa kutoka mfumo wa rika zinazotambulika na jamii. Sampuli hizi zilikuwa za kuridhisha shughuli za utafiti huu na iliwakilisha wanajamii wote.

### **3.5 Kikundi Lengwa**

Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006), wanaeleza kwamba walengwa wa utafiti ni kundi la watu, vitu au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzitumia katika utafiti wake. Uteuzi wa kundi lengwa ni utaratibu unaotumiwa na mtafiti kuchagua orodha za vitu ama watu kwa minajili ya sampuli yake ya utafiti(Sharma G, 2017).Utafiti huu ulihusisha makundi mawili ya wanajamii na elementi kadhaa katika sehemu ya utafiti ili kupata data ya utafiti huu. Kikundi cha kwanza kilikuwa ni mangariba wote ambao huongoza shughuli za jandoni na pili ni wanaume au vijana wa kiume ambao wamefuzu

jandoni. Japo utafiti ulifanyika katika kaunti ya Bomet, ambapo mtafiti aliteua sampuli, hiyo sampuli ya walengwa iliwakilisha wanajamii wa Kipsigis. Sehemu hii iliteuliwa kwa kuwa sherehe za jando hutiliwa mkazo na wazee wakongwe wenye tajriba nyingi huongoza sherehe hizo.

### **3.6 Sampuli**

Kwa mujibu wa Kothari (2004) anafafanua sampuli kama kundi la watu fulani lililomo katika mkusanyiko wa watu ambalo mtafiti ana imani litampa habari anazozitaka katika uchunguzi wake. Fauka ya hayo, mtafiti aliteua sehemu ndogo ya wanajamii ambao huitwa kundi lengwa. Sampuli iliteuliwa katika maeneo ya utafiti huu kwa kujikita katika mbinu mbili ambazo ni: sampuli nasibu na lengwa. Katika utafiti huu, sampuli tano ziliteuliwa ambazo ni mangariba watatu na watahiriwa wawili.

#### **3.6.1 Mbinu za Kuteua Sampuli**

Kuteua sampuli ni kitendo ambacho hujumlisha washiriki au watakaowakilisha kikundi kikubwa cha watu ambacho husaidia katika kupatikana kwa habari na data za utafiti. Haya ni kwa mujibu wa Kothari (2004). Kwa minajili ya utafiti huu, mtafiti alitumia mbinu ya sampuli lengwa.

#### **3.6.2 Usampulishaji Lengwa**

Kwa mujibu wa Kombo na Trump (2006) wanafafanua kwamba mbinu ya usampulishajii lengwa ni kuteua sampuli ya utafiti ambayo hutoa idhini ya kuteua atakayetoa taarifa na anaaminika kwamba ana habari muhimu ambazo zitasaidia kuyajibu maswali ya utafiti wake. Usampulishaji ni hatua za kuteua kundi ndogo kutoka kwenye kundi kubwa la watafitiwa ukiwa na kusudi la kukadiria kuhusiana na kundi lililoteuliwa (Sigh, 2007). Sampuli hii ni ya kimakusudi na ilitokana na malengo ya mtafiti. Sampuli ya aina hii huhitaji mtafiti kufanya maamuzi ya watafitiwa ambao wanajumuishwa katika utafiti wake. Hali hii hutokea wakati mtafiti anapohitaji data mahususi ambazo kwa mtazamo wake hupatikana katika sampuli aliyochagua kufanyia uchunguzi (Oso na Onen, 2009; Mugenda na Mugenda, 2003). Kwa sababu ni vigumu kupata data katika jamii yote ya Wakipsigis, mtafiti aliteua wale wanaoishi katika kaunti ya Bomet na hasa katika kaunti ndogo tatu zilizotambuliwa. Sampuli lengwa ilimwongoza mtafiti kupata wanajamii ambao wana tajriba kuhusu mafunzo ya jandoni. Utafiti huu ulihusisha watu tano wa kutoa taarifa; ngariba watatu na watahiriwa wawili. Mbinu hii ilimwezesha mtafiti kupata data inayofaa ili kufanikisha madhumuni ya

utafiti huu. Kombo na Trump (2006) wanaeleza kuwa sampuli ya nasibu ni mbinu ambayo humpa kila mhusika miongoni mwa kundi lengwa nafasi sawa ya kuteuliwa ili kushiriki katika utoaji wa habari muhimu za utafiti. Mtafiti alitumia mbinu hii katika utafiti huu kuteua kundi la washiriki ambao wamefuzu jandoni ili kupata mada walizofunzwa kuhusu tendo la ndoa. Kundi hili lilijumuisha wanaume kutoka rika zote saba zinazotambulika na jamii. usampulishaji nasibu ulifanywa kwa vile ni vigumu kuwasaili wanaume wote ambao wamefuzu jandoni.

### **3.7 Mbinu za Kukusanya**

Hakuna mbinu mojawapo ya utafiti ambayo huwa imejitosheleza. Mbinu za utafiti hutegemea data atakayokusanya mtafiti. Ukusanyaji wa data huongozwa na malengo ya mtafiti. Ukusanyaji wa data wa kazi hii ulihusisha kusoma tasnifu, majarida na vitabu ili kupata yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti pamoja na nadharia Uchanganuzi wa Usemi Mkabala wa Historia. Katika utafiti huu mtafiti alitumia majarida, maoni na vitabu vya wataalamu mbalimbali vinavyopambanua kwa kina diskosi za kujamiiana na mafunzo ya jandoni. Data hiyo ilitufaa sana katika kubainisha na kuchanganua diskosi katika jamii. Mahojiano, masimulizi na majadiliano ndizo mbinu kuu zilizotumiwa katika kupata data thabiti wa kutegemewa na vilevile zilifaidi madhumuni na kujaza pengo lililodhamiriwa. Walengwa walitarajiwa kuonyesha ushirikiano kwa kujibu maswali na kujieleza kwa njia wazi. Mtafiti aliwategemea baadhi ya wahojiwa na ngariba katika shughuli za fasili na fasiri ya data. Jambo hili lilikuwa la manufaa katika utafiti huu kwa sababu lilimpa mtafiti fursa ya kutumia ujuzi na tajriba ya wahojiwa katika uchambuzi wa data kwa kina. Wazo hili linashadidiwa na Wanjala (2015) ambaye alibainisha kwamba ili kuelewa dhana fulani lazima pawe na mchakato unaotakana na ushirikiano wa kiutendaji, uneni pamwe na usemezano kati ya mtafiti na jamii inayotafitiwa. Dhana hii inaungwa mkono na Matinde (2012) anayesema kwamba jambo linaeleweka vyema kupitia kwa kuuliza maswali kati ya mtendaji, wasikilizaji na mhakiki katika muktadha maalum wa mazungumzo. Wasomi hawa wanakubaliana kwamba ushirika, ushauri na maagano kati ya mhakiki, mtunzi na hadhira ni suala nyeti.

### **3.8 Uchanganuzi wa Data**

Mugenda na Mugenda (1999) wanasema katika utafiti wa kiuthamano, data ukusanywa na kuchanganuliwa kwa mwambatano wa moja kwa moja. Data iliyopatikana ilipangwa

kwa utaratibu kwa kuongozwa na madhumuni ya utafiti. Katika uchanganuzi huu, mtafiti aliangazia mada za diskosi za tendo la ndoa na mikakati ya mafunzo. Jumla ya matini za miviga ya jando kumi na tatu zilizoakisi diskosi za tendo la ndoa zilikusanywa na kuchanganuliwa. Miviga hiyo kumi na tatu ziliwekwa katika matini ya lugha ya Kipsigis na kutafsiriwa katika lugha ya Kiswahili. Tafsiri huru ilizingatiwa. Mtafiti alichanganua data kwa kujikita katika madhumuni na mihimili ya nadharia kwa kuzingatia kauli na simulizi za wahojiwa mahususi kuhusu mada za diskosi za tendo la ndoa, pamoja na kuhakiki tamathali za usemi kwa kujikita katika kipengele cha kiisimu ambacho ni semantiki.

Kulingana na Du Bois, Schutze-Coburn Cumming na Danao (1993), wanafafanua kwamba unukuzi wa matini kama utaratibu wa kuandaa maandishi au mazungumzo ili yatumiwe katika uchanganuzi. Kunazo aina mbili kuu za kunukuu; unukuzi mpana na finyu. Kwa mujibu wa watafiti hawa, unukuzi ambao ni mpana huhusisha taarifa zote za msingi ambazo zilinukuliwa kwa mfano maneno tamkwa, zamu za mazungumzo, vituo, vicheko na milio. Kuhusu unukuzi finyu wanaeleza kwamba unahusu ukamilifu kwa sababu toni, lafudhi na kelele zingine hujumlishwa. Katika utafiti huu tulitumia unukuzi mpana kwa kuzingatia maneno halisi na walionena maneno hayo. Fauka ya hayo tulichanganua data kwa kujikita katika vipashio vya lugha kama vile; nomino, vishazi na vitenzi vinavyosawiri diskosi za tendo la ndoa. Uchanganuzi ulizingatia baadhi ya tamathali za usemi kama vile tashbihi, chuku, tasfida, taswira, taashira, jazanda na istihizai kwa msingi wa kisemantiki kama wanavyoeleza Habwe na Karanja (2004) semantiki ndio mwavuli wa vipengele vingine vya kiisimu. Zaidi ya hayo ni kwa sababu dhima ya lugha ya binadamu ni kufaulisha mawasiliano ambayo yanasababisha jamii kupiga hatua kimaendeleo. Mawasiliano baina ya binadamu husababishwa na hali ya binadamu kuwa na uwezo wa kufasiri maana ya kile ambacho kinasemwa au kutiwa katika maandishi na binadamu mwingine. Kulingana na Simala (2013), semantiki ndicho kipengele ambacho kina uwezo wa kutekeleza jambo hili na hivyo basi kuleta maendeleo katika jamii inayohusika. Katika utafiti huu maana ya kisemantiki ilikuwa muhimu kwa sababu ilituwezesha kuchanganua diskosi za tendo la ndoa kwa kujikita katika fasiri ainati za maana.

### **3.9 Tafsiri ya Data**

Ngariba na watahiriwa katika jamii ya Kipsigishutumia lugha ya Kipsigis wakiwa jandoni. Data iliyokusanywa katika lugha hii ilifanyiwa tafsiri katika lugha ya Kiswahili. Mtafsiri huwa na dhima kuu ya kuhifadhi data katika maana asilia hata baada ya kufanya tafsiri (Hatim na Mason, 1990). Ili kufaulu katika kutafsiri mtafiti aliongozwa na mambo kadha kama vile; muktadha wa mazungumzo(jandoni) na ujumbe, masuala na muktadha wa kijamii na muktadha wa Kipragmatiki ambao huhusisha wakati, mahali, utamaduni na diskosi ambazo mazungumzo haya huzunguka (Yieke, 2002). Hatim na Mason (1990) wanadokeza kanuni kuu za tafsiri kama vile; mawasiliano, Pragmatiki na Semitiki ambazo taratibu zote humweka anayetafsiri kuwa nguzo kuu katika mchakato huu wa mawasiliano (Ndambuki, 2010). Ili kuhakikisha kuwa kuna mawasiliano kutoka kwa lugha asili hadi lugha lengwa, ni lazima mtafsiri ajibidiishe kukabiliana na changamoto za kijamii wakati ambapo anatafsiri kutoka kwa lugha neni hadi kwa msikilizji wa lugha ya pili ambapo wote wawili wapo kwenye mfumo mmoja wa kijamii. Zaidi ni kuwa mtafsiri aliepuka tafsiri sisisi na ya neno kwa neno kwa ajili ya udhaifu wazo katika mchakato wa kutafsiri matini. Fauka ya hayo mtafiti ni miongoni mwa wanajamii wa jamii hii hivyo basi hakupata tatizo katika kutafsiri data hii.

### **3.10 Uzingativu wa Maadili**

Kulingana na Padgett (2002), masuala ya kimaadili yanafaa kuzingatiwa iwapo yalijitokeza katika aina mbalimbali za utafiti. Masuala hayo ni kama vile kuomba kibali cha utafiti katika eneo la utafiti, kuzingatia usiri, uwazi, hiari ya kushiriki kwa wasailiwa na utiifu miongoni mwa mengine. Mtafiti aliomba kibali cha kufanya utafiti na kufuata hatua kadhaa zinazolengwa kuhakikisha kuwa maadili ya utafiti yalizingatiwa katika utafiti huu. Kwanza, mtafiti aliomba idhini kutoka kwa wakuu wa chuo kikuu cha Laikipia na pia idara inayohusika na masuala ya utafiti nchini Kenya (NACOST). Mtafiti aliwahakikishia watafitiwa wake kwamba majina yao yote hayatatajwa katika tasnifu. Utafiti huu haukujihusisha na masuala yoyote ambayo yataathiri mazingira, usalama au afya za watafitiwa.

## SURA YA NNE

### UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

#### 4.1 Utangulizi

Katika sura hii matokeo ya utafiti yamewasilishwa kulingana na maswali ya utafiti na kuchanganuliwa kwa misingi ya nadharia ya Mkabala wa Kihistoria. Swali la kwanza katika utafiti huu lilikuwa ni; mada zipi za diskosi ya tendo la ndoa zinazodhihirika katika mafunzo ya jandoni katika jamii ya Wakipsigis? Hivyo basi, sehemu ya kwanza katika sura hii itahusu kujibu swali hili ambapo mada mbalimbali zilijitokeza katika mafunzo ya jando. Uchanganuzi ulifanywa kwa kujikita katika mihimili ya urejelezi, ubishi na ufifishaji.

Sehemu ya pili inahusu swali la pili la utafiti ambalo ni, mikakati ipi inayotumiwa katika mafunzo ya diskosi za tendo la ndoa zinazofunzwa jandoni katika jamii ya Wakipsigis? Mikakati hii imewasilishwa na kuhakikiwa katika mikakati ya mbinu za lugha. Uchanganuzi ulifanywa kwa kujikita katika mihimili ya uarifishaji na mkabala.

Ili kurahisisha urejelezi wa data na kuhakikisha kuwa kuna utaratibu mzuri wa mjadala na usomaji, mtafiti alipanga data yake kwa kuisimba. Usimbaji huu ulihusisha alfabeti na tarakimu kwa pamoja kuashiria yafuatayo: NgKvMd- Ng- ngariba, Kv- kiviga na Md- mada. Tarakimu ziliongezewa kwenye ufupisho huu kuashiria ngariba wa kwanza, kiviga cha kwanza na aina mbali mbali za mada za tendo la ndoa kama vile, Ng1Kv1Md1, Ng2Kv2Md2 nakufululiza. Aidha watahiriwa walipewa kodi ya MtKvMd: Mt- mtahiriwa Kv- kiviga, Md-mada. Pia tarakimu za kufululiza zilitumika kama vile Mt1Kv1Md1 kuashiria mtahiriwa wa kwanza kiviga cha kwanza na mada ya kwanza. Katika utafiti huu picha pia zilitumika na kupewa kodi ya PMd; P- Picha, Md –mada. Kisha zikapewa kodi ya P1Md1,P2Md2 na kufululiza. Fauka ya hayo nyimbo ambazo zilitumika zilipewa kodi ya W1Md1 kuashiria: W1-wimbo wa kwanza Md1-mada ya kwanza.

#### 4.2 Mada za Tendo la Ndoa

Utafiti huu ulifanywa nyanjani hivyo basi, mtafiti alishiriki katika kukusanya data nyanjani. Aliwahoji wanajamii na kunasa mahojiano hayo kwa ajili ya kuichanganua data hiyo baadaye. Mtafiti aliwahoji ngariba watatu kutoka maeneo matatu, ambayo hayajaathirika kiteknolojia na dini; ngariba 1 (Ng1) kutoka kaunti ndogo ya Sotik,

ngariba 2 (Ng2) kutoka kaunti ndogo ya Chepalungu na ngariba 3 (Ng3) kutoka kaunti ndogo ya Bomet mashariki.

Aidha, wanaume wawili ambao wamefuzu jandoni pia walihojiwa, wanaume hao waliteuliwa kutoka mfumo wa rika zinazotambulika na jamii. Mtahiriwa 1 (Mt1) kutoka rika ya tatu ‘*korongoroo*’ ambaye alitahiriwa miaka 1985-1990. Mtahiriwa 2 (Mt2) kutoka rika ya sita ‘*kaplelaach*’ ambaye alitahiriwa miaka 1990 -2002. Sampuli hizi zilikuwa za kurahisisha shughuli za utafiti huu na iliwakilisha wanajamii wote.

Katika utafiti huu, mada mbalimbali zilijitokeza jambo ambalo linaoana na kauli ya Nandwa (1976) anayesisitiza kwamba shughuli za tohara zilikuwa muhimu sana kwa mtu binafsi na wanajamii kwa jumla, kwa sababu waliopashwa tohara walifunzwa maadili, utu uzima, siri tamaduni na historia ya jamii. Wasomi wengine kama vile Nyaga (1970) na Kanake (2001) wanaunga mkono kauli hii. Hata hivyo, mtafiti alijikita tu katika mada ambazo zinaambatana na madhumuni ya utafiti. Mada hizi zilijitokeza katika mahojiano kati ya mtafiti, ngariba na watahiriwa. Katika kuafiki madhumuni ya utafiti, mtafiti alizibaini mada zifuatazo; Idhini ya kushiriki tendo la ndoa (Md1) , kiwango cha kushiriki tendo la ndoa (Md2), Jinsi ya kushiriki tendo la ndoa (Md3) na Unyeti na maadili ya tendo la ndoa (Md4)

**Jedwali 1: Mada na diskosi zilizojitokeza kuhusu lugha ya tendo la ndoa na washiriki waliochangia.**

<b>Mada</b>	<b>Diskosi zilizojitokeza</b>	<b>Ngariba waliochangia</b>	<b>Watahiriwa waliochangia</b>
Idhini ya kushiriki tendo la ndoa	4	2	0
Kiwango cha kushiriki tendo la ndoa.	2	2	0
Jinsi ya kushiriki tendo la ndoa.	3	2	0
Unyeti na maadili ya tendo la ndoa.	4	2	2
<b>JUMLA</b>	<b>13</b>	<b>8</b>	<b>2</b>

Jedwali hili linaonyesha baadhi ya mada ambazo zilizungumziwa katika utafiti huu.

#### 4.2.1 Idhini ya Kushiriki Tendo la Ndoa

Idhini ya kushiriki ngono ni suala linalozingatiwa sana katika jamii ya Kipsigis. Hii ni hali ambayo mtahiriwa anaonyesha kwamba amekomaa na ako na ruhusa ya kutafuta mchumba na kufunga ndoa baada ya kutahiriwa (Greer, 2000). Wavulana ambao hawajatahiriwa hawana idhini ya kushiriki ngono katika jamii hii. Ng1KV1Md1 alieleza diskosi zinazotumika katika mafunzo haya kwa wavulana katika muktadha wa jandoni kwa kurejelea kiviga cha *yatitaet*.

##### **Ng1Kv1Md1 *Yatitaet* (kukata)**

*Tumin ini keyoe en kotap tumiin, murenik chekikiyatita ak kwonyik ichegen chekiyonchin kochut kotap tumiin. Machamdayat kochut ng'etik anan ko korusyek. Yoon kikonye keip mecheita ketieni, ago yakakoit motiryot kotoche en tekisto ne oo. Yotitoi motiryot anan ko tarji ng'etet agenga agenge ago nyolu koboor muitaet ng'etet ingeyotitoi, yekakobata yatitaet ako kamuita inendet, kosimee chepyosok konyil ang'wan, akomwa kamet anan ko chepyoso kole, "kokayam kwam sorom nemi buut kut". Kowool murenik en kipangenge kole "eeh kakoyam".*

##### **Tafsiri**

Kukabiliana na kisu cha ngariba kwa ujasiri ni jambo ambalo linashabikiwa sana na wanajamii na ni ishara ya ushujaa. Sherehe hii hufanywa katika mazingira ya jando (tazama P1Md1) na wanaume kwa wanawake ambao walipitia kisu cha ngariba ndio wanaoruhusiwa kuhudhuria. Sherehe hii inajulikana kama 'yatitataet' tafsiri yake ni kukata au kutoanisha. Ni hatia kwa wasichana wadogo kukaribia sehemu hiyo. Tendo hili huchukuliwa kuwa tendo la kisiri miongoni mwa wale waliopitia na wale ambao wanajitayarisha kupitia. Nyimbo mbalimbali huimbwa kabla kisu cha ngariba kuletwa na kisha ngariba kuwasili. Ngariba anapowasili, yeye hupewa heshima ya kipekee na kisha anaanza shughuli za kutahiri wavulana.

Kila mvulana anakabiliana na ngariba pekee huku wanawake na wanaume wakishuhudia kwa umbali. Katika mchakato huu, mvulana anapaswa kuonyesha ujasiri kwa kustahimili uchungu wa kisu. Wakati mvulana ametahiriwa bila kulia au kulalamika au kutikiza kichwa, basi

kina mama wanashangilia na nderemo mara nne. Baada ya nderemo, mamake mzazi au ajuza atainua mikono na kusema kuwa, ‘mvulana huyu ametoshea kula mnyama ambaye ana manyoya mdomoni huku wanaume wataitika kwa kauli moja ‘ametoshea’.



***P1Md1- chanzo ni utafiti wa mtafati nyanjani***

Katika jamii ya Kipsigis idhini ya kwanza ambayo mvulana anapewa ili kushiriki tendo la ngono lazima akabiliane na kisu cha ngariba. Maneno haya yanaashiria idhini ya kushiriki tendo la ndoa, punde tu atakapomaliza shughuli za jando, na baada ya miezi michache ya kupona. Kwa msingi wa nadharia ya Mkabala wa Historia mhimili wa urejelezi huhusika na jinsi mtu anavyotajwa na kurejelewa kilugha. Unominishaji huwakilisha wahusika wa kikundi katika jamii. Mhimili huu unatoa taswira ya mhusika ambaye huwakilisha kundi fulani katika jamii. Tunaona ajuza akirejelea idhini ya kushiriki ngono kwa kurejelea uke kama mnyama mwenye manyoya. Katika matini hii, ni ishara tosha ya kupewa idhini ya kutafuta mwanamke na kushiriki ngono naye. Msemaji wa maneno haya ni mhusika maalum siyo mwanamke yeyote, bali ni mhusika anayeaminika kupeana mamlaka. Maana ya ndani ya usemi huo ni kwamba; mnyama mwenye manyoya mdomoni ni uke wa mwanamke. Hii ni taswira ya uke wa mwanamke ambaye amekomaa. Kwa kawaida, nywele katika sehemu za siri huota wakati mtu amekomaa. Kwa hivyo, mvulana anapata funzo la kufahamu mwenye anafaa kumhusisha katika tendo la ndoa. Anafaa awe msichana aliyekomaa na yuko

tayari kuingia katika mahusiano ya kimapenzi. Uke wa mwanamke ambaye amekomaa huwa na kinena; sehemu iliyo chini ya tumbo. Sehemu hiyo huwa na nywele na hivyo basi taswira hiyo inalinganishwa na usemi wa maneno hayo kuwa mnyama mwenye manyoya mdomoni.

Katika muktadha huu neno ‘mdomo’ limetumika kama urejelezi wa uke wa mwanamke. Kwa kawaida, sehemu nyeti ya mwanamke huwa na sehemu mbili kuu; kinembe na uke. Kinembe ni kinyama kilichoko mlangoni mwa uke ambao husababisha mwanamke kupata ashiki ya kukutana na mwanamume. Hivyo basi, diskosi inafafanua uke wa mwanamke kama mdomo wa kufanikisha tendo la ndoa.

Usemi wa neno ‘kula’ limetumika kwa muktadha wa mapenzi kumaanisha kushiriki tendo la ndoa. Kwa hivyo mkakati wa urejelezi unatumika kurejelea tendo la ngono ambapo msichana ndiye *analiwa* na mvulana ambaye ametahiriwa. Katika jamii hii, mwanaume amepewa hadhi ya kuanzisha mchakato wa ngono na kwa kawaida mwanamume hutoa posa ya ndoa. Hivyo basi, mwanaume amesawiriwa kama mtumiaji mkuu wa uke wa mwanamke. Aidha, uke wa mwanamke umesawiriwa kama chakula ambacho mwanamume hula. Diskosi hii inafafanua kuwa siyo kila mtu hupewa ruhusa ya kula chakula hicho bali ni baada ya mvulana kupitia kisu cha ngariba. Huu ni mkakati wa ubaguzi unaobagua wavulana wa kushiriki tendo la ndoa.

### **Ng1Kv2Md1: Mutulik**

*Inoni ko tumdo ne kiyae yaan kamwetge tarusyek. Cheng'e tarusyot age tugul chemeriat anan ko chepto ne aechindos asi kobokokyi kirokto nekoikochin motiryot. Yekakonyoor chemeriat anan ko chepto konyolu kotinyeen kirokotet kubesto, suet ak batet yeityo komwa kole "karokoite tugukab lakwandit ako achopot atoi sobet age" kowalu agine chemeriat kule "Karataach" ak konam kirokto, kou yekakineet agine en menjo nenywan chemosyan, ak kwa oinet kowirchi beek kirokotet asi kolaa beek.*

### **Tafsiri**

Hii ni sherehe ya siku za mwisho katika jando baada ya watahiriwa kuoga miili yao, sherehe hii huitwa ‘mutulik’. Kila mtahiriwa anaruhusiwa kutafuta msichana ambaye ako katika unyagoni au yeyote aliyebaleghe; mwenye umri

sawa. Mtahiriwa hupewa kijiti maalum cha ngariba na anapaswa kugusa paja, kiuno au mgongo wa msichana kwa kuvuta kile kijiti katika sehemu hiyo ya mwili. Mvulana anapaswa kusema ‘nimepeana kila kitu cha utoto wangu na niko tayari kuingia sehemu ya mwisho ya maisha’. Iwapo msichana ako unyagoni anapaswa kuitika kwa kusema nimeipokea; huku akikabidhiwa kile kijiti. Katika upande mwingine, kuitika kwa msichana ni kuwa hata yeye amefunzwa na ngariba wao na alitarajia mchakato huo. Baada ya msichana kukishika, anatarajiwa kuenda mtoni na kukitupa kile kijiti kisombwe na maji.

Matini hii inadhamiria kueleza idhini ya kushiriki tendo la ndoa kwa wahusika wote wawili. Kwa kuzingatia mhimili wa ubishi ambao hutoa ishara chanya au hasi kuhusu mhusika au kundi fulani. Usemi huu ni wa kupendelea au kubagua ili kuhalalisha jambo fulani. Katika kauli hii wahusika wanajaribu kuhalalisha idhini ya kushiriki ngono kwa kutumia urejelezi wa neno kijiti kama sehemu za siri za kiume. Mvulana anaposema nimepeana kila kitu cha utoto wangu ni ishara kwamba ametoka utotoni na kuingia utu uzima. Pia kitendo cha kuoga miili yao kinaashiria kwamba wameacha mambo ya utotoni na sasa ni watu wazima ambao wako tayari kuingia katika ndoa. Matini inadhihirisha wahusika wote wanatarajiwa na jamii kuo au kuoleka na vilevile kushiriki tendo la ndoa baada ya kufuzu. Matumizi ya neno kijiti, ni ishara ya uume wa mtahiriwa mvulana ambao umeelekezwa kwa mwili wa msichana. Kijiti kinaashiria kwamba mvulana anatarajiwa kushiriki tendo la ndoa na msichana mwenye rika moja hivyo basi, wale ambao si wa hilo rika wanabaguliwa. Aidha, anaposema mvulana hupeana kijiti kwa msichana kunamaanisha kuwa jinsia ya kiume katika jamii hii ndiyo huanzisha mchakato wa tendo la ndoa. Msichana kwa upande wake huwa na jukumu la kukubali au kukataa posa au ombi la kushiriki tendo la ndoa. Isitoshe, upande wa wasichana wanaposema nimeipokea ni ishara ya kukubali kila ncha ya mwanamume kuingizwa kwa uke wake wakati wa tendo la ndoa. Msichana huchukua kile kijiti na kukitupa mtoni ni kauli inayorejela jinsi mvulana ameacha mambo ya kitoto na anafaa kuyasahau kabisa. Diskosi hii ni ishara tosha ya idhini ya kushiriki tendo la ndoa.

**Ng2Kv3Md1: Yatet ab oret (kufungua njia)**

*Kikyaen en mabwaita tumii, ako kikichomchin biik chekiba tum kityo en yotet.*

*Kitechee kiit neu munandet netinye kurget ak kinde kiptangasiat anan ko menet ak ketesyi suswek barak. En tumii kekanye tarusyot konyo akoi mundanet elee*

*miten chepkamet. Nyolu koboisyen tarusyek keldo kotyech ngatatiet akoileen kubestab chepkam konyil somok. Yekakotar kokochi kwanda kirokto ak panget asi kotil kirokotet, oloon testetai kotile kotebee motiryet kole “ngete nana mongete” ak kowool kwanda agine kole “ngetee” yeityo koketyi kotyech nyatatek ak koilen kameet kora kou ye kayai en chepkamet.*

### **Tafsiri**

‘Yatet ab oret’ (kufungua njia) ni sherehe ambayo hufanywa katika mahali mwafaka; mashariki mwa chumba cha mzee wa boma. Wahusika huwa ni mama mzazi, baba mzazi, ngariba, mvulana ambaye ametahiriwa na wanajamii ambao wametahiriwa. Ua linatengenezwa likiwa na lango ambapo mtahiriwa atapita kisha chini yake samadi ya ngombe au udongo uliofinyangwa huwekwa juu ya nyasi. Katika sherehe hii, msichana ambaye ni ndugu yake mtahiriwa atatumia mguu wake kumpaka mvulana mtahiriwa samadi au udongo mara tatu katika paja lake. Baada ya mchakato wa kwanza, mama mzazi atamsubiri pale na mtahiriwa akiwasili atapewa kijiti na babake mzazi na kukata kwa upanga. Baada ya kukata, ataukanyaga udongo ulio chini kwa kutumia mguu na kuwekelea kwenye paja la mamake na mamake pia atafanya hivyo. Hayo yakiendelea ngariba ataseme ‘itakatika ama haitakatika?’ huku baba mzazi akijibu; ‘itakatika’

Mchakato huu unalenga kuonyesha idhini ya kushiriki tendo la ndoa na mafunzo kadha yanoyohusiana na tendo hilo. Kwa mjibu wa mkakati wa ubishi ambao hutoa ishara chanya au hasi kuhusu mhusika au kundi fulani na topoi kutumiwa kutoa usemi wa kupendelea au kubagua ili kuhalalisha jambo hilo. Inadhihirika wazi kuhusishwa kwa msichana ambaye ni dadake, inamaanisha kuwa ana kibali cha kuhusishwa katika kushiriki kwa tendo la ndoa na jinsia ya kike. Vilevile, anaposema awepo mamake mzazi katika shughuli hii ni ishara ya kumtayarisha mtahiriwa kuzoea mwanamke katika maisha yake. Aidha, samadi au udongo ambao umeelekezwa kwa paja huku mguu ukitumika kama ala, ina maana ya idhini ya kushiriki tendo la ndoa. Udongo au samadi kuwekwa kwenye ua, unasawiriwa na kuamsha ashiki za ngono. Kwa kawaida ashiki au ari ya ngono huamshwa na mguso wa sehemu nyeti. Hivyo basi, katika mchakato huu mtahiriwa amepewa idhini ya kuamsha ashiki za jinsia ya kike ambayo itasababisha ushiriki ya tendo la ndoa. Kauli hizi zote zinajikita katika mhimili wa ubishi ili kuhalalisha kushiriki kwa ngono kwa mvulana ambaye amepashwa tohara.

Fauka ya hayo, kutengenezwa kwa ua maalum, ambapo mtahiriwa atapita kufanikisha mchakato huo, ni ishara ya kutoshea au kufuzu kutenda jambo fulani. Ua lenye kilango ni ishara ya uke wa mwanamke, aidha, ua hilo haliwezi kushirikishwa na mtu mwingine bali ni yeye pekee ndiye hupita. Ubinafsi huo hutambuliwa kwa maisha ya kawaida katika jamii hii kwamba mwanamke anafaa kushiriki tendo hili la ngono na mwanamume mmoja teule au bwanake tu.

### **Ng2Kv4Md1: Kweisit**


*Tarusyot age tugul kiinete kochop kweisit asi kopoisien en loget ab taritik. Kweisit kotinye kebeberwek somok, neta ko metit ne nerat, ak nebo aeng' ko borto ne koi ako tenden kikureen merenget ak nebo somok ko katutyet nekindoi kororik ab ingongiet. Katutyet kechope kokararanit kokerkeit ak saruryet ab tarikit asi ko maiywei taritik. Yekakochobok kweisit konyolu komanda tarusyek koba loget kocheng' taritik, ak yekakobor taritik koname motiryot ak konde mabwai asi kobangan en lain tarusyek kowiir sapaa age tugul. Oloon wiree tarusyot age tugul komwae motiryot kole "kwere" kowolu tarusyot kole "kwere".*

### **Tafsiri**

Wavulana wanapokuwa jandoni hufunzwa kutengeneza kifaa cha kutumia kuwinda ndege (tazama P2Md1, P3Md1 na P4Md1). Kifaa hiki huitwa 'kweisit'. Kila mmoja hutengeneza kifaa hicho ambacho hutumiwa kuwinda ndege. Taswira ya kifaa hicho huwa na sehemu tatu; kichwa, mwili na mkia. Sehemu ya kichwa huwa ni kubwa na pana, ilhali mwili huwa mwembamba na ni laini. Sehemu ya mwisho ni mkia ambao huwekwa manyoya ya kuku. Mkia hurembeshwa kwa lengo la kuisaidia kuongeza mwendo kasi wa kifaa hicho kwa mawindo. Aidha, urembeshaji huo huwa na lengo la kupumbaza ndege wasiogope kifaa hicho na wawe na dhana ya kufananisha na kuku au ndege mwenzao.

Kifaa hicho kinapokuwa tayari, vijana wanaenda nyanjani kuwinda ndege. Baada ya kufaulu katika mawindo. Ndege aliyenaswa na windo huletwa hadi pale jandoni na kuwekwa mahali mwafaka. Kisha vijana hawa wanaelekezwa na mzee ngariba kulenga shabaha moja kwa moja

wakiwa foleni. Katika mchakato huo kabla, mvulana kulenga shabaha, ngariba atatamka ‘ itagonga’ naye mtahiriwa atajibu ‘ itampata’



***P2Md1 chanzo: utafiti wa mtafiti nyanjani***



***P3Md1 chanzo: utafiti wa mtafiti nyanjani***



***PP4Md1 chanzo: utafiti wa mtafiti nyanjani***

Taswira ya kifaa hicho (P2Md1) kinaashiria uume. Hali hii ni matumizi ya mhimili wa urejelezi ambapo dhakari inalinganishwa na mshale. Kichwa chake ambacho ni pana

kushinda mwili na kina umbo sawa na dhakari. Aidha mwili wake mwembemba ni urejelezi sawa na mwili wa uume. Isitoshe, sehemu ya mwisho ni mkia, wenye manyoya. Huu ni urejelezi wa sehemu ya mwisho wa uume ambapo kuna mavuzi.

Wavulana wanaporuhusiwa kutumia kifaa hicho katika muktadha wa jando ni sawa na idhini ya kushiriki tendo la ndoa. Hii ni kwa sababu katika windo kichwa cha kifaa hicho hutangulia, kisha mwili wake. Vilevile, katika ngono kichwa cha dhakari pia hutangulia na huongoza shughuli hiyo, kisha mwili hufuata. Aidha, kauli kwamba kichwa cha kifaa hicho ndicho nguzo muhimu katika windo na hufanikisha shughuli za windoni ni urejelezi wa kichwa cha uume kama nguzo katika kufanikisha ushiriki wa tendo la ndoa. Dhana hizi zimejengwa kwa msingi wa mkakati wa ubishi kwani zinaashiria mambo chanya ambayo mtahiriwa atayatekeleza baada ya kupashwa tohara. Hivyo basi, kutengezwa na kutumiwa kwa kifaa hicho katika shughuli za jando inamaanisha kuwa mtahiriwa ametoshea na amepewa idhini ya kutumia uume wake kushiriki tendo la ndoa punde tu, atakapotoka jandoni. Hivyo basi, mafunzo hayo yametumika kiurejelezi katika kufanikisha diskosi ya idhini ya kushiriki tendo la ngono miongoni mwa wavulana kwani kifaa hiki na uume vimelinganishwa kwa njia ya kiujarabati ili kuafiki malengo ya matumizi yake.

#### **4.2.2 Kiwango cha Kushiriki Tendo la Ndoa**

Katika jamii hii, ni mwiko kushiriki tendo kama bado hujatahiriwa. Mafunzo yanayotolewa jandoni yanalenga kufahamisha wavulana na watu ambao wanafaa kushiriki tendo la ndoa nao, hivyo basi, kauli ya Ng2Kv3Md2 ambayo imenukuliwa hapo juu inaashiria haya;

Sherehe hizi ni za kipekee huwa za mwisho kwa mvulana kumkaribia dadake na mamake kwa njia hiyo. Kwa kuzingatia mhimili wa ufifishaji ambao husaidia katika kupunguza na kuvumisha hadhi kwa kufifisha au kuongeza makali nguvu ya usemi ilokusheni. Matini hii inabainisha wahusika ambao wanafaa kushiriki ngono katika jamii hii. Mchakato huu unadhamiria kuonyesha washiriki wa kushiriki tendo la ndoa. Kwa kawaida tendo la ndoa huwa ni shughuli ya siri, lakini sherehe hizi hufanyika kwa uwazi, hii ina maana kuwa wahusika wa shughuli ni wa kufanyia ujarabati tu. Hivyo basi, mtahiriwa hafai kushiriki tendo la ndoa na mamake au dadake. Aidha, mamake anawakilisha kina mama wengine wa umri sawa.

## **Ng3Kv5Md2: Kailet**

*Inoni ko tumdo nekiyae en gaa kotomo kwoo ng'etet en gaa kotokyigee menjo. Kiyaen mabwaitab gaa nebo ng'etet, ago kiipu kuinetab teta nemiten orit mwaitab asi koileen chepkam togoch nebo ng'etatab kam newendi tum. En kailanitet konyolu koboisien eut ab taa, koileen togoch teget ak kubesto nebo kataam konyil ang'wan. Yekatotar kailet komwachi kolenji "kakityakteen iwee" akowol ng'etet kole "karayan awoo".*

### **Tafsiri**

'Kailet'(kupaka mafuta) ni sherehe ambayo hufanywa kabla ya mvulana kukabiliana na kisu cha ngariba, hii ilifanywa tu baada ya kuondoka kwao. Shughuli hufanywa mahali mwafaka ambapo hujulikana kama 'mabwaita' (sehemu ambayo imetakaswa) mafuta ya kujipaka huwekwa kwenye pembe ya ng'ombe na dadake mvulana huchaguliwa kumpaka mafuta hayo huku wanajamii wote wakimtazama. Katika mchakato huu ni sharti dadake atumie mkono wake wa kulia na kumpaka nduguye. Humpaka; kwenye utosi, kifua na paja la kushoto, kila upako hufanywa mara nne huku akizunguka sehemu hiyo mwafaka mara nne. Baada ya mchakato huo dadake atamwambia 'tumekuachilia utoke' naye mvulana atajibu 'nimekubali kutoka'.. Sherehe hizo zilikuwa za mwisho kabla ya mvulana kuondoka kwao kuelekea jandoni. Hii pia ilikuwa njia ya kumtakia mvulana mema akielekea safari ya jando na vilevile kila la heri katika shughuli zote za jando. Aidha, atakaporudi nyumbani atakuwa na ufahamu wa mila na desturi za jamii hio.

Sherehe hizo ni za kipekee kwa sababu zitakuwa mara ya mwisho kumkaribia dadake au msichana yeyote wa ukoo wao. Kuwepo kwa dada kunadhihirisha kwamba wavulana hawapaswi kushiriki tendo la ngono na dada zao. Huu ni mwiko katika jamii hii. Hivyo basi, ikiwa alikuwa ameshiriki tendo la ndoa na dadake au msichana wa ukoo wao, basi sherehe hii ilikuwa ni njia ya kuomba msamaha na kumtakasa. Maneno aliyonena kuwa nimekubali kutoka ni ishara tosha kuwa hatafanya hivyo tena au kumruhusu dadake kugusa paja lake kama vile amefanyiwa katika sherehe hii. Sherehe hii huwa ni muhimu katika jamii ya Wakalenjin kwa kuwa inaweka mipaka au Washiriki wanaofaa kushiriki tendo la ngono nao. Kwa upande mwingine, uwepo wa

wahusika wa familia ni kutoa ushahidi kuwa mvulana amefuzu mchakato huo na iwapo atatenda kinyume na makubaliano hayo, basi laana ya familia itampata.

### **4.2.3 Jinsi ya Kushiriki Tendo la Ndoa**

Mafunzo mengine yanayotolewa katika muktadha wa jandoni ni namna ya kushiriki tendo la ndoa. Mafunzo haya hutolewa na ngariba kwa wavulana walio jandoni. Husheheni namna ya kutongoza msichana na jinsi ya kuanzisha mchakato wa kushiriki ngono. Ng2Kv3 ambaye kauli yake imenukuliwa hapo juu katika kueleza sherehe ya Yatetab oret (kufungua njia) inadhihirisha mafunzo haya;

Matini hii inalenga kutoa mafunzo jinsi ya kushiriki tendo la ndoa. Ua lililotengezwa na kuhakikisha mtahiriwa anapita limetumiwa kama urejelezi wa sehemu nyeti ya jinsia ya kike. Kutembelea ndani la lile ua linatoa hamasisho kuwa mwanamume anafaa kuuweka uume wake ndani ya uke wa mwanamke. Anaposema kwamba ua hilo huwa ni ndogo na mtahiriwa huinama wakati wa kulipita ndani huu ni uhalisia kushiriki tendo la ndoa. Kwa kuwa sehemu nyeti ya jinsia ya kike imeumbwa mahali ambapo sio rahisi kufikia na huhusisha kunyoosha mwili ipasavyo ili kuendeleza tendo la ngono. Hali hizi ngumu anazopitia mvulana ni za kutia makali kwamba, kuna mitindo ya kuzingatia katika kushiriki ngono.

Anaposema kuna mchakato wa matumizi ya samadi ya ng'ombe na matumizi ya mguu yanahimizwa; hii ni njia ya kipekee ambapo mama anamwonyesha mtahiriwa sehemu ya kushiriki tendo la ndoa. Kutumika kwa mguu kama ala ya kupitisha samadi ya ng'ombe kinatiliwa maanani sana. Samadi katika jamii hii hutumiwa kujenga nyumba na pia kama mbolea ya mimea. Hivyo basi, mguu ni urejelezi wa uume na jinsi ya kupitisha mambo muhimu, ambapo katika diskosi hii ni kupitisha uhai wa jamii. Kama vile samadi husaidia kurutubisha mimea na hivyo kuwepo kwa mazao mengi. Kwa kawaida ushiriki wa tendo la ndoa husababisha kuendelezwa kwa kizazi. Hata hivyo, mtahiriwa anapata funzo kuwa samadi imeelekezwa kwa sehemu nyeti, hivyo basi anapaswa kuelekeza uume wake ndani ya sehemu nyeti ya mwanamke ili aweze kujenga jamii na kukiendeleza kizazi.

**Mawazo ya Ng2Kv4Md2** kama alivyonukuliwa hapo juu katika uundaji wa *kweisit*. Taswira ya kifaa hicho ni urejelezi wa uume, kichwa chake ambacho ni pana kushinda mwili na kina umbo sawa na uume. Aidha mwili wake mwembemba ni sawa pia na uume. Isitoshe, sehemu ya mwisho ni mkia wenye manyoya. Manyoya hayo ni sawa na sehemu ya mwisho ya uume ambapo kuna nywele. Utumiaji wa kifaa hicho katika muktadha wa jando ni ishara ya mafunzo ya namna ya kushiriki tendo la ndoa. Kwa sababu katika windo kichwa cha kifaa hicho hutangulia, kisha mwili wake. Vilevile, katika ngono kichwa cha uume pia hutangulia na huongoza shughuli hiyo, kisha mwili hufuata. Aidha, kichwa cha kifaa hicho ndicho nguzo muhimu katika windo na hufanikisha shughuli za windo. Kwa upande mwingine, kichwa cha dhakari ni nguzo katika kufanikisha ushiriki wa tendo la ndoa.

Matumizi ya kifaa hicho huwa sawa na jinsi ya kushiriki ngono. Hivyo basi, mafunzo yanayopitishwa kwa kulenga shabaha ni sawa na jinsi ya kushiriki ngono na kutia mwanamke mimba. Ndege katika muktadha huu ametumika kama uke na kifaa hiki kinaashiria uume. Isitoshe, kifaa hiki kinafaa kulenga shabaha sawa sawa. Hivyo basi, mvulana anapaswa kulenga uke katika ushiriki wa tendo la ndoa sawia na kulenga shabaha ndege katika muktadha wa jandoni.

### **Ng3Kv6Md2: *Kayaet ab taruusyek***

*Tumii keyae en oinet anan ko silanga. Kitechee munandet netinye kurget en beek orit keboisen isyeek, munandet notet kegureen musangit. Tumii koki oretab mwetetabgee netai en menjo kong'eten ingobaa menjo. Nyolu kotwolchi beek ak kochut orit kobuun kurget ab musangit ako mong'unen komosto nebo aeng' ako yekakomong' ketyenchin ak kikochi kainetab kekureen arap koboora kole kakoik murenik.*

### **Tafsiri**

Ni sherehe ya kutakasa watahiriwa, ambapo hufanywa katika mto au bwawa la maji. Sherehe hii hujulikana kama 'kayaet ab taruusyek'. Ngariba hutengeneza ua lililo na umbo la lango ndani ya maji. Ua hilo hutengenezwa kwa vijiti na majani ya mmea fulani ambao ukiguza mwili unawasha na kusababisha uchungu, tazama picha P4Md3. Sherehe hii ilikuwa ya muhimu kwa sababu ni mara ya kwanza kuoga miili tangu

waingie jandoni. Kila mtahiriwa alipaswa kuruka ndani ya maji kwa kuogelea na kuhakikisha ameingia katika lile ua lililo ndani ya maji kwa kutokea sehemu ya pili. Mtahiriwa anapofaulu kupita lile ua basi hupewa jina la heshima ili aweze kuongeza katika jina lake, jina hilo ni araap. Jina hili ni la heshima kumaanisha amekuwa mwanamume na shujaa katika jamii. Sherehe hio huhusisha nyimbo mbalimbali za kitamaduni za kusifu wanaumme huimbwa papo hapo. Sherehe hii ni ya kipekee kwa sababu nyimbo hizo hazitaimbwa tena kwingine hadi sherehe nyingi kama hiyo ifanyike.



### ***P4Md3***

Maana ya ua ndani ya maji ni urejelezi wa jinsi ya kushiriki tendo la ndoa. Ua lililotengenezwa ndani ya maji linalinganishwa na uke. Mvulana au mwanamume anapaswa kuingiza uume wao ndani. Maji kutumika hapa ni kwa lengo la kuleta taswira ya sehemu nyeti ya mwanamke. Isitoshe, majani mabichi yanayowasha yanatoa funzo ya kujitahidi na kustahimili matatizo ya kushiriki kwa tendo la ndoa. Kwa kawaida mvulana hutarajia kumwoa msichana bikira, hivyo basi, ugumu na uchungu wa mchakato huu unalinganishwa na ule wa kuvunja ubikira wa mwanamke.

Diskosi hii inatoa funzo la mwanamume kufahamu jinsi ya kushiriki tendo la ndoa wakati wa ndoa. Kupewa jina la heshima ni kumhamasisha aweze kujihusisha na tendo

la ndoa kwa lengo la kuendeleza kizazi. Isitoshe, hata yeye asubiri atakapojaliwa na mvulana pia, ampe jina hilo la heshima.

#### **4.2.4 Unyeti na Maadili ya Tendo la Ndoa**

Maadili katika masuala ya tendo la ngono ni mambo muhimu katika jamii hii na yanapaswa kuzingatiwa kwa undani. Katika muktadha wa jandoni mafunzo ya maadili katika tendo la ngono hupitishwa na wazee kwa vijana wanaopashwa tohara. Mafunzo haya hutolewa kupitia sherehe za jandoni kwa mfano Ng2Kv3Md4 kama alivyonukuliwa hapo juu katika sherehe ya Yate tab oret (kufungua njia).

Diskosi hii inalenga kumfunza mtahiriwa kuhusu unyeti wa jinsia ya kike ili aweze kuzoea au kupata maarifa zaidi. Kwa mujibu wa mkakati wa ubishi ambao hutumia ishara chanya au hasi kuhusu mhusika au kundi fulani, ni wazi kwamba kauli hii inalenga topoi ili kutoa usemi wa kupendelea au kubagua ili kuhalalisha jambo. Kwa msingi huu, sherehe hii ambayo inahusisha mama mzazi na dadake, humtayarisha mtahiriwa kuheshima unyeti wa wahusika hao. Hii ni kwa sababu ni mara yake ya mwisho kumkaribia mamake kwa njia hiyo. Kwa hivyo wanajaribu kuhalalisha maadili ambayo yanafaa kuzingatiwa katika tendo la ngono. Sherehe hii pia humpa mtahiriwa hadhi sawa na babake katika elimu ya unyeti ndiposa babake anashiriki pia. Hivyo basi, amepata uwezo na uhalali wa kuzungumza na babake kuhusu masuala ya tendo la ndoa iwapo atapata changamoto wakati wa ndoa.

*Dadake mvulana huchaguliwa kumpaka mafuta hayo huku wanajamii wote wakimtaazama. Katika mchakato huo ni sharti dadake atumie mkono wake wa kulia kumpaka nduguye. Atampaka; kwenye utosi, kifua na paja la kushoto, kila upako hufanywa mara nne huku akizunguka sehemu hio mwafaka mara nne. Baada ya mchakato huo dadake atamwambia 'tumekuachilia utoke' naye mvulana atajibu 'nimekubali kutoka'.*

*Sherehe hiyo huwa ya mwisho kabla ya mvulana kuondoka kwao kuelekea jandoni. Hii pia huwa njia ya kumtakia mvulana mema akielekea safari ya jando na vilevile kila la heri katika shughuli zote za jando. Aidha, atakaporudi nyumbani atakuwa na ufahamu wa mila na desturi za jamii hio.*

*Sherehe hizo ni za kipekee kwa sababu huwa za mwisho kumkaribia dadake au msichana yeyote wa ukoo wake. Ikiwa alikuwa ameshiriki tendo la ndoa na dadake au msichana wa ukoo wao, basi sherehe hii huwa ni njia ya kuomba msamaha na maneno alionena kuwa nimekubali kutoka ni ishara tosha kuwa hatafanya hivyo tena au kuruhusu dadake kugusa paja lake kama vile amefanyiwa katika sherehe hii.*

Sherehe hii huwa ni muhimu katika jamii ya Wakalenjin kwa kuwa inaweka mipaka na maadili ya kushiriki tendo la ndoa. Huu ni mkakati wa ubishi ambao unatumia ishara chanya kutoa usemi wa kupendelea au kubagua ili kuhalalisha suala la maadili katika tendo la ndoa. Kwa upande mwingine, uwepo wa wahusika wa familia ni kutoa ushahidi kuwa mvulana amefuzu mchakato huo na iwapo atatenda kinyume na makubaliano hayo ya kimaadili, basi laana ya familia itampata. Kwa hivyo, diskosi hii ina umuhimu katika kuweka maadili mema kwenye tendo la ndoa. Hivi kwamba mtahiriwa anapata ufahamu wa kutosha kuhusu madhara ya utovu wa nidhamu katika masuala ya tendo la ndoa. Maadili hayo yatamwongoza maishani na anatarajiwa kutii sheria hizo.

#### **Mt1Kv7Md4: Chemenjo**

*Chemenjo ko chepyoset ne kimutii kwoo menjo kotomo kosopcho ng'etik komie. Kikiboisien kimueen tarusyek kayai kesesnotet ak chemenjo. Tarusyot nekoibor makeet ab koyai kesesnotet kokinyoru kergong'et. Inoni koko oret nekiboorchin kelee monyolu koyai kesesnatet ak chepyoset neo.*

#### **Tafsiri**

Watahiriwa wanapokuwa jandoni baada ya kukabiliana na kisu cha ngariba na kuelekea kupona, ajuza huandamana na ngariba hadi jandoni. Mama huyu hupewa jina la kimajazi Chemenjo. Watahiriwa hutishiwa kushiriki ngono na mama huyo mkongwe licha ya wao kutopona kwa uume wao. Mchakato huo ni funzo kuwa watakapotoka jandoni hawafai kushiriki tendo la ndoa na mwanamke anayewazidi umri. Aidha, katika mchakato wa jandoni mambo huwekwa wazi kwamba sehemu nyeti zao huonekana na ni sharti ngariba aweze kukagua kila mara.

Diskosi hii ya ajaza kuwatembelea na kutoa kauli hii ni dhihirisho ya mkakati wa ubishi. Hii ni kwa sababu ajaza anatumiwa kama topoi ya kuhalalisha maadili ambayo vijana wanafaa kuzingatia kuhusiana na tendo la ngono. Hii ilikuwa njia ya kuwajaribu na kutambua mtahiriwa ambaye ataweza kupata ashiki za ngono au misuli ya uume kulisimuka. Iwapo kutatokea mmoja ambaye atasisimuka kingono, basi hupewa adhabu ya kutosha na ngariba. Hii ni mbinu ya kuhakikisha mtahiriwa anafuata maadili ya kutopata ashiki za ngono na ajaza.

Maoni ya Mt2Kv8 Md4 kuhusu nyimbo anaeleza kwamba nyimbo hizihuimbwa na watahiriwa wanapokuwa jandoni. Ngariba huwafunza nyimbo hizo na jinsi ya kuimba. Baadhi ya nyimbo hizo ni za kuburudisha na zingine kukuza talanta kwa wale ambao watapenda kuimba. Lakini nyimbo zingine hutoa mafunzo kuhusu kushiriki kwa tendo la ndoa.

#### **W1Md4**

*Chepokumiin tiony ooh eeh*

*Kumiin tiony sigiriet*

*Chepune ainab tich*

#### **Tafsiri**

Wa kutenda ngono kwa uuke ooh eeh

Tenda kwa ukakamavu kama punda

Ingiza kwa uuke

Katika matini ya W1Md4, mtahiriwa anafunzwa kuhusu tendo la ndoa, na anapewa mfano wa mnyama punda. Kwa kuzingatia mhimili wa ufifishaji ambao husaidia katika kupunguza na kuvumisha hadhi ya kihisishi kwa kufifisha au kuongeza makali nguvu ya usemi ilokusheni. Utafiti huu umebainisha jinsi wahusika, kundi au vyombo teule vilitumika katika usemi wa kuweka uzito katika nyimbo hizi. Hii ndio sababu wanamtumia mnyama punda ambaye huwa na sifa za ukakamavu katika ngono. Hivyo basi, watakapotoka jandoni wanapaswa kuwa wakakamavu na wenye bidii sawia na punda katika tendo hilo. Aidha, katika mshororo wa tatu, neno uke limetajwa hii ni

muhimu zaidi katika kuisitiza maadili katika ngono. Hii ni kwa sababu anapaswa kuingiza uume wake kwenye uke wa mwanamke pekee sio kwa mnyama yeyote.

Diskosi hii pia hutoa funzo la kuwa na nidhamu kama punda. Mnyama huyo hutambulika kwa sifa ya nidhamu ya kutoshiriki ngono kila wakati. Ni mnyama ambaye ana uwezo wa kustahimili miaka mingi bila kushiriki ngono. Kwa mjibu wa mkakati wa ufifishaji ambao unasisitiza na kutilia uzito suala fulani. Watahiriwa wanafunzwa maadili ya kuwa wastahimilivu kuhusu kushiriki ngono na wavumilie hadi watakapofunga ndoa. Aidha, mnyama huyo ana sifa ya uvumilivu hadi mwenzio wa kushiriki ngono atakapopatikana, hata ikichukuwa muda mnyama huyo huwa na subira. W1Md4 huwa na umuhimu sana katika maisha ya mvulana na anastahili kutumia hilo kama funzo wakati wowote. Isitoshe, wimbo huu unadhamiria kusuta uvivu katika tendo la ndoa hasa kwa wanaume.

#### **W2Md4**

*Kisole chii kwony*

*Chii kwony konon buus*

*Chepokerta oor*

*Kerta oor masielel*

#### **Tafsiri**

Mwanamke hubembelezwa

Mwanamke nipee uke

Uuke na uume kuingiana ipasavyo

Kuingiana ipasavyo hadi kilele

Katika W2Md4, mtahiriwa anapewa funzo la kunyenyekea mbele ya mwanamke katika mchakato wa matayarisho ya kushiriki tendo la ndoa. Mkakati unaotumiwa hapa ni wa ufifishaji ambapo dhana ya kunyenyekea na kuzingatia maadili katika masuala ya ngono inatiliwa mkazo. Hii ilikuwa njia ya kuwasuta wale wanaobaka wanawake na kuwafanya wajue kuwa mwanamke akibembelezwa atakubali. Aidha, sehemu hizo nyeti zimetajwa kwa neno *kuingiana* ni ishara ya watu wenye umri unaokaribiana au

rika moja. Wimbo huu unaeleza kwa maana ya ndani kwamba uke na dhakari zinapaswa kuingiana au kutoshana kwa nguvu na umri. Hivyo basi, kutoshana kwa sehemu hizo italeti raha na msisimuko katika kilele. Wimbo unalenga kutoa funzo kwa wavulana kutoshiriki tendo la ndoa na wasichana wadogo ambao hawajabaleghe. Mathalan, kwa msichana mdogo sehemu hizo hazitaingiana ipasavyo na anaweza kuumia na hatafika kilele kama inavyostabili.

### **4.3 Mikakati Inayotumiwa katika Mafunzo**

Sehemu hii inashughulikia lengo la pili la utafiti huu ambalo ni kuhakiki mikakati ya usemi inayotumika kudhihirisha mada za lugha ya tendo la ndoa jandoni katika jamii ya Wakipsigis. Kuchunguza mikakati ya usemi ni muhimu kwa kuwa ina uhusiano mkubwa na maudhui (Wamitila, 2016). Mikakati ya usemi humwezesha mzungumzaji kuwasilisha maudhui. Kinachowasilishwa kama kauli ya usemi kinaweza kuhakikiwa kwa kuchunguza mikakati yake ya usemi. Leech (1969) anafafanua mikakati ya usemi kama njia au jinsi lugha inavyotumiwa katika matini. Anaendelea kuelezea kuwa matini yoyote ile huathiriwa kwa kiasi kikubwa na mikakati ya usemi ambayo imetumika kwa sababu katika kila muktadha msemaji huchagua jinsi ya kuzungumza. Kwa muktadha wa utafiti huu, mikakati ya usemi ni jumla ya tamathali za semi ambazo ngariba ametumia kuwasilisha mada kuhusu tendo la ndoa. Aidha, maudhui yanaweza kuhakikiwa kwa mazingatio ya uwazi na usimbaji wa mikakati ya usemi ili kubaini viwango mada za tendo la ndoa.

Nkumbo (2019) anaeleza kuwa mikakati ya usemi hujaribu kujibu swali la ni vipi? Hivyo basi, ubunifu wa ngariba na uwezo wake wa kuteua mikakati ya usemi mwafaka ndivyo vifaa vinavyomwezesha kuwasilisha mada yake. Chepkorir (2016) anahoji kuwa mikakati ya usemi hufanya miviga iwe ya kuvutia na yenye mnato pamoja na kusisitiza ujumbe unaowasilishwa. Mintaarafu ya hayo, mtafiti alibaini kuwa ngariba wametumia mikakati ya usemi kuwasilisha mada kuhusu tendo la ndoa.

Katika utafiti huu mikakati mbalimbali ilijitokeza. Hata hivyo mtafiti alijikita tu katika mikakati ambayo inaambatana na madhumuni ya utafitihuu. Katika kuafiki madhumuni ya utafiti, uchanganuzi wa mikakati ulifanywa kwa kuzingatia mihimili ya urejelezi, uarifishaji na mkabala, mtafiti alibaini mikakati ifuatayo;

### **4.3.1 Jazanda**

Kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2011), jazanda ni picha inayomwingia mtu kichwani. Aidha, kamusi kuu ya Kiswahili (2015) inafafanua jazanda kama picha ya kitu inayojengeka akilini mwa mtu. Isitoshe, Wamitila (2003) anasema jazanda ni dhana ambayo hurejelea matumizi ya taswira au picha kwa ukamilifu wake.

Job (2022) alieleza jazanda kama kunga za utunzi ambazo zinatumia lugha kuchora picha fulani yanayotokana na maelezo yaliyotumia maneno teule pamoja na tamathali za usemi. Kwa msingi huu mtunzi humwezesha msomaji kuona au kuhisi kitu ambacho kinatolewa maelezo.

Honara (2010) anafafanua kuwa jazanda ni za aina tatu; kiubia, jamii na za kibinafsi. Jazanda za kiubia ni zile zinazotumia dunia nzima kama vile tamaduni. Jazanda za jamii ni zile zinafungamana na jamii husika na jazanda za kibinafsi ni zile mtu anaweza kuzitafsiri pekee yake. Okwena (2013) ameinisha jazanda kulingana na wanyama, miti, ndege, mimea, wanyama na kadhalika.

Utafiti huu uliweza kubaini jazanda katika mafunzo ya jando katika jamii ya wakipsigis ambazo zimetumika kama taashira ya kuwasilisha funzo fulani., mtafiti ameeleza kwa uangavu na kwa kina maana iliyokusudiwa na ngariba. Aidha, jazanda zinarejelea uhalisia wa maisha na watahiriwa wanapaswa kufanyia ujarabati baada ya kufuzu jandoni kwa mfano.

#### **Kiamb.1**

*Yekaketar keyatitoo nge'etet ako kamuita, kosimee chepyosok konyil ang'wan,  
akomwa kaamet anan ko chepyoso kole, "kokayam kwam sorom nemi buut kut".  
Kowool murenik en kipangenge kole "eeh kakoyam".*

#### **Tafsiri**

Wakati mvulana ametahiriwa bila kulia au kulalamika au kutingiza kichwa, basi kina mama wanashangilia kwa nderemo mara nne. Baada ya nderemo, mamake mzazi au ajuzi atainua mikono na kusema 'mvulana huyu ametoshea kula mnyama ambaye ana manyoya mdomoni, huku wanaume wataitika kwa kauli moja 'ametoshea.'

Maana ya ndani ya mkakati huu unadhamiria kurejelea sehemu nyeti ya mwanamke. Kwa msingi wa mhimili wa mkakati wa mkabala ambao hutambuliwa kwa unukuzi, utoaji wa taarifa, matumizi ya maelezo na masimulizi. Ajuza anadhihirisha haya kwa matumizi ya masimulizi ya kijazanda, urudiaji na ishara, neno ambalo limerudiwa ni *kakoyam* (ametoshea) na jazanda inayojitokeza ni matumizi ya mnyama mwenye manyoya, kwa hivyo, anakwepa kutamka neno uke moja kwa moja. Mkakati huu hulenga kutoa mwelekeo kwa mhusika mnenewa. Katika matamshi mwelekeo anaopewa mtahiriwa ni kwamba anatosha kushiriki ngono. Kwa kawaida sehemu nyeti ya mwanamke ambaye amekomaa huwa ni sehemu iliyo chini ya tumbo na juu ya kinembe. Sehemu hiyo huwa na mavuzi na hivyo basi taswira hiyo inalinganishwa na usemi wa maneno hayo, kuwa mnyama mwenye manyoya mdomoni. Utafiti huu uligundua kwamba mnyama anayerejelewa katika kifungu ni uke wa mwanamke. Hivyo basi, jamii hii imefasiri uke kwa kutumia jazanda ya mnyama. Kwa sababu sifa za kimaumbile hasa uwepo wa manyoya mdomoni umelinganishwa na kusawazishwa na maelezo ya mafunzo ya jandoni. Jazanda hii imetumika ili kuficha siri za masuala ya ngono kwa wale ambao hawajapashwa tohara.

## **Kiamb.2**

*Nyolu kocheng'e tarusyot age tugul chemeriat anan ko chepto ne aechindos asi kobokokyi kirokto nekoikochin motiryot. Yekakonyoor chemeriat anan ko chepto konyolu kotinyeen kirokotet kubesto, suet ak batet yeityo komwa kole "karokoite tugukab lakwandit ako achopot atoi sobet age" kowalu agine chemeriat kule "Karataach" ak konam kirokto, kou yekakineet agine en menjo nenywan chemosyan, ak kwa oinet kowirchi beek kirokotet asi kolaa beek.*

## **Tafsiri**

Baada ya watahiriwa kuosha miili yao. Kila mtahiriwa anaruhusiwa kutafuta msichana ambaye ako katika unyagoni au yeyote aliyebaleghe; mwenye umri sawa. Mtahiriwa hupewa kijiti maalum na ngariba na anapaswa kugusa paja, kiuno au mgongo wa msichana kwa kuvuta kile kijiti na sehemu hiyo ya mwili. Mvulana anapaswa kusema 'nimepeana kila kitu cha utoto wangu na niko tayari kuingia sehemu ya mwisho ya maisha'. Iwapo msichana ako katika unyagoni anapaswa kuitika kwa kusema nimeipokea; huku akikabidhiwa kile kijiti. Baada

ya msichana kukishika, anatarajiwa kuenda mtoni na kukitupa kile kijiti kisombwe na maji.

Mkakati huu ni wa kijazanda kwa sababu maana yake ya kina inaweza kufafanuliwa kutokana na mchakato huo. Huu ni mkakati wa ubishi ambao umejikita katika topoi ambapo usemi wa kupendelea au kubagua hutumika ili kuhalalisha jambo. Maana ya kushiriki tendo la ndoa inasisitizwa zaidi, hivyo basi kuhalalisha suala la ngono kwa wavulana waliopashwa tohara. Mvulana kupeana kijiti kwa msichana na kuitika kwa msichana na kukipokea kijiti ina maana ya kina. Kijiti hiki ni jazanda ya dhakari ya mtahiriwa mvulana ambayo imeelekezwa kwa mwili wa msichana. Kijiti hicho kinaashiria kwamba mvulana anatarajiwa kushiriki tendo la ndoa na msichana wa rika sawa. Aidha, mvulana kupeana kijiti kwa msichana kunamaanisha kuwa jinsia ya kike katika jamii hii ndio huanzisha mchakato wa tendo la ndoa. Msichana kwa upande wake huwa na jukumu la kukubali au kukataa posa au ombi la kushiriki tendo la ndoa. Isitoshe, upande wa wasichana ni jazanda ya kukubali kila ncha ya mwanamume kuingizwa kwa uke wake wakati wa tendo la ndoa.

### **Kiamb. 3**

*Kitechee kiit neu munandet netinye kurget ak kinde kiptangasiat anan ko menet ak ketesyi suswek barak. En tumii kekanye tarusyot konyo akoi mundanet elee miten chepkamet. Nyolu koboisyen tarusyek keldo kotyech ngatatiet akoileen kubestab chepkam konyil somok. Yekakotar kokochi kwanda kirokto ak panget asi kotil kirokotet, oloon testetai kotile kotebee motiryet kole “ngete nana mongete” ak kowool kwanda agine kole “ngetee” yeityo koketyi kotyech nyatatek ak koilen kameet kora kou ye kayai en chepkamet.*

### **Tafsiri**

Ua lilitengenezwa likiwa na lango ambapo mtahiriwa atapita kisha chini yake samadi ya ngombe au udongo uliofinyangwa huwekwa juu ya nyasi. Katika sherehe hii, msichana ambaye ni ndugu yake mtahiriwa atatumia mguu wake kumpaka mvulana mtahiriwa ile samadi au udongo mara tatu katika paja lake. Mama mzazi atamsubiri pale na mtahiriwa akiwasili atapewa kijiti na babake mzazi na kukikata kwa upanga. Baada ya kukikata, ataukanyaga udongo ulio chini kwa kutumia mguu na kuuwekelea kwenye paja la mamake na mamake

pia atafanya hivyo. Hayo yakiendelea ngariba atauliza baba mzazi wa mtahiriwa 'itakatika ama haitakatika?' huku baba mzazi akijibu; 'itakatika'.

Miviga hii, inafafanua masuala mengi ya maisha kijazanda na mvulana anatarajiwa kuyatii hayo maishani. Katika mchakato huu, ua lililotengenezwa limetumiwa kijazanda kumaanisha kuhitimu kwa kiwango fulani katika jamii hiyo. Kwa mujibu wa uchanganuzi usemi wa diskosi kama mkabala wa historia mkakati wa ufifishaji umetumika kuongeza makali yaani kutilia mkazo. Miviga hii inalenga kutoa mafunzo kuhusu jinsi ya kushiriki tendo la ndoa. Ua ambalo hutengezwa na kuhakikisha mtahiriwa anapita linalinganishwa na sehemu nyeti ya jinsia ya kike kijazanda. Kutembea ndani ya lile ua kunatoa hamasisho kuwa mwanamume anafaa kuiweka dhakari yake kwenye uke wa mwanamke. Mara nyingi ua hilo huwa ni ndogo na mtahiriwa huiinama wakati wa kuipiti ndani. Huu ni uhalisia wa kushiriki tendo la ndoa kwa kuwa sehemu nyeti imeumbwa mahali ambapo sio rahisi kufikia na huhusisha kunyoosha mwili ipasavyo.

Mchakato wa samadi ya ng'ombe na kutumia mguu unahimizwa. Hii ni jazanda ya kipekee ambapo mama anamwonyesha mtahiriwa sehemu ya kushiriki tendo la ndoa. Huu ni mkakati wa ufifishaji ambapo umejikita kwa kuvumisha ufahamu na ukubalifu wa tendo la ngono miongoni mwa wavulana waliotahiriwa. Kutumika kwa mguu kama ala ya kupitisha samadi ya ng'ombe inatiliwa maanani sana. Samadi katika jamii hii hutumiwa kujenga nyumba na pia kama mbolea ya mimea. Hivyo basi, mguu ni jazanda ya dhakari. Dhakari ni kiungo muhimu sana cha kuendeleza jamii katika diskosi hii ni kupitisha uhai wa jamii. Kwa kawaida ushiriki wa tendo la ndoa husababisha kuendelezwa kwa kizazi. Hata hivyo, mtahiriwa anapata funzo kuwa samadi imeelekezwa kwa sehemu nyeti, hivyo basi anapaswa kuelekeza uume wake kwenye sehemu nyeti ya mwanamke ili aweze kujenga jamii na kuendeleza kizazi. Samadi au udongo ambao umeelekezwa kwa paja huku mguu ukitumika kama ala inajaribu kueleza uhalisia wa kushiriki tendo la ndoa. Udongo au samadi kuwekwa kwenye ua, ni jazanda ya kuamsha ashiki za ngono, kwa kawaida ashiki au ari ya ngono huamshwa na mguso wa sehemu nyeti.

#### **Kiamb. 4.**

*Tumii keyae asikobit kwoo ng'etet en gaa koriin. Nyolu komiten kuinetab teta nemiten orit mwaita asi koileen chepkam togoch nebo ng'etetab kam newendi*

*tum. En kailanitet konyolu koboisien eut ab taa, koileen togoch teget ak kubesto nebo kataam konyil ang 'wan. Yekatotar kaileet komwachi kolenji "kakityakteen iwee" akowol ng'etet kole "karayan awoo".*

### **Tafsiri**

Katika sherehe hii, mafuta ya kujipaka huwekwa kwenye pembe la ng'ombe na dadake mvulana huchaguliwa kumpaka mafuta hayo huku wanajamii wote wakimtazama. Katika mchakato huu, ni sharti dadake atumie mkono wake wa kulia na kumpaka nduguye. Atampaka; kwenye utosi, kifua na paja la kushoto, kila upako hufanywa mara nne huku akizunguka sehemu hio teule mara nne. Baada ya mchakato huo dadake atamwambia 'tumekuachilia utoke' naye mvulana atajibu 'nimekubali kutoka'.

Sherehe hii imetumia mkakati wa kijazanda ili kufanisha lengo lake la kuwasilisha maana katika jamii ya Wakipsigis. Mhimili wa uarifishaji umezingatiwa katika kuchanganua kauli hii kwani mhimili huu hueleza tabia kwa njia hasi na chanya kwa kutumia maelezo ya lugha kwa uwazi. Mkakati huu hulenga kumtambulisha mhusika kwa njia ambayo inaweza kupunguza au kuzidisha namna wanavyosawiriwa. Mhusika anatambuliwa kwa kupakwa mafuta katika sehemu tofauti mara nne, kwa hivyo anasawiriwa kijazanda kama aliyefuzu kushiriki ngono na kutengana na mamake na dadake. Heshima na maadili ndio nguzo muhimu zinazodhamiriwa katika shughuli nzima ya jandoni. Katika mchakato huo, hiyo ilikuwa mara ya mwisho kumkaribia dadake au msichana yeyote wa ukoo wao. Iwapo alikuwa ameshiriki tendo la ndoa na dadake au msichana wa ukoo wao, basi sherehe hii ilikuwa ni njia ya kuomba msamaha na kumtakasa. Vilevile kutumika kwa pembe za ng'ombe ni jazanda ya kutorudia kosa hilo, hii ni kwa sababu pembe zikikatwa kwa kichwa cha ng'ombe kamwe hazitarudishwa au kuwekwa tena. Hivyo basi, mtahiriwa anatarijiwa kutomkaribia dadake kingono tena.

### **Kiamb. 5.**

*Tumii koki oretab mwetetabgee netai en menjo kong'eten ingobaa menjo. Kitechee kiit neu munandet netinye kurget en beek orit keboisen isyeek, munandet notet kegureen musangit. Nyolu kotwolchi beek ak kochut orit kobuun*

*kurget ab musangit ako mong'unen komosto nebo aeng' ako yekakomong'  
ketyenchin ak kikochi kainetab kekureen arap koboora kole kakoik murenik.*

### **Tafsiri**

Katika sherehe ya kutakasa watahiriwa, ngariba hutengeneza ua lililo na umbo la lango ndani ya maji. Ua hilo linatengenezwa na vijiti na majani ya mmea fulani ambao ukiguza mwili unawasha na kusababisha uchungu. Kila mtahiriwa alipaswa kuruka ndani ya maji kwa kuogelea na kuhakikisha ameingia katika lile ua lililo ndani ya maji kwa kutokea sehemu ya pili. Mtahiriwa anapofaulu kupita lile ua basi hupewa jina la heshima.

Matayarisho na utaratibu wa kutenda sherehe hii ina maana ya ndani inayoenziwa katika jamii ya Wakipsigis. Kwa msingi wa mhimili wa ufifishaji, kitendo hiki kina vumisha ufahamu na ukubalifu wa kushiriki tendo la ndoa na kuonyesha ukakamavu na ustadi mkubwa. Mkakati huu husaidia katika kupunguza na kuvumisha hadhi kwa kufifisha au kuongeza makali nguvu ya usemi. Maana ya kutengeneza ua majini ni jazanda ya kueleza jinsi ya kushiriki tendo la ndoa. Ua lililotengenezwa ndani ya maji linalinganishwa na uke, ambapo mvulana au mwanamume anapaswa kuingiza dhakari yake ndani. Maji yanayotumika hapa ni kwa lengo la kuleta jazanda ya sehemu nyeti ya mwanamke. Isitoshe, majani mabichi yanayowasha yanatoa funzo kijazanda ya kujitahidi na kustahimili matatizo yanayoambatana na ushiriki wa tendo la ndoa. Kwa kawaida mvulana hutarajia kumwoa msichana bikira, hivyo basi, ugumu na uchungu wa mchakato huu unalinganishwa na ule wa kuvunja ubikira wa mwanamke. Aidha, akienda kando ya ua atagusa majani ambayo yanawasha. Hii ni jazanda ya kupata matatizo iwapo atashiriki ngono nje ya ndoa. Aina za diskosi za kijanda zinazojitokeza katika kauli hii ni kama vile, maji, ua na mimea

#### **4.3.2 Mkakati wa Kitasfida**

Tasfida ni mojawapo wa mkakati wa semantiki wa kimazungumzo ambao hulenga kupunguza makali, kuepuka kuzua hisia hasi na maoni mabaya kuhusu jambo husika. Huu ni mkakati wa ufifishaji. Huwa ni matumzi ya neno au kundi la maneno ambalo linakubalika zaidi katika nafasi ya neno au kundi la maneno ambalo linachukuliwa kuwa la kuudhi katika mazungumzo na hayapendezi kwa msikilizaji (Gomaa na Shi, 2012). Dhima ya tasfida imenawiri sana na hutumika kila siku bila hata kutarajiwa (Linfoot-Ham, 2005; Warren, 1992). Fauka ya hayo, tasfida huhitajika kutokana na

shinikizo za kijamii na kihisia kwa jinsi inayofanikisha mazungumzo kuhusu masuala muhimu kama vile jinsia. Katika sehemu hii, tutarejelea istilahi za kitasfida zinazotumiwa kurejelea sehemu za siri katika mafunzo ya diskosi za tendo la ndoa katika muktadha wa jandoni.

**Jedwali la majina ya kitasfida ya kurejelea sehemu za siri.**

	<b>Muktadha wa jandoni</b>	<b>Tafsiri (Muktadha wa jandoni)</b>	<b>Muktadha wa kawaida</b>	<b>Tafsiri (Muktadha ya kawaida)</b>
1.	<i>Kipkererwet</i>	Bonde linaloraruka	<i>Mokolet</i>	Uuke
2.	<i>Monyiset</i>	Kionja vimiminio	<i>Ndirit</i>	Dhakari
3.	<i>Sotonik ab lakwa</i>	Vibuyu vya mtoto	<i>Kinaik</i>	Matiti
4.	<i>Kimestowet</i>	Mchungaji wa mifugo	<i>Kwetiot</i>	Matako
5.	<i>Nyusit</i>	Malazi nyororo	<i>Buutek</i>	Mavuzi
6.	<i>Tolikenik</i>	Mbegu	<i>Mukuik</i>	Makende

Jedwali 2.

Katika muktadha wa jandoni wavulana wanapofunzwa kuhusu masuala ya tendo la ngono istilahi za tasfida hutumika. Istilahi hizi huundwa kwa kutumia mikakati ya mkabala wa kihistoria mathalan, mkakati wa urejelezi na ufifishaji. Kwa mfano neno linatumiwa wakati wa kurejelea sehemu za siri za jinsia ya kike ni *kipkererwet* (bonde linaloraruka) kwa kurejelea uke kama bonde liloraruka ni kutumia mkakati wa urejelezi kwani sehemu hii inalinganishwa na bonde ambalo lina ufa. Hii ni tasfida ilioundwa kwa msingi wa mandhari ya mkoa wa bonde la ufa ikumbukwe pia wanajamii wa Kipsigis ni miongoni mwa wakaaji wa mkoa wa bonde la ufa. Sehemu za siri za wanaume zinarejelewa na istilahi za kitasfida kama vile *monyiset* (kionja vimiminio) istilahi hii inatumia mkakati wa ufifishaji ambapo dhana fulani inatiliwa mkazo. Mkazo unaotumiwa katika neno hili ni kushiriki ngono ndiposa inarejelewa kama kionja vimiminio, kwa hivyo wavulana wanaopashwa tohara wanalinganishwa na waonjaji wa vimiminio. Vimiminio katika muktadha wa jandoni ni sehemu za siri za kike.

Sehemu nyingine inayorejelewa kwa kutumia mkakati wa ufifishaji ni makende. Yanarejelewa kwa istilahi ya kitasfida kama *tolikenik* (mbegu) kwa kurejelea sehemu hii kama mbegu inatilia mkazo uwezo wa wanaume kuweza kuzalisha. Kwa hivyo, ni mkakati wa kuweka uzito au kupunguza uzito. Kimsingi, kifaa kitumiwacho kurejelea suala fulani huwa ni kibayolojia au kiasili kwa hivyo dhana ya mbegu ni ya

kibayolojia. Mavuzi kurejelewa kama *nyusit* (malazi nyororo) ni mkakati wa urejelezi ambapo mavuzi yanalinganishwa na malazi ambayo ni nyororo. Mkakati wa urejelezihutoa taswira ya kifaa au dhana ambayo huwakilisha dhana fulani katika jamii dhana inayowasilishwa hapa ya kijamii ni sehemu ya kulala.

Sehemu ya matako inarejelewa kitasfida kama *kimestowet* (mchungaji wa mifugo) sehemu hii kurejelewa kama mchungaji wa mifugo inashaaria suala la kimsingi la urejelezi ambapo dhana huwakilishwa kwa kuzingatia dhana ya kibayolojia au kiasili. Neno hili limejikita katika msingi wa kiasili kwani jamii hii ni ya wafugaji na hivyo basi anayefuga malishoni tunatarajia wakati mwingine anaketi. Ndiposa neno mchungaji wa mifugo limetuka, fauka ya hayo mchungaji hufuata mifugo yake nyuma (sehemu ya matako) kwa hivyo urejelezi wa kiasilia unatumika.

Sehemu ya matiti nayo inarejelewa kama *Sotonik ab lakwa* (vibuyu vya mtoto) neno hili ni la kitasfida kwa sababu linaficha ukali wa kutaja neno matiti moja kwa moja. Huu ni mkakati wa ufifishaji kwa sababu mkakati huu huwa ni wa kuvumisha ufahamu na ukubalifu wa vihusishi. Mkakati husaidia katika kupunguza na kuvumisha hadhi kwa kufifisha au kuongeza makali nguvu. Sehemu hii kurejelewa kama vibuyu vya mtoto ina maana kwamba anavumisha hadhi ya matiti kwani matiti ndiyo hutumiwa kunyonyesha mtoto. Hivyo basi, ni ishaara ya kibuyu cha kuhifadhi maziwa, ifahamike kwamba jamii hii ina sifa ya kuhifadhi maziwa ili yagande, maziwa haya huhifadhiwa vibuyuni kwa hivyo mkakati wa urejelezi kiasili umetumika katika kuunda istilahi hii ya kitasfida. Aina ya diskosi katika maneno haya ni ya mifugo, eneo, malazi, mbegu na vifaa vya nyumbani.

Katika kurejelea dhana ya tendo la ngono Kiamb 6 kilitumika.

### **Kiamb. 6**

*Kisiimee chepyosok konyil ang'wan, akomwa kamet anan ko chepyoso kole,  
"kokayam kwam sorom nemi buut kut". Kowool murenik en kipangenge kole  
"eeh kakoyam".*

### ***Tafsiri***

Baada ya nderemo, mamake mzazi au ajuza atainua mikono na kusema tafsiri yake ni kuwa, mvulana huyu ametoshea kula mnyama ambaye ana manyoya mdomoni, huku wanaume wataitika kwa kauli moja tafsiri yake ametoshea.

Mkakati wa uarifishaji umetumika katika kauli hii, mkakati huu huja baada ya unominishaji kwani hueleza suala kwa njia wazi. Baada ya mvulana kuwa jandoni kwa siku kadhaa mama mzazi au mkongwe ndiye husema kauli hii, ambayo ni tasfida ya kushiriki tendo la ngono. Anaposema kauli hii huwa anatoa taarifa kwa jamii hivyo basi, ni uarifishaji kwamba mvulana anatosha kushiriki ngono. Usemi wa neno ‘kula’ umetumika kwa muktadha wa mapenzi kumaanisha kushiriki tendo la ndoa. Mkakati huu hulenga kumtambulisha mhusika kwa njia ambayo inaweza kupunguza au kuzidisha namna wanavyosawiriwa kwa hivyo, hapa anasawiriwa kama mtu aliyekomaa. Hali hii pia ni udhalilishaji wa mwanamke, ambapo mwanamke analinganishwa na chakula. Katika jamii hii mwanaume amepewa hadhi ya kuanzisha mchakato wa ngono na kwa kawaida mwanamume hutoa posa ya ndoa. Hivyo basi, mwanaume amesawiriwa kama mtumiaji mkuu wa uke wa mwanamke. Aidha uke wa mwanamke umesawiriwa kama chakula ambacho mwanamume hula. Hivyo basi, neno ‘kula’ limetumika ili kupunguza makali badala ya kutaja tendo la kushiriki ngono. Aina ya diskosi iliyotumika katika kauli hii ni diskosi ya kula.

### **4.3.3 Sitiari**

Ojode (2017) anaelezea kuwa sitiari ni matumizi ya neno au fungu la maneno kwa njia fiche. Neno huweza kutumiwa kimawazo katika kutoa wasifu wa kitu au mtu fulani kwa kujaribu kuonyesha kuwa vyote vina sifa sawa. Ni kule kuhamisha maana kutoka dhana moja hadi nyingine. Ndung’u (2021) anadai kuwa kinachohamishwa ni tabia, umbo, au kazi ya kitu kwa kuihusisha na tabia au kazi ya kitu kingine. Hali hii hutokea tu iwapo msemaji wa kauli ana uwezo wa kulinganisha mambo tofauti katika mazingira yake. Fasiri hii inlandana na uchunguzi wetu kwa kuwa ngariba kwa kiwango fulani wametumia kauli zenye sitiari kuchochea fikra za hadhira. Sitiari hizi zimetumika kuendeleza maudhui ya mafunzo ya tendo la ndoa jandoni kama inavyojitokeza katika matini ifuatayo..

## **Kiamb. 8**

*'kakoyam kwam sorom nemi buut kut',*

### **Tafsiri**

Mvulana huyu ametoshea kula mnyama ambaye ana manyoya mdomoni,

Mkakati huu umetumika kuleta sitiari ya uke. Mhimili wa urejelezi umetumika ambapo mkakati wa unominishaji umehusika kwa kurejelea uke kama mnyama mwenye manyoya mdomoni. Hii ni sitiari ya uke wa mwanamke ambaye amekomaa. Kwa kawaida, mavuzi katika sehemu za siri huota wakati mtu amekomaa, hivyo basi mvulana anapata funzo la kufahamu mwenye anafaa kumhusisha katika tendo la ndoa. Katika jamii hii walioruhusiwa kushiriki ngono ni watu waliokomaa na kuoana. Sehemu ya siri ya mwanamke huwa na mavuzi na hivyo basi sitiari hiyo inalinganishwa na usemi wa maneno hayo kuwa mnyama mwenye manyoya mdomoni

Katika muktadha huu neno 'mdomo' limetumika kama sitiari ya uke wa mwanamke. Kwa kawaida, sehemu nyeti ya mwanamke huwa na sehemu mbili kuu; kinembe na uke. Kinembe ni kinyama kilichoko mlangoni mwa uke ambacho husababisha mwanamke kupata ashiki ya kukutana na mwanamume. Katika utafiti huu ulimi ndioa unatumika kama sitiari ya kinembe. Nacho kinywa kinatumika kama sitiari ya uke. Hivyo basi, aina ya diskosi inayotumiwa hapa ni majina ya wanyama, ambapo diskosi hii inafanua uke wa mwanamke kama mdomo yaani sitiari ya kufanikisha tendo la ndoa.

#### **4.3.4 Taashira**

Kamusi Kuu ya Kiswahili (2015), taashira ni hali ya kitu kinachoashiria jambo fulani. Kamusi ya TUKI (2011) inafanua taashira kama alama ya kuonyesha hali au kitendo kitakachofanyika.

Loynce (2016) katika senkoro (1982) alieleza taashira kama kutumia lugha kiishara ili kwakilisha ujumbe, jambo au jinsi kitu fulani kinavyotumiwa kuwakilisha kitu kingine na kile kilichotumiwa.

## **Kiamb. 9**

*Igochin motiryot tarusyot age tugul ketit asi koipchi chemeriat anan ko chepto ako konyolu kotinyeen kirokotet kubesto, suet ak batet yeityo komwa kole “karokoite tugukab lakwandit ako achopot atoi sobet age” kowalu agine chemeriat kule “Karataach” ak konam kirokto, kou yekakineet agine en menjo nenywan chemosyan, ak kwa oinet kowirchi beek kirokotet asi kolaa beek.*

## **Tafsiri**

Mtahiriwa hupewa kijiti maalum na ngariba na anapaswa kugusa paja, kiuno au mgongo wa msichana kwa kufuta kile kijiti na sehemu hiyo ya mwili. Mvulana anapaswa kusema ‘nimepeana kila kitu cha utoto wangu na niko tayari kuingia sehemu ya mwisho wa maisha’. Baada ya msichana kukishika, anatarajiwa kuenda mtoni na kukitupa kile kijiti kisombwe na maji.

Kijiti hiki, ni ishara ya dhakari ya mtahiriwa ambayo imeelekezwa kwa mwili wa msichana. Mhimili wa mkabala umetumika kuchangunua kitendo hiki, kwani masimulizi yamewasilishwa kwa njia ya taashira au ishara. Mkakati wa mkabala hunuia kueleza jinsi jambo au tendo fulani linavyofasiriwa katika jamii husika na inavyochukuliwa na itikadi za jamii. Matumizi ya kijiti kinaashiria kwamba mvulana anatarajiwa kushiriki tendo la ndoa na msichana mwenye rika moja. Isitoshe, upande wa wasichana ni ishara ya kukubali kila ncha ya mwanamume kuingizwa kwa uke wake wakati wa tendo la ndoa. Kutupa kijiti majini ni ishara ya kuacha tabia zote za kitoto na kuingia katika utu uzima. Aina ya diskosi zilizotumika katika kitendo hiki ni vijiti na maji ambazo ni ishara ya kukubaliwa kushiriki tendo la ndoa.

## **Kiamb. 1**

*Kikyaen en mabwaita tumii, ako kikichomchin biik chekiba tum kityo en yotet. Kitechee kiit neu munandet netinye kurget ak kinde kiptangasiat anan ko menet ak ketesyi suswek barak. En tumii kekanye tarusyot konyo akoi mundanet elee miten chepkamet. Nyolu koboisyen tarusyek keldo kotyech ngatatiet akoileen kubestab chepkam konyil somok. Yekakotar kokochi kwanda kirokto ak panget asi kotil kirokotet, oloon testetai kotile kotebee motiryet kole “ngete nana mongete” ak kowool kwanda agine kole “ngetee” yeityo koketyi kotyech nyatatek ak koilen kameet kora kou ye kayai en chepkamet.*

## **Tafsiri**

Wahusika huwa ni mama mzazi, baba mzazi, ngariba, mvulana ambaye ametahiriwa na wanajamii ambao wametahiriwa. Ua linatengenezwa likiwa na lango ambapo mtahiriwa atapita kisha chini yake samadi ya ngombe au udongo uliofinyangwa huwekwa juu ya nyasi. Katika sherehe hii, msichana ambaye ni ndugu yake mtahiriwa atatumia mguu wake kumpaka mvulana mtahiriwa ile samadi au udongo mara tatu katika paja lake. Baada ya mchakato wa kwanza, mama mzazi atamsubiri pale na mtahiriwa akiwasili atapewa kijiti na babake mzazi na kukata kwa upanga. Baada ya kukata, atakanyaga udongo ulio chini kwa kutumia mguu na kuwekelea kwenye paja la mamake na mamake pia atafanya hivyo. Hayo yakiendelea ngariba ataseme 'ng'ete anan mang'ete' (itakatika ama haitakatika?) huku baba mzazi akijibu; 'ng'ete' (itakatika).

Kitendo hiki kimejikita katika mhimili wa mkabala kwani masimulizi yamewasilishwa kwa njia ya taashira au ishara. Mhimili wa mkabala hunuia kueleza jinsi jambo au tendo fulani linavyofasiriwa katika jamii husika na inavyochukuliwa na itikadi za jamii. Matumizi ya, samadi au udongo ambao umeelekezwa kwa paja huku mguu ukitumika kama ala ni taashira au ishara ya kushiriki tendo la ndoa. Udongo au samadi kuwekwa kwenye ua, unaashiria tendo la kuamsha ashiki za ngono miongoni mwa wahusika, kwa kawaida ashiki au ari ya ngono huamshwa na mguso wa sehemu nyeti. Ua hilo ni ishara ya uke wa mwanamke, aidha, ua hilo haliwezi kushirikishwa na mtu mwingine, bali ni yeye pekee ndiye hupita. Aina za diskosi ambazo zinajitokeza katika kitendo hiki ni diskosi za samadi, ua, sehemu za mwili kuashiria dhana mbalimbali katika tendo hili la ndoa.

## **Kiamb. 11**

*Tarusyot age tugul kiinete kochop kweisit asi kopoisien en loget ab taritik.  
Kweisit kotinye kebeberwek somok,*

## **Tafsiri**

Wavulana wanapokuwa jandoni hufunzwa kutengeneza kifaa cha kutumia kuwinda ndege. Kifaa hiki huitwa 'kweisit'. Kila mmoja hutengeneza kifaa hicho ambacho hutumiwa kuwinda ndege.

Kifaa hicho kinapokuwa tayari, vijana wanaenda nyanjani kuwinda ndege. Baada ya kufaulu katika mawindo. Ndege aliyenaswa na windo huletwa hadi pale jandoni na kuwekwa mahali mwafaka. Kisha vijana hawa wanaelekezwa na mzee ngariba kulenga shabaha moja kwa moja wakiwa foleni. Katika mchakato huo, kabla mvulana kulinga shabaha, ngariba atatamka ‘itagonga’ naye mtahiriwa atajibu ‘itampata’

Kifaa hiki kimetumika kama taashira ya dhakari, mchakato wa kutengeneza kifaa hiki ni ishara ya kutahiriwa, hivyo basi, wavulana wanapotahiriwa, ni taashira ya kuchonga mshale. Hivyo, mhimili wa mkabala umetumika kuchanganua kitendo hiki kwani, ujumbe unawasilishwa kwa njia ya taashira au ishara. Mhimili wa mkabala hunuia kueleza jinsi jambo au tendo fulani linavyofasiriwa katika jamii husika na inavyochukuliwa na itikadi za jamii. Umbo lake na utendakazi wake ni sawa na dhakari. Aidha, ndege anayewindwa ni ishara ya uke, ambapo mwanamume anafaa kufikia wakati wa tendo la ndoa. Itikadi inayojitokeza hapa ni kwamba wanaume ndio huwinda wanawake katika jamii hii. Mchakato wa kulenga shabaha kwa kutumia kifaa hicho ni mafunzo ya kulenga uke wa mwanamke wakati wa kushiriki tendo la ndoa. Aidha, mshale kulenga sawasawa ni ishara ya kushiriki ngono na mwanamke kuwa mja mzito. Aina za diskosi zinazojitokeza kitaashira katika kitendo hiki ni diskosi za ndege, mshale na uwindaji.

### **Kiamb. 12**

*Tumii keyae en oinet anan ko silanga. Kitechee munandet netinye kurget en beek orit keboisen isyeek, munandet notet kegureen musangit.*

### **Tafsiri**

‘Kayaet ab taruusyek’. ni sherehe ya kutakasa watahiriwa katika mto, Ngariba hutengeneza ua lililo na umbo la lango ndani ya maji. Ua lilitengenezwa na majani ya mmea fulani ambao ukiguza mwili unawasha na kusababisha uchungu.

Majani mabichi yanayowasha yametumika kitaashira kwa hivyo, mhimili wa mkabala umetumika kuchanganua kitendo hiki kwani kitendo hiki, kinawasilisha ujumbe kwa njia ya taashira au ishara. Mkakati wa mkabala hunuia kueleza jinsi jambo au tendo fulani linavyofasiriwa katika jamii husika na inavyochukuliwa na itikadi za jamii.

Matumizi ya majani yanayowasha ni taashira ya kutoa funzo la kujitahidi na kustahimili matatizo yanayoambatana na ushiriki wa tendo la ndoa. Kwa kawaida, mvulana hutarajia kumwoa msichana bikira, hivyo basi, ugumu na uchungu wa mchakato huu ni taashira ya kuvunja ubikira wa mwanamke. Aidha, majani haya yanaashiria kwamba iwapo utashiriki ngono nje ya ndoa kuna baadhi ya matatizo utakumbana nayo kama vile magonjwa hatari na kuvunja ndoa yako. Itikadi inayowasilishwa kitaashira ni kutakasa watahiriwa katika mto kuashira wameacha tabia za kitoto na kuingia katika utu uzima.

#### **4.3.5 Nyimbo**

Wimbo ni utungo ambao hufuata mapigo ya mahadhi ya kupanda na kushuka kwa kuzingatia urari wa sauti maneno yaliyopangwa kwa mpangilio maalum. Muundo wa nyimbo huwa wa lugha ya mkato na matumizi ya taswira. Katika kazi, mtafiti alibaini nyimbo zifuatazo kwenye kiambatisho 13 na 14, ambazo zina maudhui yanayofungamana na shughuli za jandoni. Maudhui yanayojitokeza ni bidii na tendo la ndoa.

#### **Kiamb. 13**

*Chepokumiin tiony ooh eeh*

*Kumiin tiony sigiriet*

*Chepune ainab tich*

***Tafsiri***

Wa kutenda ngono kwa uuke ooh eeh

Tenda kwa ukakamavu kama punda

Ingiza kwa uuke

#### **Kiamb. 15**

*Kisole chii kwony*

*Chii kwony konon buus*

*Chepokerta oor*

*Kerta oor masielel*

## **Tafsiri**

Mwanamke hubembelezwa

Mwanamke nipee uuke

Uke na uume kuingiana ipasavyo

Kuingiana ipasavyo hadi kilele

Matumizi ya nyimbo ni mojawapo ya mikakati ya kupitisha mafunzo kuhusu masuala ya ndoa katika muktadha wa jandoni. Mhimili wa uarifishaji ulitumika kuchanganua diskosi za nyimbo. Mhimili huu huja baada ya unominishaji, hivi kwamba baada ya kutambua mhusika au kundi fulani mkakati wa uarifishaji hufuata. Katika nyimbo hizi wahusika wametambuliwa kuwa ni mwanamke na mwanamume. Mkakati huu hueleza tabia kwa njia hasi na chanya kwa kutumia maelezo ya lugha kwa uwazi kwa mfano, mshororo wa pili umetumia lugha kwa uwazi unaposema *mwanamke nipee uke*. Mkakati huu hulenga kumtambulisha mhusika kwa njia ambayo inaweza kupunguza au kuzidisha namna wanavyosawiriwa. Nyimbo hizi zinadhihirisha mafunzo ya kubembeleza mwanamke ili ashiriki ngono. Hii ina maana kwamba lazima kuwe na maelewano katika suala la tendo la ndoa na kila mshiriki atafurahia.

### **4.3.6 Stihizai**

Hii ni mbinu ya kutumia dhihaka katika kuwasilisha mafunzo katika muktadha wa jandoni. Dhihaka hutumiwa ili kuondoa urasmi mingoni mwa watu. Pia ni mbinu inayotumiwa kuondoa fedheha miongoni mwa wanatohara. Kwa mfano

#### **Kiamb. 16**

*Watahiriwa wanapokuwa jandoni baada ya kukabiliana na kisu cha ngariba na kuelekea kupona, ajuza huandamana na ngariba hadi jandoni. Mama huyu hupewa jina la kimajazi Chemenjo. Watahiriwa hutishiwa kushiriki ngono na mama huyo mkongwe licha ya wao kutopona kwa umme wao.*

Matini hii inawasilisha stihizai inayotumiwa katika muktadha wa jandoni ambapo ajuza anafika jandoni na kufanya dhihaka kwamba wavulana waliopashwa tohara watahiriki ngono naye. Mhimili wa ubishi ulitumika kuchanganua kitendo hiki, kwani kuna dhana ya topoi ambayo imetumika kama mbinu ya upembuzi kwa mfano; kitendo cha ajuza

kufika jandoni. Mkakati huu huwa na ukuruba wa ndani wa matukio ya ushawishi na uhalalishaji wa usemi wa kibaguzi. Mathalan, mama mzee hudhuhaki kwamba atashiriki ngono na wavulana waliopashwa tohara. Topoi hufafanuliwa kama sehemu ya ubishi inayohusiana na uwajibikaji wa ukweli. Ubishi unajitokeza kwani ni nadra sana ajuza kushiriki ngono na wavulana wa umri mdogo. Zaidi ya hayo, hawa wavulana hawajapona hivyo basi, ni mbinu ya utopia tu inayotumiwa. Topoi huelezwa kama jambo lenye maana, faida na kasoro, kwa hivyo katika kitendo hiki faida inayopatikana ni funzo kwa watahiriwa kwamba hawapaswi kushiriki ngono na wakongwe. Aidha, kuna kasoro iwapo watapata ashiki za ngono wakimwona ajuza huyu. Mchakato huu ni funzo kuwa watakapotoka jandoni, hawafai kushiriki tendo la ndoa na mwanamke anayewazidi umri. Ifahamike kwamba, mambo huwekwa wazi jandoni na sehemu nyeti huonekana na ni sharti ngariba aweze kukagua kila mara.

Diskosi hii ya ajuza kuwatembelea ni njia ya kuwajaribu na kutambua mtahiriwa ambaye ataweza kupata ashiki za ngono au misuli ya uume kuisimuka. Iwapo kutatokea mtahiriwa atakayesisimuka kingono, basi hupewa adhabu ya kutosha na ngariba. Hii ni mbinu ya kuhakikisha na kumzuia mtahiriwa kutopata ashiki za ngono na ajuza.

## **SURA YA TANO**

### **MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **5.1 Utangulizi**

Utafiti huu ulilenga kuchanganua mada za diskosi ya tendo la ndoa zinazofunzwa jandoni. Aidha, utafiti huu ulitathmini mikakati inayotumiwa katika mafunzo ya diskosi za tendo la ndoa. Maswali ya utafiti yalikuwa; ni mada zipi za diskosi ya tendo la ndoa zinazodhihirika katika mafunzo ya jandoni katika jamii ya Wakipsigis? Mikakati ipi inayotumiwa katika mafunzo ya diskosi za tendo la ndoa zinazofunzwa jandoni katika jamii ya Wakipsigis? Katika sura hii tumezingatia muhtasari wa yale yaliyoshughulikiwa katika tasnifu yote na kutoa mapendekezo kwa watafiti wa baadaye kuhusu mada ya Diskosi ya mafunzo ya tendo la ndoa katika jando miongoni mwa Wakipsigis.

#### **5.2 Muhtasari wa Tasnifu**

Tasnifu hii ilihusu uchanganuzi wa diskosi kuhusu lugha ya tendo la ndoa miongoni mwa jamii ya Kipsigis. Sura ya kwanza ina usili wa mada, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, upeo na mipaka ya utafiti na umuhimu wa utafiti. Sura ya pili inahusu mapitio ya maandishi ambayo yamefanywa kulingana na madhumuni ya utafiti. Pia kuna sehemu ya msingi wa nadharia. Katika sura ya tatu ni mbinu za utafiti. Nayo sura ya nne inahusu uwasilishaji na uchanganuzi wa data. Sura ya tano ni mahitimisho na mapendekezo ya utafiti huu.

#### **5.3 Matokeo ya Utafiti**

Utafiti huu ulifaulu kujaza pengo lililokusudiwa na mtafiti kwani maswali ya utafiti yalijibiwa. Katika kuafiki, madhumuni ya kwanza ya utafiti ya kubainisha na kufafanua mada za diskosi ya tendo la ndoa zinazofunzwa jandoni. Mtafiti alizibaini mada zifuatazo; idhini ya kushiriki tendo la ndoa, kiwango cha kushiriki tendo la ndoa, jinsi ya kushiriki tendo la ndoa unyeti na maadili ya tendo la ndoa. Katika jamii ya Kipsigis idhini ya kwanza ambayo mvulana anapewa ili kushiriki tendo la ngono lazima akabiliane na kisu cha ngariba. Mafunzo haya hutolewa na ngariba kwa wavulana walio jandoni. Husheheni namna ya kutongoza msichana na jinsi ya kuanzisha mchakato wa kushiriki ngono. Maadili katika masuala ya tendo la ngono ni mambo muhimu katika jamii hii na yanapaswa kuzingatiwa kwa undani. Katika muktadha wa jandoni mafunzo ya maadili kuhusu tendo la ngono hupitishwa na wazee kwa vijana wanaopashwa

tohara. Mada hizi zilichanganuliwa kwa kuzingatia mihimili ya urejelezi, ubishi na ufifishaji

Mtafiti pia alifaulu kuafiki madhumuni ya pili ambayo yalikuwa kuchanganua mikakati inayotumiwa katika mafunzo ya diskosi za tendo la ndoa. Utafiti huu ulibaini mikakati ifuatayo; jazanda, tasfida, sitiari, taashira, nyimbo na stihizai. Jazanda zinarejelea uhalisia wa maisha na watahiriwa wanapaswa kufanyia ujarabati baada ya kufuzu jandoni. Katika muktadha wa jandoni wavulana wanapofunzwa kuhusu masuala ya tendo la ngono istilahi za tasfida hutumika. Istilahi hizi huundwa kwa kutumia mikakati ya mkabala wa kihistoria mathalan mkakati wa urejelezi na ufifishaji. Mafunzo ya tendo la ndoa huandamana na nyimbo. Nyimbo hizi zilidhihirisha maudhui ya bidii na tendo la ndoa. Mbinu ya istihizai au kejeli ilitumika katika kuwasilisha mafunzo jandoni. Dhihaka ilitumiwa ili kuondoa urasmi mingoni mwa watahiriwa, pia ni mbinu inayotumiwa kuondoa fedheha miongoni mwa wanatohara. Utafiti huu ulibaini kwamba katika sherehe hizi ambazo huandamana na miviga mbalimbali, wanafamilia huhusishwa kwa kila hatua kama vile baba, mama, dada na wanajamii wakongwe ili kuleta ukubalifu wa mafunzo haya.

Fauka ya hayo, utafiti huu umebainisha kuwa kuna mafunzo ya jandoni ambayo husheheni historia ya jamii ya Wakipsigis na mchakato wa mafunzo hayo huhusisha mikakati mbalimbali. Hivyo basi, uchanganuzi usemi mkabala wa kihistoria ulikuwa nadharia mwafaka ya kuchanganua mafunzo haya kwa kuangazia kwa undani mikakati mbalimbali inayohusiana na masuala ya jandoni.

#### **5.4 Mapendekezo**

Mtafiti amechunguza na kuchanganua mafunzo ya tendo la ndoa katika jando miongoni mwa Wakipsigis. Mtafiti anapendekeza haya;

Utafiti ulijikita katika diskosi ya mafunzo ya jandoni miongoni mwa wanajamii wa Kipsigis. Utafiti huu unapendekeza kuwa watafiti wengine wachunguza diskosi ya kujamiiana katika maisha ya kawaida katika jamii hii. Vilevile, ni mapendekezo ya mtafiti ni kwamba tafiti zaidi zifanywe kuhusu diskosi mbalimbali za jando kwa kuzingatia nadharia tofauti na iliyotumiwa katika utafiti huu.

Suala muhimu na la msingi katika mafunzo ya jando ni kudhihirisha jinsi historia, imani na itikadi zinavyotekelezwa katika jamii hata hivyo, utafiti huu haukujishughulisha na mambo hayo. Kwa hivyo, tulipendekeza watafiti wengine kushughulikia masuala ya mafunzo ya jandoni katika jamii ya Wakipsigis au jamii nyingine.

Utafiti huu haukuchunguza taaluma ya nyimbo zinazoimbwa jandoni katika jamii ya Wakipsigis bali ulijikita zaidi kuchunguza diskosi zinazotumika katika mafunzo tu. Hivyo basi, mtafiti anapendekeza utafiti ufanywe katika taaluma ya nyimbo na maudhui ya nyimbo hizo.

Mojawapo ya dhima ya fasihi ni kuelimisha jamii. Tulipendekeza watafiti wengine kuchanganua maudhui ya uaminifu katika ndoa, athari za talaka katika jamii ya Wakipsigis na mtazamo wa jamii kuhusu kupanga uzazi. Mambo haya hayakushughulikiwa katika utafiti huu. Utafiti ufanywe kuhusu usasa wa sherehe zingine za Afrika kwa kuzingatia vipengele vya lugha na vitanzu vingine vya fashi ili kudhihirisha mitindo ya lugha inayotumika katika viviga vya kisasa.

## **5.5 Hitimisho**

Kwa kuhitimisha ni kwamba tumetoa muhtasari wa tasnifu yote ili kuwafaa wasomaji wa kazi hii. Mbali na muhtasari, sura hii imetoa mapendekezo ambayo yatawauni watafiti wa baadaye kuhusu mafunzo ya tendo la ndoa katika jando miongoni mwa Wakipsigis atapata msingi na mwanga wa jambo analotafitia.

## MAREJELEO

- Abudi, M., & Yieke, F. (2011) Language, Gender and power relations. Unpublished MA Thesis. Egerton University, Kenya.
- Austin, J. (1962). *How to Do Things with Words*. Cambridge: M.A Harvard University Press.
- Bach, K. (2008, Mei 31). Speech Acts. <http://online.sfsu.edu/kbach/spchacts.html>.
- Barasa, N (2014) *Discursive Strategies in Kenya's 2008 Post-Election Consultation*
- Beck, R. (2015). *Sheng: An Urban Variety of Swahili in Kenya*. Katika N. Nico, & H. Andrea
- Bible Society of Kenya. (1992). *Biblia. Habari Njema*. Nairobi: Bible Society of Kenya Boston: South end press.
- Bucholtz, M. & Hall, K. (2004). *Theorizing identity in language and sexuality research. Language in Speaking Youth. Revista Alicantina de Estudios Ingleses 24, 235-256.*
- Bucholtz, M. (2004). *Theorizing Identity in language and sexuality Research*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Butler, J. (1990). *Gender Trouble: Feminism and the subversion of identity*. London Routledge:
- Cain, K.& Nash, H.M.(2011) 'Exploring the intersections of migration,desire and intimacy'. Cambridge University Press.
- Cameron, D. & Kulick, D. (2003). *Language and Sexuality*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Chepkorir, F. (2016).*Uchanganuzi wa Mtindo Katika Tahariri ya Gazeti la Taifa Leo. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa iliyowasilishwa katika Chuo Kikuu Cha Nairobi.*
- Cole and J.H Morgan (Ed) *syntax and semantics vol,3.speech acts (pp.41 – 58)* New York Academic press.
- Connell, R. (2011). *Masculinity research and global society*. Pp. 51-72 in Esther Nganling Educational Publishers.
- Empowerment: Young Women and the Negotiation of Safe Sex*. London: The Tufnell Press.
- Fairclough N.(1989) *Language and Power*. London:Longman.
- Fairclough, N.(1995) *Critical Discourse Analysis*.London:Longman.

- Fairclough, N. (1993) 'Critical Discourse Analysis and the Marketization of public discourse', . New York: Pantheon
- Foucault, M. (1979). *The history of sexuality Vol.1*. London, Allen lane, Paris.
- Foucault, M. (1972). *The Archeology of Knowledge and the Discourse of Language*. New York.
- Foucault, M. (1977). *Politics, Philosophy Culture: Interviews and other Writings*. New York: Pantheon
- Foucault, M. (1978). *The history of sexuality*. New York: Pantheon.
- Gazeti la mwananchi tarehe 10 Oktoba 2010
- Gazeti la taifa leo tarehe 4 Aprili 2018
- Gonzalez, F., & Anna-Brita, S. (2011). *Expressive Devices in the Language of English and Spanish Discourse and Analysis* 4(2):133-168
- Goodman, R. (2005). *Pragmatism. Critical Concepts*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Greer, G. (2000). *The whole Women*. Anchor: London.
- Grice, H.P. (1989). *Studies in the way of Words*. Cambridge, Mass: Harvard University
- Hai-long, H. (2008) Intercultural study of euphemism in Chinese and English [on-line]
- Hall, K. & Bucholtz, M. (ed) (1995). *Gender articulated language and the society constricted self. Discourse and Analysis* 4(2):133-168
- Hamidullah, M. (1983). *Introduction to Islam*. Kwalalumpar: Polygraphic Press.
- Holland, J., Ramazanoglu, C., Scott, S., Sharpe, S., & Thomason, R. (1991). *Pressure, Resistance, Intercourse and Consent to Unwanted Sexual Intercourse: College Students' Dating Experiences in Three Countries. Journal of Sex Research* 31, 125- 131.
- Joseph, G.I & Lewis, J (1981). *Common differences: conflicts in black and white feminist perspective Journal of Education psychology, language in urban and Chicago University of Illinois press*
- Jumbe, A. (2015). *Matumizi ya Lugha katika Muziki wa Kizazi Kipya: Mifano kutoka katika Nyimbo za Mapenzi za Wasanii Inspecta Haroun Na Mwanafalsafa*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili ambayo haijchapishwa iliyowasilishwa katika Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Kakai, P. W. (1992): *Social Concepts in the Initiation Rituals of the Abatachoni: historical study*. M.A.Thesis, Kenyatta University.

- Karithi, F. (2015) *Ulinganuzi wa usemi wa kisiasa katika kampeni za urais nchini Kenya miezi mitano kabla ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 na 2013*. Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa) Chuo kikuu cha Laikipia.
- Kezilahabi, E. (1975). *Shaaban Robert: Mwandishi wa Riwaya*. Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Khaemba, J. M. (2013). *The Discursive Construction of Hegemonic Masculinities in Selected Rituals of the Bukusu of Kenya*. (Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa). Njoro: Ndaki ya Egerton
- Kieti, M. (1999). *Myali songs. Social Critique among the Kamba*. Tasnifu ya Uzamili: Chuo kikuu cha Kenyatta.
- Kieti, M. na Coughlin, P. (1990). *Barking, You Will Be Eaten. The Wisdom of Faith*. Nairobi, Kenya Literature Bureau.
- King'ei, K & Kisovi, C. N. M. (2005), *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi, Kenya Literature Bureau.
- Kingei, K. (1993) *Language Culture and Communication: The Role of Taarab Songs in Kenya* *Kritische Afrikastudien*, 9 (5), 123-149.
- Kwenye E. Uchendu, *Masculinities in Contemporary Africa*. CODESRIA
- Leap, W. na Boetlstorff, I. (Wahariri) (2004). *Speaking in Queer Tongues: Globalization and gay*. The Kenyan Experience Society 33:469 - 515.
- Leech, G. & Svartvik, J. (2002). *A Communicative Grammar of English*. London: Pearson Education Ltd. London: Routledge.
- M'Ngaruthi (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni: Kitabu cha Walimu na Wanafunzi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Manguliechi, W. J. (2007): *An Oral Interview at his Miruri home on zo" April 2007 on Bukusu Circumcision Songs and History*. Kenyatta University
- Malenya, M. (2008) *Matumizi ya Lugha na Jazanda katika nyimbo za Jacob Luseno*. Tasnifu ya Chuo kikuu cha Kenyatta.
- Markman, R.H, Markman, P.T and Waddel, M.L. (1982). *10 Steps in Writing the Reseach Paper*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Markman, R.H, Markman, P.T na Waddel, M.L. (1982). *10 Steps in Writing the Reseach Paper*. New York: Academic Press.
- Marshall, C and Rossman, G.B. (2006). *Designing Qualitative Research*. London: Sage Publications.

- Masayi, Z (2012). *Mahojiano ya ana kwa ana yaliyofanyika Bukonde, tarehe 23 Disemba*.
- Matei, A.K. (2011). *Fani ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: Oxford University Press.
- Mbiti, J.S (1969). *African Religions and Philosophy*. London: Hienemann
- Mohamed, S.A. (1995). *Kunga za Nathari. Katika Kiswahili*. Nairobi: East African
- Morgan (Wahariri). New York: Academic Press.
- Mugai, M.(2005) *Ubunifu wa mtafsiri katika tamthilia ya 'Masaibu ya Ndugu Jero' Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa) Chuo kikuu cha Kenyatta*.
- Mugenda, O. na Mugenda A. (1999). *Research Methods. Quantitative Approaches*. African Centre for Technology Studies.
- Mutwiri, G. (2005). *Mitazamo ya utendakazi wa Nyiso katika jamii ya Watigania. MA Thesis, Kenyatta University, Kenya*
- Nandwa, J. A. (1976): *Oral Literature of the Abaluhya*. University of Nairobi
- Nandwa, J., Bukenya, A. (1983). *African Oral Literature for Schools*. Nairobi: Longman.
- Ndemo, P.M. (2014). *Uchanganuzi wa Lugha ya Amani na Maridhiano katika Muziki Nchini Kenya(2008-2012)*.Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa iliyowasilishwa katika Chuo Kikuu cha Moi.
- Nguma, N. (2001). *Taswira ya Mwanamke Jinsi Iliyochorwa Katika Riwaya ya Kezilahabi*. uzamili (Haijachapishwa) Chuo kikuu cha Kenyatta.
- Nkumbo. D (2019) *Uchanganuzi wa Matangazo ya Ngoni Salama katika Mtandao wa Durex Facebook*. Phd Thesis laikipia university (Haijachapishwa)
- Nkumbo.D (2013) *Dhima ya Tafida na Lugha Mwiko katika Jamii ya Ameru laikipia university M.A (Haijachapishwa)*
- Nyaga, M. (1970): *Home and Family Social Changes: The Kikuyu*, Kenyatta University
- Ogechi, N. (2005). *The Language of Sex and HIV/AIDS Among. Stichpoben.Wiener Zeitschrift fur : African Journal of reproductive Health*. Tol.11. (3)
- Ogolla, A.R. (2007). *Uchanganuzi wa Jinsi lugha inavyotumika kuhamasisha wanawake kuhusu haki zao: Mfano kutoka wilayani Kisumu*. Tasnifu ya M.A, (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Egerton.
- Onyango, J. O. (2008). "Masculine Discursive Construction of Rape in the Kenyan Press": Division of Research and Extension, Egerton University

- Onyango, J. O. (2011). *Discursive Masculinities and The War Against AIDS*: Division of Research and Extension, Egerton University
- Padgett, D. (2002). *Qualitative Methods in Social Work Research: Challenges and Rewards*. London: pub.com.uk.
- Reisigl, M. na Wodak, R. (2001) 'The discourse-historical approach (DHA): History, agenda Sage Publications Inc.
- Routledge. (1996). *Routledge Dictionary of Language and Linguistics*. London: Routledge.
- Safinia, K.A. (2017). *Kuchunguza Matumizi ya Lugha na Dhamira katika Tamthilia Teule za Mwandishi Emmanuel Mbogo*. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa iliyowasilishwa katika Chuo Kikuu cha Tanzania.
- Searle, J. (1975). "Indirect Speech Acts". *Katika: Syntax and Semantics*. P. Cole na J.L. Sage Publications Inc.
- Senkoro, F.M. (1987). *Fasihi na jamii*. Dar es salaam : Press and Publicity Centre.
- Senkoro, K. (2006). *Fasihi ya Kiswahili ya Majaribio: Makutano baina ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi*. Kioo cha Lugha, 4, 22-38.
- Shiffrin, D. (1995). *Approaches to Discourse*. O.U.P: Blackwell Publishers Inc.
- Silverman, D. (2005). *Doing Qualitative Research*. London: SAGE Publications.
- Simiyu, F.W. (2007). *Nyiso za Wabukusu. Maudhui na Lugha*. Tasnifu ya Uzamili.
- Smith, B. (2008, May, 31). *Towards a History of Speech Acts Theory*. <http://ontology.buffalo.edu>.
- Sprecher, S., Hatfield, E., Cortese, A., Potapova, E., & Levitskaya, A. (1994). *Token Resistance to Sexual Youth Language Practices in Africa and Beyond* (kur. 51-80). Mouton: De Gruyter
- Steven, T.M. (2009, February 12) *Journal for the Study of the Old Testament*. <http://www.Sage> theory and methodology'. Katika R. Wodak na Meyer.
- TUKI (2004), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press
- UNAIDS, (2000). *Joint United Nation Programme on HIV/AIDS*. Geneva: Switzerland
- Undie, C. Crichton, J. & Zulu, E (2006). 'Talking about sex using youth languages in sexual Education'. University press.
- Van Dijk, T. (1997). *Discourse as social Interaction*: Sage publication

- Walya, E. (1995). *Discourse Strategies in Banking Discourse*. M.A. Thesis, Kenyatta University.
- Wamitila (2003), *Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd
- Wanjala, S. F, (2015). *Mwingilianotanzu katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika: Mfano wa Embalu na Mwaka Kogwa. Tasnifu ya Uzamifu*. Nairobi: Ndaki ya Kenyatta.
- Wanjala, S. F. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi: Kwa Shule, Vyuo na Ndaki*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers.
- Wardhaugh, R. (1992). *An Introduction to Sociolinguistics*. Oxford: Blackwell. Publishers  
 Wodak, R. (1996). *Critical Linguistics and critical analysis: handbook of pragmatics*. Amsterdam: Benjamins.
- Wodak, R., & Dijk, T. A. (2000). *Racism at the top. Parliamentary discourses on ethnic issues in six european states*. Klagenfurt: Drava.
- World Health Organization (WHO) (2005) *The World Health Report*.Switzerland: Geneva.York: Barrons Educational Series, Inc.

## VIAMBATISHO

### **Kiambatisho I: Ngariba 1:D1: Yatitaet (kukata)**

*Tumin ini keyoe en kotap tumiin, murenik chekikiyatita ak kwonyik ichegen chekiyonchin kochut kotap tumiin. Machamdayat kochut ng'etik anan ko korusyek. Yoon kikonye keip mecheita ketieni, ago yakakoit motiryot kotoche en tekisto ne oo. Yotitoi motiryot anan ko tarji ng'etet agenga agenge ago nyolu koboora muitaet ng'etet ingeyotitoi, yekakobata yatitaet ako kamuita inendet, kosimee chepyosok konyil ang'wan, akomwa kamet anan ko chepyoso kole, "kokoyam kwam sorom nemi buut kut". Kowool murenik en kipangenge kole "eeh kakoyam".*

### **Tafsiri**

Kukabiliana na kisu cha ngariba kwa ujasiri ni jambo ambalo linashabikiwa sana na wanajamii na ni ishara ya ushujaa. Sherehe hii hufanywa katika mazingira ya jando (tazama picha 4.2.D.1) na wanaume kwa wanawake ambao walipitia kisu cha ngariba ndio wanaoruhusiwa kuhudhuria. Sherehe hii inajulikana kama 'yatititaet' tafsiri yake ni kukata au kutoanisha. Ni hatia kwa wasichana wadogo kukaribia sehemu hiyo. Tendo hili huchukuliwa kuwa tendo la kisiri miongoni mwa wale waliopitia na wale ambao wanajitayarisha kupitia. Nyimbo mbalimbali huimbwa kabla kisu cha ngariba kuletwa na kisha ngariba kuwasili. Ngariba anapowasili, yeye hupewa heshima ya kipekee na kisha anaanza shughuli za kutahiri wavulana.

Kila mvulana anakabiliana na ngariba pekee huku wanawake na wanaume wakishuhudia kwa umbali. Katika mchakato huu, mvulana anapaswa kuonyesha ujasiri kwa kustahimili uchungu wa kisu. Wakati mvulana ametahiriwa bila kulia au kulalamika au kutikiza kichwa, basi kina mama wanashangilia na nderemo mara nne. Baada ya nderemo, mamake mzazi au ajuza atainua mikono na kusema kuwa, 'mvulana huyu ametoshea kula mnyama ambaye ana manyoya mdomoni, huku wanaume wataitika kwa kauli moja 'ametoshea'.



P4

### **Ngkv1Mutulik**

*Inoni ko tumdo ne kiyae yaan kamwetge tarusyek. Cheng'e tarusyot age tugul chemeriat anan ko chepto ne aechindos asi kobokokyi kirokto nekoikochin motiryot. Yekakonyoor chemeriat anan ko chepto konyolu kotinyeen kirokotet kubesto, suet ak batet yeityo komwa kole "karokoite tugukab lakwandit ako achopot atoi sobet age" kowalu agine chemeriat kule "Karataach" ak konam kirokto, kou yekakineet agine en menjo nenywan chemosyan, ak kwa oinet kowirchi beek kirokotet asi kolaa beek.*

### **Tafsiri**

Hii ni sherehe ya siku za mwisho katika jando baada ya watahiriwa kuoga miili yao, sherehe hii huitwa 'mutulik'. Kila mtahiriwa anaruhusiwa kutafuta msichana ambaye ako katika unyagoni au yeyote aliyebaleghe; mwenye umri sawa. Mtahiriwa hupewa kijiti maalum na ngariba na anapaswa kugusa paja, kiuno au mgongo wa msichana kwa kufuta kile kijiti na sehemu hiyo ya mwili. Mvulana anapaswa kusema 'nimepeana kila kitu cha utoto wangu na niko tayari kuingia sehemu ya mwisho wa maisha'. Iwapo msichana ako katika unyagoni anapaswa kuitika kwa kusema nimeipokea; huku akikabidhiwa kile kijiti. Katika upande mwingine, kuitika kwa msichana ni kuwa hata yeye amefunzwa na ngariba wao na alitarajia mchakato huo. Baada ya msichana kukishika, anatarajiwa kuenda mtoni na kukitupa kile kijiti kisombwe na maji.

**Ngkv2: Yatet ab oret (kufungua njia)**

*Kikyaen en mabwaita tumii, ako kikichomchin biik chekiba tum kityo en yotet.*

*Kitechee kiit neu munandet netinye kurget ak kinde kiptangasiat anan ko menet ak ketesyi suswek barak. En tumii kekanye tarusyot konyo akoi mundanet elee miten chepkamet. Nyolu koboisyen tarusyek keldo kotyech ngatatiet akoileen kubestab chepkam konyil somok. Yekakotar kokochi kwanda kirokto ak panget asi kotil kirokotet, oloon testetai kotile kotebee motiryet kole “ngete nana mongete” ak kowool kwanda agine kole “ngetee” yeityo koketyi kotyech nyatatek ak koilen kameet kora kou ye kayai en chepkamet.*

**Tafsiri**

‘Yatet ab oret’ (kufungua njia) ni sherehe ambayo ilifanywa katika mahali mwafaka; mashariki mwa chumba cha mzee wa boma. Wahusika huwa ni mama mzazi, baba mzazi, ngariba, mvulana ambaye ametahiriwa na wanajamii ambao wametahiriwa. Ua linatengenezwa likiwa na lango ambapo mtahiriwa atapita kisha chini yake samadi ya ngombe au udongo uliofinyangwa huwekwa juu ya nyasi. Katika sherehe hii, msichana ambaye ni ndugu yake mtahiriwa atatumia mguu wake kumpaka mvulana mtahiriwa ile samadi au udongo mara tatu katika paja lake. Baada ya mchakato wa kwanza, mama mzazi atamsubiri pale na mtahiriwa akiwasili atapewa kijiti na babake mzazi na kukata kwa upanga. Baada ya kukata, atakanyaga udongo ulio chini kwa kutumia mguu na kuwekelea kwenye paja la mamake na mamake pia atafanya hivyo. Hayo yakiendelea ngariba ataseme ‘itakatika ama haitakatika?’ huku baba mzazi akijibu; ‘itakatika’

**Ngkv3: Kweisit**

*Tarusyot age tugul kiinete kochop kweisit asi kopoisien en loget ab taritik. Kweisit kotinye kebeberwek somok, neta ko metit ne nerat, ak nebo aeng’ ko borto ne koi ako tenden kikureen merenget ak nebo somok ko katutyet nekindoi kororik ab ingongiet. Katutyet kechope kokararanit kokerkeit ak saruryet ab tarikit asi ko maiywei taritik. Yekakochobok kweisit konyolu komanda tarusyek koba loget kocheng’ taritik, ak yekakobor taritik koname motiryot ak konde mabwai asi kobangan en lain tarusyek kowiir sapaa age tugul. Oloon wiree*

*tarusyot age tugul komwae motiryot kole “kwere” kowolu tarusyot kole “kwere”.*

### **Tafsiri**

Wavulana wanapokuwa jandoni hufunzwa kutengeneza kifaa cha kutumia kuwinda ndege (tazama picha 4.2). Kifaa hiki huitwa ‘kweisit’. Kila mmoja hutengeneza kifaa hicho ambacho hutumiwa kuwinda ndege. Taswira ya kifaa hicho huwa na sehemu tatu; kichwa, mwili na mkia. Sehemu ya kichwa huwa ni kubwa na pana, ilhali mwili huwa mwembamba na ni laini. Sehemu ya mwisho ni mkia ambao huwekwa manyoya ya kuku. Mkia hurembeshwa kwa lengo la kuisaidia kuongeza mwendo kasi wa kifaa hicho kwa mawindo. Aidha, urembeshaji huo huwa na lengo la kupumbaza ndege wasiogope kifaa hicho na wawe na dhana ya kufananisha na kuku au ndege mwenzao.

Kifaa hicho kinapokuwa tayari, vijana wanaenda nyanjani kuwinda ndege. Baada ya kufaulu katika mawindo. Ndege aliyenaswa na windo huletwa hadi pale jandoni na kuwekwa mahali mwafaka. Kisha vijana hawa wanaelekezwa na mzee ngariba kulenga shabaha moja kwa moja wakiwa foleni. Katika mchakato huo kabla, mvulana kulenga shabaha, ngariba atatamka ‘’ itagonga’’ naye mtahiriwa atajibu ‘’ itampata’’





### Ng3kv5 3:D5: Kailet

*Inoni ko tumdo nekiyae en gaa kotomo kwoo ng'etet en gaa kotokyigee menjo. Kiyaen mabwaitab gaa nebo ng'etet, ago kiipu kuinetab teta nemiten orit mwaitab asi koileen chepkam togoch nebo ng'etatab kam newendi tum. En kailanitet konyolu koboisien eut ab taa, koileen togoch teget ak kubesto nebo kataam konyil ang'wan. Yekatotar kaileet komwachi kolenji "kakityakteen iwee" akowol ng'etet kole "karayan awoo".*

#### **Tafsiri**

'Kailet'(kupaka mafuta) ni sherehe iliyofanywa kabla ya mvulana kukabiliana na kisu cha ngariba, hii ilifanywa tu baada ya kuondoka kwao. Shughuli ilifanywa mahali mwafaka ambao hujulikana kama 'mabwaita' (sehemu ambayo imetakaswa) mafuta ya kujipaka huwekwa kwenye pembe ya ng'ombe na dadake mvulana huchaguliwa kumpaka mafuta hayo huku wanajamii wote wakimtazama. Katika mchakato huu ni sharti dadake atumie mkono wake wa kulia na kumpaka nduguye. Atampaka; kwenye utosi, kifua na paja la kushoto, kila upako hufanywa mara nne huku akizunguka sehemu hio mwafaka mara nne. Baada ya mchakato huo dadake atamwambia 'tumekuachilia utoke' naye mvulana atajibu 'nimekubali kutoka'.. Sherehe hizo zilikuwa za mwisho kabla ya mvulana kuondoka kwao kuelekea jandoni. Hii pia ilikuwa njia ya kumtakia mvulana mema akielekea safari ya jando na vilevile kila la heri katika shughuli zote za jando. Aidha, atakaporudi nyumbani atakuwa na ufahamu wa mila na desturi za jamii hio.

### **Ng3kv6: Kayaet ab taruusyek**

*Tumii keyae en oinet anan ko silanga. Kitechee munandet netinye kurget en beek orit keboisen isyeek, munandet notet kegureen musangit. Tumii koki oretab mwetetabgee netai en menjo kong'eten ingobaa menjo. Nyolu kotwolchi beek ak kochut orit kobuun kurget ab musangit ako mong'unen komosto nebo aeng' ako yekakomong' ketyenchin ak kikochi kainetab kekureen arap koboora kole kakoik murenik.*

### **Tafsiri**

Ni sherehe ya kutakasa watahiriwa, ambapo hufanywa katika mto au bwawa la maji. Sherehe hii hujulikana kama 'kayaet ab taruusyek'. Ngariba hutengeneza ua lililo na umbo la lango ndani ya maji. Ua hilo linatengenezwa na vijiti na majani ya mmea fulani ambao ukiguza mwili unawasha na kusababisha uchungu, tazama picha 4.2.D.6. Sherehe hii ilikuwa ya muhimu kwa sababu ni mara ya kwanza kuoga miili tangu waingie jandoni. Kila mtahiriwa alipaswa kuruka ndani ya maji kwa kuogelea na kuhakikisha ameingia katika lile ua lililo ndani ya maji kwa kutokea sehemu ya pili. Mtahiriwa anapofaulu kupita lile ua basi hupewa jina la heshima ili aweze kuongeza katika jina lake, jina hilo ni araap. Jina hili ni la heshima kumaanisha amekuwa mwanamume na shujaa katika jamii. Sherehe hio huhusisha nyimbo mbalimbali za kitamaduni za kusifu wanaumme huimbwa papo hapo. Sherehe hii ni ya kipekee kwa sababu nyimbo hizo hazitaimbwa tena kwingine hadi sherehe nyingi kama hiyo ifanyike.



Dadake mvulana huchaguliwa kumpaka mafuta hiyo huku wanajamii wote wakimtazama. Katika mchakato huu ni sharti dadake atumie mkono wake wa kulia na kumpaka nduguye. Atampaka; kwenye utosi, kifua na paja la kushoto, kila upako hufanywa mara nne huku akizunguka sehemu hio mwafaka mara nne. Baada ya mchakato huo dadake atamwambia ‘tumekuachilia utoke’ naye mvulana atajibu ‘nimekubali kutoka’.

Sherehe hiyo ilikuwa ya mwisho kabla ya mvulana kuondoka kwao kuelekea jandoni. Hii pia ilikuwa njia ya kumtakia mvulana mema akielekea safari ya jando na vilevile kila la heri katika shughuli zote za jando. Aidha, atakaporudi nyumbani atakuwa na ufahamu wa mila na desturi za jamii hio.

Sherehe hizo ni za kipekee kwa sababu itakuwa mara ya mwisho kumkaribia dadake au msichana yeyote wa ukoo wake. Ikiwa alikuwa ameshiriki tendo la ndoa na dadake au msichana wa ukoo wao, basi sherehe hii ilikuwa ni njia ya kuomba msamaha na maneno alionena kuwa nimekubali kutoka ni ishara tosha kuwa hata fanya hivo tena au kuruhusu dadake kugusa paja lake kama vile amefanyiwa katika sherehe hii.

### **Mt1: Chemenjo**

*Chemenjo ko chepyoset ne kimutii kwoo menjo kotomo kosopcho ng’etik komie. Kikiboisien kimueen tarusyek kayai kesesnotet ak chemenjo. Tarusyot nekoibor makeet ab koyai kesesnotet kokinyoru kergong’et. Inoni koko oret nekiboorchin kelee monyolu koyai kesesnatet ak chepyoset neo.*

### **Tafsiri**

Watahiriwa wanapokuwa jandoni baada ya kukabiliana na kisu cha ngariba na kuelekea kupona, ajuza huandamana na ngariba hadi jandoni. Mama huyu hupewa jina la kimajazi Chemenjo. Watahiriwa hutishiwa kushiriki ngono na mama huyo mkongwe licha ya wao kutopona kwa

uume wao. Mchakato huo ni funzo kuwa watakapotoka jandoni hawafai kushiriki tendo la ndoa na mwanamke anayewazidi umri. Aidha, katika mchakato wa jandoni mambo huwekwa wazi kwamba sehemu nyeti yao huonekana na ni sharti ngariba aweze kukagua kila mara.

**Mt2:**

**W 1**

*Chepokumiin tiony ooh eeh*

*Kumiin tiony sigiriet*

*Chepune ainab tich*

**Tafsiri**

Wa kutenda ngono kwa uuke ooh eeh

Tenda kwa ukakamavu kama punda

Ingiza kwa uuke

**W2**

*Kisole chii kwony*

*Chii kwony konon buus*

*Chepokerta oor*

*Kerta oor masielel*

**Tafsiri**

Mwanamke hubembelezwa

Mwanamke nipee uuke

Uuke na uume kuingiana ipasavyo

Kuingiana ipasavyo hadi kilele



### **Kiamb.1**

*Yekaketar keyatitoo nge'etet ako kamuita, kosimee chepyosok konyil ang'wan, akomwa kaamet anan ko chepyoso kole, "kokayam kwam sorom nemi buut kut". Kowool murenik en kipangenge kole "eeh kakoyam".*

### **Tafsiri**

Wakati mvulana ametahiriwa bila kulia au kulalamika au kutikiza kichwa, basi kina mama wanashangilia na nderemo mara nne. Baada ya nderemo, mamake mzazi au ajuza atainua mikono na kusema 'mvulana huyu ametoshea kula mnyama ambaye ana manyoya mdomoni, huku wanaume wataitika kwa kauli moja 'ametoshea.'

### **Kiamb.2**

*Nyolu kocheng'e tarusyot age tugul chemeriat anan ko chepto ne aechindos asi kobokokyi kirokto nekoikochin motiryot. Yekakonyoor chemeriat anan ko chepto konyolu kotinyeen kirokotet kubesto, suet ak batet yeityo komwa kole "karokoite tugukab lakwandit ako achopot atoi sobet age" kowalu agine chemeriat kule "Karataach" ak konam kirokto, kou yekakineet agine en menjo nenywan chemosyan, ak kwa oinet kowirchi beek kirokotet asi kolaa beek.*

### **Tafsiri**

Baada ya watahiriwa kuosha miili yao. Kila mtahiriwa anaruhusiwa kutafuta msichana ambaye ako katika unyagoni au yeyote aliyebaleghe; mwenye umri sawa. Mtahiriwa hupewa kijiti maalum na ngariba na anapaswa kugusa paja, kiuno au mgongo wa msichana kwa kufuta kile kijiti na sehemu hiyo ya mwili. Mvulana anapaswa kusema ‘nimepeana kila kitu cha utoto wangu na niko tayari kuingia sehemu ya mwisho ya maisha’. Iwapo msichana ako katika unyagoni anapaswa kuitika kwa kusema nimeipokea; huku akikabidhiwa kile kijiti. Baada ya msichana kukishika, anatarajiwa kuenda mtoni na kukitupa kile kijiti kisombwe na maji.

### **Kiamb. 3**

*Kitechee kiit neu munandet netinye kurget ak kinde kiptangasiat anan ko menet ak ketesyi suswek barak. En tumii kekanye tarusyot konyo akoi mundanet elee miten chepkamet. Nyolu koboisyen tarusyek keldo kotyech ngatatiet akoileen kubestab chepkam konyil somok. Yekakotar kokochi kwanda kirokto ak panget asi kotil kirokotet, oloon testetai kotile kotebee motiryet kole “ngete nana mongete” ak kowool kwanda agine kole “ngetee” yeityo koketyi kotyech nyatatek ak koilen kameet kora kou ye kayai en chepkamet.*

### **Tafsiri**

Ua lilitengenezwa likiwa na lango ambapo mtahiriwa atapita kisha chini yake samadi ya ng'ombe au udongo uliofinyangwa huwekwa juu ya nyasi. Katika sherehe hii, msichana ambaye ni ndugu yake mtahiriwa atatumia mguu wake kumpaka mvulana mtahiriwa ile samadi au udongo mara tatu katika paja lake. Mama mzazi atamsubiri pale na mtahiriwa akiwasili atapewa kijiti na babake mzazi na kukikata kwa upanga. Baada ya kukikata, ataukanyaga udongo ulio chini kwa kutumia mguu na kuuwekelea kwenye paja la mamake na mamake pia atafanya hivyo. Hayo yakiendelea ngariba atauliza baba mzazi wa mtahiriwa 'itakatika ama haitakatika?' huku baba mzazi akijibu; 'itakatika'.

### **Kiamb. 4.**

*Tumii keyae asikobit kwoo ng'etet en gaa koriin. Nyolu komiten kuinetab teta nemiten orit mwaita asi koileen chepkam togoch nebo ng'etatab kam newendi tum. En kailanitet konyolu koboisien eut ab taa, koileen togoch teget ak kubesto*

*nebo kataam konyil ang'wan. Yekatotar kaileet komwachi kolenji "kakityakteen iwee" akowol ng'etet kole "karayan awoo".*

### **Tafsiri**

Katika sherehe hii, mafuta ya kujipaka huwekwa kwenye pembe la ng'ombe na dadake mvulana huchaguliwa kumpaka mafuta hayo huku wanajamii wote wakimtazama. Katika mchakato huu, ni sharti dadake atumie mkono wake wa kulia na kumpaka nduguye. Atampaka; kwenye utosi, kifua na paja la kushoto, kila upako hufanywa mara nne huku akizunguka sehemu hio teule mara nne. Baada ya mchakato huo dadake atamwambia 'tumekuachilia utoke' naye mvulana atajibu 'nimekubali kutoka'.

### **Kiamb. 5.**

*Tumii koki oretab mwetetabgee netai en menjo kong'eten ingobaa menjo. Kitechee kiit neu munandet netinye kurget en beek orit keboisen isyeek, munandet notet kegureen musangit. Nyolu kotwolchi beek ak kochut orit kobuun kurget ab musangit ako mong'unen komosto nebo aeng' ako yekakomong' ketyenchin ak kikochi kainetab kekureen arap koboora kole kakoik murenik.*

### **Tafsiri**

Katika sherehe ya kutakasa watahiriwa, ngariba hutengeneza ua lililo na umbo la lango ndani ya maji. Ua hilo linatengenezwa na vijiti na majani ya mmea fulani ambao ukiguza mwili unawasha na kusababisha uchungu. Kila mtahiriwa alipaswa kuruka ndani ya maji kwa kuogelea na kuhakikisha ameingia katika lile ua lililo ndani ya maji kwa kutokea sehemu ya pili. Mtahiriwa anapofaulu kupita lile ua basi hupewa jina la heshima.

**Jedwali la majina ya kitafsidi ya kurejelea sehemu za siri.**

	<b>Muktadha wa jandoni</b>	<b>Tafsiri (Muktadha wa jandoni)</b>	<b>Muktadha wa kawaida</b>	<b>Tafsiri (Muktadha ya kawaida)</b>
1.	<i>Kipkererwet</i>	Bonde linaloraruka	<i>Mokolet</i>	Uuke
2.	<i>Monyiset</i>	Kionja vimiminio	<i>Ndirit</i>	Dhakari
3.	<i>Sotonik ab lakwa</i>	Vibuyu vya mtoto	<i>Kinaik</i>	Matiti
4.	<i>Kimestowet</i>	Mchungaji wa mifugo	<i>Kwetiot</i>	Matako
5.	<i>Nyusit</i>	Malazi nyororo	<i>Buutek</i>	Mavuzi
6.	<i>Tolikenik</i>	Mbegu	<i>Mukuik</i>	Makende

**Kiamb. 6**

*Kisiimee chepyosok konyil ang'wan, akomwa kamet anan ko chepyoso kole, "kokayam kwam sorom nemi buut kut". Kowool murenik en kipangenge kole "eeh kakoyam".*

**Tafsiri**

Baada ya nderemo, mamake mzazi au ajuza atainua mikono na kusema tafsiri yake ni kuwa, mvulana huyu ametoshea kula mnyama ambaye ana manyoya mdomoni, huku wanaume wataitika kwa kauli moja tafsiri yake ametoshe' ,

**Tafsiri**

Mvulana huyu ametoshea kula mnyama ambaye ana manyoya mdomoni,

**Kiamb. 9**

*Igochin motiryot tarusyot age tugul ketit asi koipchi chemeriat anan ko chepto ako konyolu kotinyeen kirokotet kubesto, suet ak batet yeityo komwa kole "karokoite tugukab lakwandit ako achopot atoi sobet age" kowalu agine chemeriat kule "Karataach" ak konam kirokto, kou yekakineet agine en menjo nenywan chemosyan, ak kwa oinet kowirchi beek kirokotet asi kolaa beek.*

**Tafsiri**

Mtahiriwa hupewa kijiti maalum na ngariba na anapaswa kugusa paja, kiuno au mgongo wa msichana kwa kufuta kile kijiti na sehemu hiyo ya mwili. Mvulana anapaswa kusema 'nimepeana kila kitu cha utoto wangu na niko tayari kuingia

sehemu ya mwisho wa maisha'. Baada ya msichana kukishika, anatarajiwa kuenda mtoni na kukitupa kile kijiti kisombwe na maji.

#### **Kiamb. 10**

*Kikyaen en mabwaita tumii, ako kikichomchin biik chekiba tum kityo en yotet. Kitechee kiit neu munandet netinye kurget ak kinde kiptangasiat anan ko menet ak ketesyi suswek barak. En tumii kekanye tarusyot konyo akoi mundanet elee miten chepkamet. Nyolu koboisyen tarusyek keldo kotyech ngatatiet akoileen kubestab chepkam konyil somok. Yekakotar kokochi kwanda kirokto ak panget asi kotil kirokotet, oloon testetai kotile kotebee motiryet kole "ngete nana mongete" ak kowool kwanda agine kole "ngetee" yeityo koketyi kotyech nyatatek ak koilen kameet kora kou ye kayai en chepkamet.*

#### **Tafsiri**

Wahusika huwa ni mama mzazi, baba mzazi, ngariba, mvulana ambaye ametahiriwa na wanajamii ambao wametahiriwa. Ua linatengenezwa likiwa na lango ambapo mtahiriwa atapita kisha chini yake samadi ya ng'ombe au udongo uliofinyangwa huwekwa juu ya nyasi. Katika sherehe hii, msichana ambaye ni ndugu yake mtahiriwa atatumia mguu wake kumpaka mvulana mtahiriwa ile samadi au udongo mara tatu katika paja lake. Baada ya mchakato wa kwanza, mama mzazi atamsubiri pale na mtahiriwa akiwasili atapewa kijiti na babake mzazi na kukata kwa upanga. Baada ya kukata, ataukanyaga udongo ulio chini kwa kutumia mguu na kuwekelea kwenye paja la mamake na mamake pia atafanya hivyo. Hayo yakiendelea ngariba ataseme 'ng'ete anan mang'ete' (itakatika ama haitakatika?) huku baba mzazi akijibu; 'ng'ete' (itakatika).

#### **Kiamb. 11**

*Tarusyot age tugul kiinete kochop kweisit asi kopoisien en loget ab taritik. Kweisit kotinye kebeberwek somok,*

#### **Tafsiri**

Wavulana wanapokuwa jandoni hufunzwa kutengeneza kifaa cha kutumia kuwinda ndege. Kifaa hiki huitwa 'kweisit'. Kila mmoja hutengeneza kifaa hicho ambacho hutumiwa kuwinda ndege.

Kifaa hicho kinapokuwa tayari, vijana wanaenda nyanjani kuwinda ndege. Baada ya kufaulu katika mawindo. Ndege aliyenaswa na windo huletwa hadi pale jandoni na kuwekwa mahali mwafaka. Kisha vijana hawa wanaelekezwa na mzee ngariba kulenga shabaha moja kwa moja wakiwa foleni. Katika mchakato huo, kabla mvulana kulinga shabaha, ngariba atatamka ‘’ itagonga’’ naye mtahiriwa atajibu ‘’ itampata’’

### **Kiamb. 12**

*Tumii keyae en oinet anan ko silanga. Kitechee munandet netinye kurget en beek orit keboisen isyeek, munandet notet kegureen musangit.*

#### ***Tafsiri***

‘Kayaet ab taruusyek’. ni sherehe ya kutakasa watahiriwa katika mto, Ngariba hutengeneza ua lililo na umbo la lango ndani ya maji. Ua lilitengenezwa na majani ya mmea fulani ambao ukiguza mwili unawasha na kusababisha uchungu.

### **Kiamb. 13**

*Chepokumiin tiony ooh eeh*

*Kumiin tiony sigiriet*

*Chepune ainab tich*

#### ***Tafsiri***

Wa kutenda ngono kwa uuke ooh eeh

Tenda kwa ukakamavu kama punda

Ingiza kwa uuke

### **Kiamb. 15**

*Kisole chii kwony*

*Chii kwony konon buus*

*Chepokerta oor*

*Kerta oor masielel*

### *Tafsiri*

Mwanamke hubembelezwa

Mwanamke nipee uuke

Uuke na uume kuingiana ipasavyo

### **Kiamb. 16**

Watahiriwa wanapokuwa jandoni baada ya kukabiliana na kisu cha ngariba na kuelekea kuona, ajuza huandamana na ngariba hadi jandoni. Mama huyu hupewa jina la kimajazi Chemenjo. Watahiriwa hutishiwa kushiriki ngono na mama huyo mkongwe licha ya wao kutopona kwa umme wao.

## **Kiambatisho II: MWONGOZO WA MAHOJIANO**

Tafadhali jitambulisha; Majina, umri, ukoo, kata, kijiji na nafasi yako katika jamii.






### **A. Maswali kwa ngariba**

1. Umekuwa ngariba kwa miaka ngapi?
2. Watahiriwa wangapi wamepata mafunzo kwako?
3. Je, mafunzo hayo yana umuhimu katika jamii?
4. Taja mada unazofunza?
5. Fafanua zaidi kuhusu mada ya tendo la ndoa?
6. Eleza mikakati na mbinu za lugha unazotumia katika mafunzo ya tendo la ndoa?
7. Ni majukumu yapi yanayotengewa wanaume katika mafunzo hayo?
8. Ni majukumu yapi yanayotengewa wanawake katika mafunzo hayo?
9. Mwanamume husawiriwaje katika mafunzo hayo?
10. Mwanamke husawiriwaje katika mafunzo hayo?

### **B. Maswali kwa waliopashwa tohara**

1. Ulitahiriwa mwaka gani?
2. Ulitahiriwa katika mfumo wa rika gani?
3. Ni mada gani ulifunzwa jandoni?
4. Mambo gani muhimu ulifundishwa ukiwa jandoni kuhusu tendo la ndoa?
5. Eleza mbinu za kiujarabati ambayo ngariba alitumia kutoa mafunzo haya kuhusu tendo la ndoa?
6. Eleza jinsi mafunzo hayo yalivyofanyiwa ujarabati na utekelezi?
7. Je, kuna uhusiano wa mafunzo haya na uhalisia wa tendo la ndoa?
8. Mafunzo hayo yamekusaidiaje maishani?

### Kiambatisho III: Kibali cha kufanya utafiti nyanjani kutoka NACOSTI

 REPUBLIC OF KENYA	 NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY & INNOVATION
Ref No: 626053	Date of Issue: 01/October/2021
<b>RESEARCH LICENSE</b>	
	
<p>This is to Certify that Mr., NICHOLAS KIRUI of Laikipia University, has been licensed to conduct research in Bomet on the topic: <b>DISKOSI YA MAFUNZO YA TENDO LA NDOA KATIKA JANDO MIONGONI MWA WAKIPSIGIS</b> for the period ending : 01/October/2022.</p>	
License No: NACOSTI/P/21/13197	
626053 Applicant Identification Number	 Director General NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY & INNOVATION
	Verification QR Code 
<p>NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.</p>	

**Kiambatisho IV: Idhini ya kufanya utafiti nyanjani kutoka kwa afisi ya rais-  
Jimbo la Bomet.**



**OFFICE OF THE PRESIDENT**  
MINISTRY OF INTERIOR AND COORDINATION OF NATIONAL GOVERNMENT

Telegrams: "DISTRICTER", Bomet  
Telephone: (052) 22004/22077 Fax 052-22490  
When replying please quote

COUNTY COMMISSIONER  
P.O BOX 71- 20400  
**BOMET**

REF: EDU.12.1VOL.IV/(124)


5<sup>th</sup> October, 2021

The Deputy County Commissioners  
**BOMET**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION – MR. NICHOLAS KIRUI**

The above named person has been authorized to carry out research on "**Diskosi ya mafunzo ya tendo la ndoa katika jando miongoni mwa wakipsigis**" in Bomet County for the period ending 1<sup>st</sup> October, 2022 by the National Commission for Science, Technology and Innovation vide their letter Ref. No.626053 dated 1<sup>st</sup> October, 2021.

Any assistance accorded would be appreciated.

  
Hesbon Kayesi  
For: County Commissioner  
**BOMET**



**Kiambatisho V: Idhini ya kufanya utafiti nyanjani kutoka kwa wizara ya elimu.**



**REPUBLIC OF KENYA  
MINISTRY OF EDUCATION  
STATE DEPARTMENT OF EARLY LEARNING AND BASIC EDUCATION**

Telegrams: "ELIMU",  
Telephone: 052-22265  
When replying please quote  
email: [cdebometcounty@gmail.com](mailto:cdebometcounty@gmail.com)  
Ref/CDE/BMT/ED/AUTH/74/VOL.II/42

COUNTY EDUCATION OFFICE,  
BOMET COUNTY,  
P.O. BOX 3-20400,  
**BOMET.**

5<sup>TH</sup> OCTOBER, 2021

NICHOLAS KIRUI  
LAIKIPIA UNIVERSITY  
P.O BOX 1100-20300  
NYAHURURU

**TO WHOM IT MAY CONCERN**

**RE: AUTHORITY TO CONDUCT RESEARCH**

Reference is made to letter Ref: No. NACOSTI/P/21/13197/626053 dated 1<sup>ST</sup> October, 2021 from NACOSTI, requiring the above mentioned Person to conduct a research on "*Diskosi ya Mafunzo ya Tendo la Ndoa Katika Jando Miongoni mwa Wakipsigis, Bomet County*)" which is scheduled to be conducted for the period ending 1<sup>ST</sup> October, 2022.

The purpose of this letter is to inform you that authority has been granted for him to carry out the study in Bomet County, including learning Institutions among others.

Kindly accord him the assistance she requires.

  
COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION,  
BOMET  
P.O. Box 3 - 20400, BOMET  
INDIATSI MABALE  
COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION  
**BOMET COUNTY.**

**CC**

Director General  
NACOSTI  
P.O BOX 30623-00100

**Kiambatisho VI: Idhini ya kufanya utafiti nyanjani kutoka kwa serikali  
gatuzi ya Bomet**

REPUBLIC OF KENYA



**COUNTY GOVERNMENT OF BOMET  
OFFICE OF THE COUNTY SECRETARY**

Telephone: 0202084068  
Email: [countysecretary@bomet.go.ke](mailto:countysecretary@bomet.go.ke)  
When replying please quote Ref and Date:

P.O Box 19-20400  
**BOMET, KENYA**

BC.24/1/1

7<sup>th</sup> October, 2021

**TO WHOM IT MAY CONCERN**

**RE: RESEARCH AUTHORISATION – MR. NICHOLAS KIRUI  
ID NO. 29130060.**

The above named person has been authorized to carry out research on “**Diskosi ya mafunzo ya tendo la ndoa katika jando miongoni mwa wakipsigis**” in Bomet County for a period ending 1<sup>st</sup> October, 2022 by the National Commission for Science, Technology and Innovation vide their letter Ref. No. 626053 dated 1<sup>st</sup> October, 2021.

Any assistance accorded would be appreciated.

  
Simon Langat (Mr.)  
**Ag. County Secretary and  
Head of County Public Service**

